**31 JANUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Nne – Tarehe 31 Januari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo: -

1. Toleo Na. 44 la Tarehe 01 Novemba, 2024;
2. Toleo Na. 45 la Tarehe 08 Novemba, 2024;
3. Toleo Na. 46 la Tarehe 15 Novemba, 2024;
4. Toleo Na. 47 la Tarehe 22 Novemba, 2024;
5. Toleo Na. 48 la Tarehe 29 Novemba, 2024;
6. Toleo Na. 49 la Tarehe 06 Disemba, 2024;

7. Toleo Na. 50 la Tarehe 13 Disemba, 2024;
8. Toleo Na. 51 la Tarehe 20 Disemba, 2024;
9. Toleo Na. 52 la Tarehe 27 Disemba, 2024
10. Toleo Na. 01 la Tarehe 03 Januari, 2025;
11. Toleo Na. 02 la Tarehe 10 Januari, 2025;
12. Toleo Na. 03 la Tarehe 17 Januari, 2025; na
13. Toleo Na. 04 la Tarehe 24 Januari, 2025.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *[The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024]*.

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *[The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024]*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Huduma za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Ngazi ya Wilaya na Tarafa kwa Wastaafu**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka huduma za Mifuko ya Jamii ngazi ya Wilaya na Tarafa ili kuwaondolea usumbufu Wastaafu kwenda kuhakikiwa Mkoani?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa sasa uhakiki wa uanachama unafanyika katika Ofisi za Mifuko zilizopo mikoani na wilayani. Pili, Mifuko imefanya maboresho zaidi katika matumizi ya TEHAMA ambapo kwa sasa mstaafu anaweza kujihakiki mwenyewe kupitia simu janja *(smartphone)* kwa kutumia programu ya kidijitali *(Online Portal)* bila kuhitaji kufika katika Ofisi za Mifuko.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, ukusanyaji wa taarifa ni shirikishi toka ngazi zote zikiwemo ngazi za tarafa, wilaya hadi mkoani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ni mkakati mzuri sana unaoendelea kuwahudumia wastaafu hawa. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya uhakiki kwa ngazi za Halmashauri katika matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha uhakiki huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika majibu, nimesikia kwamba mikoa na baadhi ya wilaya huduma hizo zimekwenda, lakini kuna baadhi ya Wilaya bado huduma hizo za uhakiki hazijafika. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hizo kwenye baadhi ya wilaya zilizobaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali ya Mheshimiwa Mama Tecla kama alivyouliza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, utaratibu wa elimu unaotolewa na mifuko yote ya hifadhi ya jamii chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni endelevu, na tunatoa kwa makundi kwanza ya wafanyakazi katika taasisi za Serikali na wale wote wanaohusika au wadau wanaohusika kwenye mtiririko mzima unaohusiana na mafao ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, kupitia mfumo huo wa kidigitali ambao tunao tumekuwa tukitoa elimu kwa wanachama wenyewe kuwapelekea *message* mbalimbali. Kwa hiyo, jambo hili linaendelea na tulikuwa tumeshafikia zaidi ya wanachama 16,000 ambao tunaendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linafanana na la kwanza. Tumefanya hii kazi katika mikoa, wilaya na mamlaka nyingine zote za Serikali. Kama kuna wilaya mahsusi ambazo Mheshimiwa Mbunge anazo na anaamini kwamba hazijafikiwa katika utoaji wa elimu, namwomba Mheshimiwa aweze kunifikishia tu hapa mezani, nami mwenyewe kwanza kwa sababu ni mama yangu nitamfuata hapo ili niweze kuhakiki ofisini kama kweli hawajaweza kufikishiwa elimu, waweze kufanyiwa hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Ujenzi wa Barabara ya Vwawa – Iganduka mpaka Isalalo**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, ni lini *TARURA* itaanza ujenzi wa barabara ya Vwawa-Iganduka hadi Isalalo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Vwawa - Iganduka hadi Isalalo ipo kwenye mpango wa uboreshaji wa miji na majiji chini ya *Program* ya *TACTIC* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia katika kundi la tatu *(Tier III)*, ambapo kwa awamu ya kwanza barabara yenye urefu wa kilomita 2.0 itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Januari, 2025, wataalam wa usanifu wameanza kuripoti katika miji 18 ya kundi la tatu ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Vwawa kuanza kazi ya usanifu kwa kipindi cha miezi sita. Baada ya usanifu kukamilika tunatarajia kutangaza zabuni za kuwapata Wakandarasi na washauri elekezi kupitia mfumo wa *NeST* ifikapo Juni, 2025 na taratibu za ununuzi zitakamilika Oktoba, 2025 ili Wakandarasi watakaopatikana waanze utekelezaji mara moja ndani ya mwezi huo wa Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami katika Makao Makuu ya Miji ya Wilaya ikiwemo Vwawa, Songwe kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa, majibu yanasema kwamba Serikali itajenga kipande cha kilomita mbili kwa awamu ya kwanza na eneo kubwa ambalo limekuwa na usumbufu mkubwa ni kuanzia Hasanga – London mpaka Mto Nkana, je, Serikali itakuwa tayari katika hii awamu ya kwanza kuongeza kilomita tatu zaidi ili zifikie tano, kusudi lile eneo ambalo lina shida liweze kupitika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa katika barabara hii kutoka Vwawa – Isalalo haitakuwa chini ya mpango huu ambao unausema kuna kilomita zitabaki nje. Je, Serikali itakuwa tayari kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kuhakikisha kwamba hii barabara ambayo ni kiungo muhimu inakamilika hadi Isalalo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi wa wapigakura wake. Naomba nijibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nimemweleza Mheshimiwa Mbunge, Japhet Hasunga kwamba Serikali kupitia mradi huu maalum kabisa wa *TACTIC* utajenga kilomita mbili kwa kiwango cha lami katika jimbo lake, kwa sababu wao kama Vwawa wapo katika kundi la tatu la miradi hii ya *TACTIC*, naomba nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaanza na kilomita mbili ambazo tayari zimeshawekwa katika utaratibu, zinafanyiwa usanifu na zitajengwa kwa kiwango cha lami. Lengo na madhumuni ni kuendelea kuongeza mtandao wa lami ili uweze kufika katika maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ukiacha tu huu mradi wa *TACTIC* ambao unatekeleza ujenzi wa hizi barabara za lami katika Jimbo lake, bado kuna fedha na bajeti ya *TARURA* ambayo inakuja kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, ameongeza bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 275 kwa mwaka mpaka sasa ni shilingi bilioni 710 kwa mwaka. Kwa hiyo, fedha zinazidi kuongezeka kwa ajili ya kuhakikisha maeneo mengi zaidi yanafikiwa na barabara zetu zinajengwa kwa viwango ambavyo vitawezesha kupitika kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya kutoka Ilula – Ibumu ipo katika mpango wa *RISE* wa kujengwa kwa lami kilomita 28. Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa sana wa hizi barabara zetu za Wilaya kiuchumi, pia kufikia huduma msingi kabisa za kijamii, inaendelea kuhakikisha kwamba inaongeza bajeti na inafikia maeneo mengi zaidi kwa ajili ya kujenga na kuimarisha miundombinu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kupitia huu mradi wa *RISE*, barabara hii ya Ilula – Ibumu yenye kilomita 28 itajengwa. Serikali inaendelea na taratibu zake

na zitakapokamilika Mkandarasi atakabidhiwa *site* ili aweze kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Mgombe – Kagera Nkanda, ni barabara inayotumiwa na wakulima kwenda mashambani, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha barabara hiyo imeharibika vibaya mno. Je, Serikali iko tayari kuitengeneza barabara hiyo kwa udharura? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri sana. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua barabara zetu hizi za Wilaya zina umuhimu mkubwa sana wa kiuchumi, lakini zinawawezesha wananchi kufikia huduma muhimu za kijamii. Ndiyo maana Serikali inafanya jitihada dhahiri shahiri kabisa kuongeza bajeti na kufikia maeneo mengi zaidi kwa ajili ya kwenda kuimarisha mindombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kwa kutambua uharibifu mkubwa uliotokea kwenye barabara zetu ambao umetokana na mvua za *El-Nino* mpaka muda huu imeshatumia gharama za shilingi bilioni 88 kwa ajili ya kufikia maeneo korofi yaliyo katika mawasiliano na kuweza kurudisha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha inafika katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo hili ulilolitaja la Kagera Nkanda ili kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa na wananchi wanaweza kuitumia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Protas Daud, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TARURA* ilisaini mikataba mingi mwezi wa Tisa, mwezi wa Saba mpaka leo wakandarasi hawapo *site*. Je, Serikali ina mpango gani kuwarudisha wakandarasi ili waendelee na ujenzi wa barabara kwa mikataba mliyosaini, hasa Jimbo la Igalula na barabara nyingi zimekufa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa hili swali lake zuri kabisa kwa manufaa ya wapigakura wake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imekuwa ikipokea fedha kutoka Wizara ya Fedha kuja *TARURA* kwa ajili ya kuwafikia wakandarasi na kuhakikisha wanapata malipo na kuanza ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, inawapatia fedha hawa wakandarasi na inahakikisha kwamba wanafika *site* kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi. Nimhakikishie hata kwenye Jimbo lake atawaona wakandarasi wanafika *site,* wanaanza kufanya kazi. Serikali inasimamia kuhakikisha hilo linafanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, *TARURA* katika Mji wa Babati hawajapewa fedha tangu mwaka 2024 na barabara ni mbovu sana. Ni lini *TARURA* watapewa fedha hizo waanze kutengeneza barabara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba

nimpongeze Mheshimiwa Pauline Gekul kwa swali hili zuri kabisa lenye lengo la kuhakikisha kwamba wapigakura wake wanapata miundombinu bora kabisa ya barabara zetu hizi za Wilaya. Naomba nimhakikishie kwamba, Serikali italeta fedha kuhakikisha kwamba bajeti ya ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya barabara katika Jimbo lake inapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 53

**Nyongeza za Posho za Madiwani Nchini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza Posho kwa Madiwani kwa kuwa wanafanya kazi kubwa kwenye Kata zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Halmashauri kuwa na uwezo mdogo wa mapato ya ndani ya kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, ilianza kulipa posho kwa Waheshimiwa Madiwani katika Halmashauri 168 kati ya 184 zilizopo. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 63.9 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya kulipa posho za Madiwani.

Mheshimiwa Spika, posho za Waheshimiwa Madiwani bado hazikidhi mahitaji kutokana na Halmashauri nyingi kutokuwa na uwezo wa kulipa kupitia mapato ya ndani. Aidha, Serikali imeendelea kubuni vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri ili hatimaye posho za Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa zilipwe kwa ufanisi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kusema kweli Madiwani wetu hawa wanafanya kazi kubwa sana katika nchi yetu, nasi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa mbele mno kuwatetea Madiwani kupata haki zao zile za posho.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu halmashauri nyingi zina mapato na halmashauri nyingine hazina mapato, naiomba Serikali ifanye uchambuzi wa kutosha kwa zile halmashauri ambazo hazina mapato ya kutosha kwa mwaka huu wa fedha 2025, wawaongezee kipato Madiwani wale kutoka shilingi 350,000 kuwa hata shilingi 500,000, kwa sababu Madiwani wao wenyewe, ukiongeza ni 150,000 tu. Naiomba Serikali kwa bajeti hii iweze kuleta bajeti ya Madiwani kwa halmashauri zile ambazo hazina uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa tuna Sheria Na. 8 na Na. 7, utaratibu ule wa Mwongozo kwa Serikali za Vijiji, Jimbo la Bunda, vijiji na vitongoji vyake vingi havipati mapato yao. Naomba kwenye maeneo ambayo kuna mapato ya Serikali kwenye minada, masoko na kwenye mitera, ile sheria ya kurudisha 20% kwenye vijiji irudishwe kwenye mpango wake wa kila siku ambao ulikuwa unapangwa na Serikali kwa sababu sasa hivi hairudishwi kabisa, lakini kuna maeneo ya minada na masoko ambayo yanatoa ushuru kwenye maeneo hayo. Naiomba Serikali ifikirie jambo hilo kwa upana zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nikawa najiuliza, bado tupo kwenye kipindi cha maswali au ni jambo lingine! Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge ameleta maombi, yapokee maombi yake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nipokee maombi mazuri sana ya Mheshimiwa Getere, nasi kama Serikali tutayachakata na kuweka kwenye mipango kwa ajili ya utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Mkakati wa Usafi Maeneo ya Miji na Majiji**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo ya majiji na miji yanakuwa safi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maeneo ya miji na majiji yanakuwa safi, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutenga bajeti ya kuboresha miundombinu ya uondoshaji taka, ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 22.3 zilitengwa na shilingi bilioni 22.1 zilitumika. Aidha, shilingi bilioni 10.3 zimetengwa katika bajeti ya 2024/2025 kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira katika majiji.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na ushirikishwaji wa mamlaka mbalimbali za umma zenye wajibu kisheria wa kusimamia usafi ikiwemo *TARURA* na *TANROAD*, matumizi ya kampuni binafsi za usafi, uhamasishaji na utoaji wa elimu ya usafi wa mazingira kwa jamii, ushirikishwaji wa wadau katika kuanzisha vituo vya uchakataji na urejelezaji wa taka

pamoja na utekelezaji wa sheria ndogo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa pamoja na jitihada hizi, bado usafi wa baadhi ya miji hauridhishi. Hivyo, itaendelea kuhakikisha usafi unafanyika kikamilifu ili majiji na miji iwe kivutio kwa jamii na wageni pamoja na kuzuia magonjwa yatokanayo na uchafu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, Serikali imekuwa ikijitoa sana kutengeneza miundombinu bora hasa barabara, masoko na vitu vingine, lakini changamoto kubwa imekuja kwenye kumudu kuzitunza barabara hizo ama kutunza masoko hayo. Kwa mfano ukiangalia Dodoma barabara inayotoka Meriwa kwenda mpaka Ilazo unakuta mifereji ni mizuri na barabara nzuri lakini kuna mchanga mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, pamoja na kutoa elimu yote hiyo, je, Serikali haioni haja sasa waweke mkakati wa kutoa elimu ama kuhamasisha wananchi waweze kufanya usafi bila shuruti? Kwa sababu nchi nyingine kwa mfano Uganda…

**SPIKA:** Mheshimiwa umeshajieleza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** …wanafanya usafi usiku na wanaweza kufanya usafi vizuri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wamekuwa wakitoa shilingi bilioni 22.3 hadi shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya usafi. Je, hawaoni haja sasa ya kuhamasisha wananchi waweze kuuza taka kama wanavyofanya nchi nyingine ili waweze kuzi-*recycle* na kuzifanya zile taka zikawa kama mbolea kwa maeneo mengine na wananchi hawa wanaweza wakawa wamepata ajira kwa sababu hizo fedha

wanazozitoatoa zinaweza zikawasaidia na Serikali ikaweza kutoa ajira hasa kwa vijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Grace Tendega kwa maswali yake mazuri sana. Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na majukumu mengine chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, imepewa jukumu la msingi la uratibu na kusimamia masuala ya usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia miradi mbalimbali imekuwa ikifanya hivyo. Ukiacha tu kuelimisha jamii kwa ujumla wake, lakini kuna mradi maalum ambao upo chini ya *TARURA* kupitia mradi wa *RISE* ambao unaitwa *CBRM (Community Based Routune Maintainance).* Mradi huu ni wa jumla ya dola za Kimarekani 350.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unashirikisha vikundi vya kijamii kusafisha na kurekebisha barabara, yaani kuzibua mifereji, kufyeka katika barabara, kufyagia barabara, kuhakikisha kwamba miundombinu yote ya kupokea taka na miundombinu ya barabara kwenye mifereji ile maji yanapopita inaweza kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, hii inakuwa ni namna mojawapo ya kushirikisha jamii katika kutunza mazingira pamoja na jamii husika kupata ajira kwa kutunza mazingira. Huo ni mradi mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kuhusiana na suala zima la *recycling.* Serikali inafanya hivyo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna mradi maalum kabisa wa *DMDP II*. Mradi huu unakwenda kugusa siyo tu ujenzi wa miundombinu ya barabara, bali ni pamoja na masoko na madampo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu, teknolojia ya kufanya *recycling* itatumika kwa maana sasa taka zinakuwa ni rasilimali ambayo inaweza ikamletea kipato Mtanzania, kwamba maana auze taka ziweze kuwa *recycled* na kutengeneza bidhaa nyingine ambazo zinaweza zikawa zina manufaa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mawanzo ya Mheshimiwa Mbunge ni mazuri sana na yanaendana na mikakati ambayo Serikali tayari inayo ya kuhakikisha kwamba inatunza mazingira; inatunza mazingira ya barabara zetu, mifereji na miundombinu mingine yote, pamoja na kuhakikisha kwamba miji na majiji yetu yanakuwa yana usafi ambao unatakiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Esther Midimu naomba sasa swali lake namba 55 lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Subiri Mheshimiwa mpaka utambuliwe kwanza, ndipo unaomba sasa kuuliza swali.

Haya, swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu litaulizwa na Mheshimiwa Minza Mjika.

Na. 55

**Ujenzi Kituo cha Afya Sanga Mwalugesha – Maswa**

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Sanga Mwalugesha, Wilaya ya Maswa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2023/2024 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 1.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kwa ajili ya ukarabari wa hospitali pamoja na ujenzi wa Vituo viwili vya Shishiyu na Badi. Aidha, ujenzi na ukarabati wa hospitali ya wilaya pamoja na vituo vya afya umekamilika na vinatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati zilizokidhi vigezo ikiwemo Kata ya Sanga Mwalugesha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Binza ni kata ambayo ni kubwa sana, ina wakazi zaidi ya 21,000 lakini haina kituo cha afya. Wananchi wale wamejitahidi, wana eneo kubwa sana ambalo ni zaidi ya hekari 15, lakini Serikali haijajenga. Je, ni lini watajenga kituo cha afya kwenye hiyo Kata ya Binza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Minza Mjika kwa swali lake zuri sana. Serikali katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya uwekezaji wa jumla shilingi bilioni 916 katika kuimarisha huduma za afya msingi, kwa maana ya kwenda kuendeleza miundombinu, kununua vifaa na vifaa tiba lakini pia kutengeneza rasilimali watu kwa ajili ya kutoa huduma hizi za afya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali mpaka wakati huu imeshajenga jumla ya vituo vya afya 601 katika kipindi cha miaka minne tu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kufikia maeneo yote yale ambayo ni ya kimkakati na yana vigezo, kata zote ambazo zina vigezo vinavyohitajika kujenga vituo vya afya vitafikiwa kwa awamu ili kuhakikisha kwamba miundombinu na huduma hizi za afya msingi zinaweza kuwafikia wananchi na zinaweza kuwasaidia kupata huduma bora ya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati katika Kata ya Mkunga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sababu Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa huduma hii ya afya msingi, na kwa sababu 75% ya jumla ya Watanzania wote wanatengemea kupata huduma ya afya katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya msingi ikiwemo vituo vya afya, nimhakikishie kuwa Serikali inaendelea na mikakati ya kuleta fedha kufikia maeneo mbalimbali kwa ajili ya kujenga vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika jimbo lake katika mwaka huu wa fedha zitaletwa jumla ya shilingi milioni 250 za kuanza kujenga miundombinu ya awali ya kituo cha afya cha kimkakati katika eneo ambalo wataliteua. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kata hii aliyoitaja ndiyo eneo la kimakakati katika jimbo lake, Serikali inaleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, mwaka 2024 Wizara ya TAMISEMI ilituletea fomu hapa Wabunge wote tukajaza vituo vyetu vya kimkakati kwenye majimbo na mpaka sasa hivi kwenye maeneo hayo wananchi wakafanya sherehe kubwa sana kulingana na changamoto za kiafya ambazo wanapata kwenye maeneo hayo. Je, Wizara ya TAMISEMI hawaoni kuwa kuna umuhimu wa kutupa tarehe maalum, kwamba ni lini vituo hivyo vitajengwa kwenye jimbo langu Kituo cha Kata cha Ivuna na Wabunge wenzangu waliokuwa wametaja kwenye maeneo yao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali zuri kabisa hili la Mheshimiwa Condester Sichalwe. Kwanza naomba nimhakikishie kwamba Serikali ina nia thabiti ya kujenga vituo hivi vya afya vya kimkakati katika kila jimbo; na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha zitaletwa jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga miundombinu ya msingi katika vituo vya afya ambako Waheshimiwa Wabunge mliainisha maeneo ya kimkakati ya kujenga. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Mheshimiwa Mbunge Condester Sichalwe kwamba wananchi wetu tuendelee kuwaambia washerehekee. Mkakati wa Serikali wa kuleta fedha hizi kwa ajili ya kujenga vituo vya afya hivi vya kimkakati kila jimbo upo palepale. Lini? Ni mwaka huu wa bajeti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Nkasi, Kata ya Sintali hakuna Kituo cha Afya, hivyo wananchi wanalazimika kufuata huduma mbali. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Sintali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika,

nampongeza sana Mheshimiwa Sylivia Sigula kwa swali lake zuri kabisa kwa maslahi ya wananchi, hasa ukizingatia kwamba huduma za afya msingi ni huduma zinazotarajiwa na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina nia na madhumuni ya kuyafikia maeneo mengi zaidi kwa kupeleka fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya kutolea huduma za afya msingi. Tayari Waheshimiwa Wabunge wote walishajaza fomu za kuainisha maeneo ya kimkakati katika majimbo yao kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika jimbo na eneo hili alilolitaja, kama ni miongoni mwa maeneo ya kimkakati, basi fedha zinakuja, shilingi milioni 250, kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya hicho cha kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majimbo yetu yana ukubwa tofauti, kwa mfano Jimbo la Hanang tuna kata 33 na mahitaji ni makubwa, je, Serikali ipo tayari kupeleka fedha kwenye Kata ya Hidet na Balangdalalu ili vituo vya afya viweze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Hhayuma kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa sana wa huduma za afya msingi, inafanya uwekezaji mkubwa wa kuhakikisha inaimarisha huduma hizi za afya msingi katika maeneo yote. Hata kwenye jimbo lake la Hanang Serikali inakusudia kuendelea kufanya uwekezaji kwa

kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya msingi ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea kufanya hivyo kupitia Serikali Kuu pamoja na mapato ya ndani ya halmashauri kujenga vituo vya afya, kuimarisha kujenga zahanati na kuimarisha huduma za afya msingi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, tayari katika majibu ya awali niliainisha kwamba Serikali katika mwaka huu wa fedha italeta jumla ya shilingi milioni 250 katika kila jimbo kwa ajili ya kuanza kujenga miundombinu ya vituo vya afya. Nimhakikishie kwamba fedha hizo zitakuja.

Mheshimiwa Spika, bado tunaendelea kuzihimiza Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kupitia mapato ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu hii muhimu katika sekta ya afya pia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa kituo cha afya Mbaya na kwa sababu amejibu kwamba vituo vyote vitapatikana, nashukuru kwa majibu hayo ya jumla.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itakamilisha maboma ambayo yamejengwa na wananchi katika Jimbo la Busokelo, hususan Kata ya Kambasegela, Kisegese, Lupigi na Mpombo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Atupele Mwakibete kwamba Serikali inatambua kuwa wananchi baada ya kuhamasika walichangia

kwenye maendeleo ya nchi kwa kuanza kujenga maboma katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ina dhamira ya dhati kabisa ya kuunga mkono jitihada hizi ambazo zimeanza kuonyeshwa na wananchi, kwa wao wenyewe kuanza kujitolea, na Serikali itaziunga mkono. Tayari kuna fedha ambazo huwa zinaletwa na zinatengwa kupitia bajeti ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, Serikali itaendelea kutenga fedha na kuzileta kwa ajili ya kuunga mkono jitihada nzuri kabisa za wananchi za ujenzi na kuendeleza miundombinu katika sekta ya afya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata katika jimbo lake jitihada hizo zitaendelea kufanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya Serikali aliyoyatoa. Nimeona nisimame ili nimfungulie, maana ameshahojiwa maswali mengi sana. Yale yote aliyoyajibu tumeongea na Wizara ya TAMISEMI. Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya CCM, tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya vituo vyote hivyo ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amevisema.

Mheshimiwa Spika, fedha hiyo inaenda sambamba pamoja na maboma ambayo wananchi wamechagia kuyajenga kwa upande wa elimu pamoja na afya. Tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha kutoa fedha. Kwa hiyo, ndani ya mwaka huu wa fedha, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tutaanza utekelezaji na ukamilishwaji wa maboma ambayo yalishajengwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha ahsante sana kwa majibu yako, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Haya, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Kuondoa Tope Bwawa la Kalemawe – Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tope lililojaa katika Bwawa la Kalemawe – Same?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha inaondoa tope lililojaa katika Bwawa la Kalemawe – Same ikiwa ni pamoja na kukamilisha kazi ya usanifu wa kina na kuandaa gharama kwa ajili ya ukarabati wa bwawa hilo kwa kuondoa tope, kukarabati utoro wa maji, kujenga msingi wa tuta na tuta la bwawa.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetenga fedha, shilingi bilioni moja, ambapo ukarabati umepangwa kufanyika katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2024/2025, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kazi hii ya kutoa tope katika Bwawa hili la Kalemawe imechukua miaka mingi sana na hivyo kuathiri kazi za kiuchumi za Wilaya ya Same hasa Jimbo la Same Mashariki kwa upande wa uvuvi na umwagiliaji, je, Waziri anaweza kuniambia kwamba anakadiria kazi hii itachukua muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Same wanataka wawe na uhakika kwamba kweli kazi hii inafanyika, je, Serikali iko tayari kunisaidia nipate andiko hili la usanifu wa kina ili niweze kuwa na ushahidi kwamba kweli kazi hii itakwenda kufanyika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika jibu la msingi kwamba kazi hii imepangwa kufanyika katika robo ya nne ya mwaka huu wa fedha, tunaendelea kumwambia Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira. Wizara inaendelea kupambana kuona namna ambavyo tunakamilisha kazi hii na kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kuondokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunataka tuwaridhishe wananchi ambao ndio wanapata changamoto kubwa ya kuenea na kuwepo kwa tope katika bwawa hili, na kwa kuwa tunataka tumpatie nafasi Mheshimiwa Mbunge cha kwenda kuzungumza kwa wananchi, tupo tayari na tutampatia hayo maelezo au hiyo taarifa ili naye aweze kujiridhisha na kazi iweze kuendelea, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Hili swali limeulizwa hapa Bungeni mara nyingi sana, na majibu yanayotolewa na Serikali ni haya haya. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kitu kimoja, naomba leo anambie ni lini atakwenda kuliona lile Bwawa la Kalemawe ili wananchi waamini kwamba Serikali iko *serious*? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama Anne Kilango kwa kumwahidi kwamba mara tu baada ya kukamilika kwa Bunge hili, nitahakikisha kwamba tunafuatana pamoja kwenda katika hilo eneo ili kuona changamoto na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi wa eneo hilo, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Ongezeko la Magugu Maji Ziwa Victoria**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, Serikali inafahamu ongezeko la magugu maji Ziwa Victoria na zipi athari za Magugu hayo na mpango wa kuyadhibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafahamu ongezeko la magugu maji katika Ziwa Victoria ambayo yanasababisha athari za kimazingira, kiuchumi na kijamii ikiwemo kupungua kwa oksijeni kwenye maji ambayo

huzuia mzunguko wa hewa na mwanga wa jua na hii husababisha vifo vya samaki na viumbe wengine wa majini. Uharibifu wa mifumo ikolojia na bioanuai ya Ziwa Victoria, huathiri maeneo ya mazalia ya samaki, shughuli za uvuvi na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua jitihada mbalimbali kuhakikisha inadhibiti magugu maji katika Ziwa Victoria ikiwemo kuandaa na kutekeleza Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kukabiliana na Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019/2029 ambao unatoa mwongozo wa namna ya kuzuia, kuingia na kuenea kwa viumbe vamizi na una mipango endelevu ya kushughulikia viumbe vamizi waliopo na wale wanaoweza kuingia.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutoa elimu na kuwajengea uwezo wananchi wanaoishi karibu na Ziwa namna ya kujitolea katika kazi za kutokomeza na kuenea kwa magugu maji kila yanapojitokeza, ikiwa ni pamoja na kung'oa, kukausha na kuchoma magugu maji; na kuendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kudhibiti uharibifu wa mifumo ikolojia ndani ya Ziwa Victoria, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na kukiri ukubwa wa tatizo la magugu maji kwenye Ziwa Victoria. Kwa kuwa ni dhahiri kuwa magugu maji yanaongezeka Ziwa Victoria wala hayapungui, na ni dhahiri kuwa huo mpango mkakati wa 2019/2029 anaouzungumzia ni aidha umeshindwa au haupo, mimi kama Mbunge kwa miaka 10 nimekuwa humu, lakini sijawahi kuona tathmini ya aina yoyote inafanyika juu ya ongezeko la magugu maji. Ni lini Mheshimiwa Waziri atafanya tathmini kuonesha ukubwa wa tatizo wa sasa ulivyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba athari kubwa ya magugu maji ni kupungua kwa samaki. Sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa samaki kutokana na mazalia ya samaki kuendelea kupotea na pia,

kuweka zuio la boti kwenye maeneo mbalimbali. Sasa ni njia gani mbadala ya haraka ambayo Serikali inafanya ili kuokoa Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kanyasu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba hii ni tathmini na ninataka nimwambie kwamba tathmini hii inaendelea, kwa sababu jambo la uwepo wa viumbe vamizi hasa magugu maji siyo jambo la kusema tunafanya leo, ni jambo ambalo limeenea takribani katika vyanzo vingi vya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia maeneo ya kule Ziwa Jipe na maeneo mengine, bado changamoto hii ipo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa aendelee kuwa na subira, bado tunaendelea kufanya tathmini. Kweli, tunakiri kwamba zipo athari kama tulivyoeleza katika jibu la msingi. Tathmini hii itakapokamilika, tutakuja kumweleza yeye na tutalieleza Bunge lako hili ili liweze kujua namna ambavyo tumefikia katika kuhakikisha kwamba tunapambana na changamoto kubwa ya uwepo wa magugu maji.

Mheshimiwa Spika, zipo juhudi kadhaa ambazo tumezichukua kama Serikali ili kuona tunaweza tukapunguza ama kuondoa kabisa changamoto hii kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira, Wizara ya Maji na *Lake Victoria Commission* na halmashauri mbalimbali ambazo ndani yake kunapatikana hii. Kwanza, tumeendelea kutoa elimu kwa maeneo mbalimbali tukiwa na lengo kwamba, ikiwezekana hata wananchi wenyewe waone namna ya kuanza kupunguza hii changamoto.

Mheshimiwa Spika, kingine tumeanza kusimamia sheria kwa sababu kinachoonekana, kuna baadhi ya mambo yanafanyika

ambayo ndiyo yanayosababisha hasa pengine kuenea kwa haya magugu maji.

Mheshimiwa Spika, kikubwa, Serikali tunaendelea kutafuta fedha ili kuona namna ambavyo tunaondoa kabisa changamoto ya uwepo wa magugu maji kwa sababu imekuwa ni athari kubwa kwanza kwenye shughuli za uvuvi, na hata shughuli za kiusalama wa wananchi. Inafika wakati wanyama wakali wanatoka kwenye magugu wanakuja kwenye mitaa kusababisha athari kwa wananchi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2023 timu ya Kitaifa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ilitembelea Ziwa Babati na Ziwa Tlawi katika Mkoa wa Manyara. Je, ni lini taarifa ya hiyo timu itarudi kwa ajili ya utekelezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba timu hiyo ilikwenda baada ya Mheshimiwa Mbunge kuleta hapa taarifa ya changamoto zilizokuwepo kule. Tukaunda timu ili kuona namna ambavyo tunaweza tukasaidia kuondoa magugu maji na changamoto nyingine zilizopo hapo. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, taarifa hii italetwa na itawasilishwa kwake ama itawasilishwa kwa maeneo husika ili wananchi pamoja na viongozi wa eneo hilo waweze kupata taarifa kamili ya utekelezaji wa timu hii, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Sheria Kabambe ya Kudhibiti Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Sheria kabambe kudhibiti uharibifu wa mazingira nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na kutatua changamoto mbalimbali za kimazingira nchini, Serikali imetunga na inatekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ambayo inasimamia masuala yote yanayohusiana na mazingira nchini Tanzania. Sheria hii imeweka msisitizo wa udhibiti wa uharibifu wa mazingira kwa kukataza uchafuzi wa maji, hewa, na udongo kupitia kemikali za viwandani, kilimo, na shughuli nyingine za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, aidha, imeweka msisitizo kwa miradi yote mikubwa kwamba ni lazima ifanyiwe tathmini ya awali ya athari za mazingira kabla ya mradi kuanza ili kuepuka uharibifu wa mazingira. Pia, sheria inahimiza wananchi kuhamasishwa kushiriki katika uhifadhi na usimamizi kupitia elimu, sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa, na mipango ya uhifadhi wa mazingira, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri kiasi ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Sheria za mazingira kwa wale wanaokosa au kuharibu kutokana na sheria hii wamekuwa wakipewa adhabu ya kulipa faini. Je, Serikali ina mpango gani kuchukua baadhi ya makosa ya uharibifu wa mazingira kuwa makosa ya kijinai?

Mheshimiwa Spika, nchi jirani ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, niseme tu, ni Kenya, tayari wana Mahakama ya Mazingira. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mahakama ya Mazingira ambayo kwa wenzetu imefanya vizuri zaidi katika kudhibiti uharibifu wa mazingira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nollo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna watu wanachafua mazingira na wanapochafua mazingira zipo hatua ambazo zimeelezwa kwenye sheria hii, sheria ambayo kwa sasa ndiyo tumeanza mchakato wa kuanza kuifanyia marekebisho kwenye baadhi ya vifungu.

Mheshimiwa Spika, tumeona wazo la kwenda kwenye Mahakama, *of course,* tutalichukua twende tukalifanyie kazi tuone linavyowezekana, lakini zaidi kwenye jambo la sheria za mazingira tumeona bora tuende zaidi kwenye maridhiano pamoja na kutoa maelekezo na kutoa onyo, fidia, faini ikiwezekana hata kuifungia kabisa ama kuzuia shughuli zisiendelee.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua sasa hivi mazingira yamekuwa ni biashara. Sasa ikiwa kila anayechafua mazingira tunasema tunampeleka Mahakamani, tunaweza tukafika mahali hata Mheshimiwa Mbunge mwenyewe tukamburuza huko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa kwamba jambo hili tumo katika mchakato wa kufanya mabadiliko madogo ya Sheria ya Mazingira Sura 191 ili hata hayo mapendekezo aliyoyapendekeza yaweze kuwemo kwenye sheria yetu hii, likiwemo suala zima la uwepo wa Mahakama ya Mazingira Tanzania, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mikakati gani wa kuweza kuimarisha sheria ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na meli baharini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeanza, ama tumekuwa na mchakato wa kufanya marekebisho madogo ya Sheria ya Mazingira Sura 191. Miongoni mwa mambo ambayo tunataka tuhakikishe kwamba tunayafanyia kazi ni jambo la uchafuzi wa vyanzo vya maji ikiwemo jambo la uchafuzi wa masuala ya mazingira kwenye maeneo ya bahari.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa, itakapokamilika sheria hii, hayo mambo ambayo ameyashauri na amependekeza yawemo, basi tutahakikisha kwamba yanakuwemo ili kuendelea kunusuru mazingira, hasa mazingira ya Bahari, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara ya Afya, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mbunge wa Dar es Salaam…

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Bonnah Kamoli…

**SPIKA:** Mheshimiwa, subiri utambuliwe kwanza. Kwa niaba ya Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 59

**Madaktari Wanaozuia Maiti kwa Sababu za Madeni**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa madaktari wanaoendelea kuzuia Maiti kutokana na deni la matibabu kinyume na maelekezo ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, maiti huwa zinazuiliwa na uongozi wa hospitali zetu na wala siyo suala la madaktari. Katika maeneo ambayo tumefanya ufuatiliaji ili kuchukua hatua za kinidhamu kwa viongozi husika, tumebaini ndugu wa marehemu ndio waliokataa kufuata utaratibu uliowekwa kwa nia ya kuzuia hoja za ukaguzi. Badala yake, ndugu hao walikimbilia kulalamika kwenye vyombo vya habari na kwa viongozi, hasa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilishatoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Waraka Na. 1 wa Mwaka 2021 wa kutozuia maiti na kuweka utaratibu wa kulipia gharama za matibabu na madeni ya miili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa matamko haya na nakala hizo za kutokuzuia maiti katika hospitali zinasemwa mara nyingi sana hapa Bungeni, lakini ukienda kwenye utekelezaji haipo kama Mheshimiwa Naibu Waziri

unavyoongea, je, Serikali inatoa tamko gani la wazi kabisa kwa wananchi ambao wanashindwa kupata maiti zao kwa wakati? Naomba nipate tamko hilo toka kwa Mheshimiwa Waziri hapa leo na litekelezwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kuanzia aliyeuliza swali, pamoja na mama yangu aliyeuliza kwa niaba kwa sababu kwa kweli amekuwa akifuatilia wananchi hasa wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kila wakati amekuwa akija kwetu kwa matatizo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe maelekezo kwamba, kwa haya maelekezo nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaanza kuchukua hatua kali kwa wanaohusika. Pia, nawaomba wananchi ambao wanakutana na matatizo hayo wakubali kufuata zile taratibu ambazo wanapewa na wataalamu wetu kwa sababu hizo taratibu zisipofuatwa, hapa ndani mtakuja kuhoji pia kwa hoja za ukaguzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kushindwa kuchukua maiti hutokana na vifo vinavyotokea ghafla. Juzi tulisikia kauli ya Mkuu wa Mkoa akieleza alivyomjibu mjamzito ambaye hakuwa na vifaa vya kujifungulia. Wakati mwingine kukosa hivyo vifaa hupelekea maambukizi wakati wa kujifungua na mwanamke kuchelewa kujifungua inaweza kupelekea mauti.

Mheshimiwa Spika, ni nini kauli ya Serikali kwa wanawake wanaoshindwa kupata vifaa vya kujifungua, lakini kwa viongozi ambao walipaswa kuwasaidia kuja na kauli za kuwakatisha tamaa, akimwambia aende mume wake akamsaidie kujifungua? Nataka kujua kauli ya Serikali kwa sababu ndiyo mambo yanayosababisha vifo na watu kushindwa kuchukua maiti zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba yeye ni Mbunge na ni mwanasiasa. Wakati mwingine anaweza akawa anazungumza watu wakakata sehemu ndogo sana ya mazungumzo yake halafu wakapotosha hali halisi ya ambacho alikuwa anasema.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba suala alilolizungumzia ni nyeti mno. Suala la akina mama na mambo mengine ya dharura tunatoa maelekezo mahususi. Kwanza, kwa hospitali za *private* pia za umma, kwamba mama na mtu yeyote wa dharura akija ni lazima kwanza apate huduma, siyo suala la kuulizwa fedha au kufanya nini. Huduma kwanza, fedha baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye hili eneo la akina mama na watoto tunajua sisi wenyewe tumepitisha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa, lakini kwa mwaka ukipiga gharama za kuwatibu akina mama na watoto ni shilingi bilioni 227 na sisi kwa huduma zote tumetenga shilingi bilioni 200.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kunakuwa na hatua mbalimbali zinazofanywa ili ku-*balance* hizo hela. Kwa sababu anapokwenda mke wa Dkt. Mollel, ni wakati gani unatambua huyu ni mke wa Dkt. Mollel amejifungua? Huyu ni wa nani na tunao watu wengi kule. Unakuta mtu huyo huyo hana bima, hana chochote, lakini anachangia harusi shilingi milioni moja, bali ikifika suala la mke wake kujifungua, hana hizo fedha, anataka asaidiwe bure.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mwendelee kutuvumilia, lakini mjue Serikali kwa mwaka juzi tu ilitumia shilingi bilioni 661 kwa eneo la msamaha tu. Serikali imekuwa ikifanya hivyo, lakini wote tukubaliane, kupanga ni kuchagua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetoa Waraka kwa Marehemu ambao ndugu zao hawana uwezo waweze kutolewa, je, Serikali haioni ipo haja ya kutupa sisi wawakilishi wa wananchi Waraka huo ili tuweze kuwaelimisha wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Serikali iko tayari kuwapa Waraka, lakini pia kuwaomba kuwaelimisha wananchi wawe tayari kufuata zile taratibu ambazo zimewekwa. Kwa sababu kule kwenye hospitali zetu zote kumewekwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ili tuweze kukwepa zile hoja za ukaguzi, kwa sababu tusipopata hivyo, watu wanaweza wakatumia mwanya huo na kusema kwamba wamesamehe, kumbe fedha za umma zimetumika vibaya.

**SPIKA:** Kwa hiyo, huo Waraka watapewa Waheshimiwa Wabunge?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kabisa na nitahakikisha Jumatatu tunauleta, tutagawa kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetoa kauli, Waraka na matamko lakini bado suala la kuzuia maiti linaendelea. Kwa nini Serikali isituletee sheria ili anayezuia maiti ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge anavyowahudumia wananchi na hasa wanawake kwenye eneo la mkoa wake. Hata hivyo, kama nilivyosema, tatizo kubwa tuliloona baada ya

kufuatilia, siyo kwamba watumishi wetu hawakubali kuachia maiti, ila wananchi wanakataa kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali. Naomba Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu tunaenda kwenye suala la Bima ya Afya kwa Wote, huduma ya afya kwa wote itakuwa suluhisho ya hili tatizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu. Kuna mwingine aliyesimama? Mbona watu mnanong'ona! Ahaa ni la kwake huyu? Ahsante sana, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Utoaji Mimba Usio Salama**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, watoto wa kike wangapi na wanawake wangapi walioathirika na utoaji mimba usio salama nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024 idadi ya wanawake na wasichana waliopata changamoto ya kuharibikiwa na mimba na kupata huduma katika vituo vya huduma za afya ni kama ifuatavyo: -

(i) Wanawake na wasichana 181,071 ambao walipatiwa huduma na kuruhusiwa kama wagonjwa wa nje *(outpatients);*

(ii) Wanawake na wasichana 32,512 ambao walipatiwa huduma wakiwa wamelazwa *(inpatients)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024, wanawake 92 walipoteza maisha kutokana na changamoto mbalimbali zinazosababishwa na kuharibika kwa mimba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA**: Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ni nini mkakati wa Serikali kutoa elimu ili kupunguza vifo vya wanawake wanaotoa mimba au mimba zinazoharibika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Baadhi ya wanawake ambao wamekuwa wakibakwa wamekuwa wakipata mimba ambazo hawakuzitarajia, ni nini kauli ya Serikali kutokana na kadhia hii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa kweli hata akiwa anatusimamia kwenye Kamati za Afya amekuwa akilisimamia eneo hili na suala zima la afya ya mwanamke.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, mkakati wa Serikali ni endelevu, tumekuwa tukitoa elimu kwa kutumia vyanzo mbalimbali lakini mkakati mwingine ni kupeleka vituo karibu zaidi na wananchi. Kama ambavyo mnajua, kwa mwaka huu tu, Serikali yetu, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejenga vituo zaidi ya 480 ili kupeleka huduma hizi karibu na wananchi na wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, Bunge hili na Watanzania waendelee kufuata maelekezo ambayo yametolewa, na tushirikiane pamoja kutoa elimu. Mheshimiwa Mbunge, nakuhakikishia Wizara ya Afya tutajipanga kutoa elimu zaidi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la akina mama kubakwa na kupata mimba, nafikiri linahitaji zaidi elimu ya saikolojia baada

ya hilo jambo kutokea. Pia, linahitaji sisi kulinda hayo maovu yasiendelee kutokea. Sisi tuwe mabalozi kwenye jamii kuhakikisha eneo hili la wanawake kunyanyaswa na kubakwa, haya mambo hayatokei kwenye jamii yetu. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba matumizi ya *P2* yanaelezwa vizuri ili wasichana wetu wasije wakaathirika baadaye kwa kukosa kupata watoto? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa 100% kwamba kumekuwa na matumizi mabaya kwenye eneo la *P2*. Hata hivyo, tayari Serikali imeshaanzisha kampeni maalumu inayosema, "Holela holela itaku-*cost*" ikilenga kuelezea matumizi mabaya ya holela holela kwenye dawa zote ikiwepo eneo hili la kutumia *P2*.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwaasa wananchi na wasichana wetu, pia nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuhimiza matumizi mazuri ya dawa pamoja na hili eneo la *P2* kwenye mikutano yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, *P2* ni nini? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni zile dawa za kuzuia mimba, wengine wanaweza wakafanya bahati mbaya ikatokea kwamba hawakutumia kinga, basi anakimbilia kutumia *P2* kabla ya masaa 72. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, wanawake wanaopoteza maisha ni Watanzania na ili tumalize tatizo, ni lazima tulijue tatizo. Napenda kufahamu, Wizara imefanya

tathmini na kugundua nini kinasababisha utoaji wa mimba usiokuwa salama? Nashukuru kwa nafasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hili suala ni *sensitive* na sisi linatutesa sana kwa maana ya kwenye vituo vyetu. Hata hivyo, linaleta gharama kubwa kwa sababu kwanza anayetoa mimba anazidiwa, na akifika hana hata shilingi kumi. Kwa hiyo, ni gharama kubwa sana kwa Serikali kuhudumia eneo hilo na unaona ni zaidi ya wananchi 180,000 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunachosema ni kwamba ni mimba ambazo hazikupangiliwa, maana yake tuna kazi kubwa sana ya kuendelea kuhimiza uadilifu kwenye jamii yetu na hasa kutoa elimu kuanzia *level* ya *primary* na *secondary*. Pia, akina mama wakati mwingine inatokea ana mimba ambayo anajua siyo ya mume wake sasa wakati mwingine inatokea mambo kama hayo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itakuja na sheria ya kumlinda mwanamke ambaye amepata mimba isiyotarajiwa, kwa mfano kubakwa au kupata mimba za ndugu, baba na watu wengine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nadhani kwanza swali lake ni zuri sana na ni la muhimu sana; lakini niseme tu kwamba, sidhani kama suala ni sheria. Zipo sheria nyingi sana za kumlinda mwanamke, lakini ni suala la kijamii.

Mheshimiwa Spika, ni suala la jamii yetu kuendelea kuhimizana utu, uadilifu, upendo, na mambo mengine. Kwa sababu tukubaliane tu kwamba hakuna Kanisa wala Msikiti

uliowahi kumuua shetani. Kwa hiyo, shetani bado yupo na anasumbua watu. Tuendelee kupambana. Hata hivyo, ninachosema, tuendelee kusisitizana kumpinga huyo shetani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge, eneo hili kwa kweli ni eneo ambalo sisi kama Wawakilishi inabidi tupeleke ombi upande wa Serikali ili waje wafanye mafunzo maalumu kwa sababu bado katika nchi yetu kutoa mimba ni kosa la jinai. Sasa, pamoja na kwamba ni kosa la jinai, lakini kuna hizo changamoto zinazojitokeza kwa wale wanaotoa mimba na kwa wale ambao mimba zinatoka.

Nafikiri kuna swali limeulizwa hapa kuhusu sheria na mambo kama hayo. Sisi ndio tunaotunga sheria, lakini ni vizuri tukawa na uelewa mpana juu ya eneo hili kabla hatujaanza kushauri kama pengine tubadilishe sheria kwenye maeneo gani.

Kwa hiyo, tutafanya utaratibu mzuri ili tupate nafasi ya kujifunza, kisha tukishawasikia wataalamu, nadhani hapo inabidi wawepo wataalamu wa afya na mambo kama hayo, tuweze kuwashauri wale tunaowawakilisha vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaelekea Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Elimu ya Mlipa Kodi**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kudai risiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na utoaji wa risiti za mauzo na ununuzi wa bidhaa na huduma. Hatua zinazochukuliwa na Serikali ni pamoja na: -

(i) Kutoa elimu elimu ya kodi kwa njia mbalimbali ikiwemo redio, runinga, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho ya biashara ya Kitaifa, Kimataifa na semina;

(ii) Kuwatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao mlango kwa mlango, kutoa elimu inayoainisha wajibu wa mlipakodi kwa *TRA* na wajibu wa *TRA* kwa mlipakodi kupitia mkataba wa huduma kwa mlipakodi;

(iii) Kuanzisha huduma za bure ikiwemo namba za simu za bure zinazowezesha walipakodi kuwasiliana na Ofisi za *TRA* moja kwa moja; na

(iv) Kuanzisha ofisi zinazotembea *(Mobile Tax Offices)* ambazo zinatumika kama ofisi kamili kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi kwa umma na kusajili walipakodi wapya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ni kwa kiasi gani Serikali inatumia teknolojia kusaidia ufuatiliaji wa ulipaji kodi na kudhibiti ukwepaji kodi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuna mpango gani wa kuboresha mfumo wa utoaji risiti kwa kutumia teknolojia rahisi kwa wajasiriamali wadogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Janeth kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Janeth kwa namna anavyohamasisha na kutoa elimu kwa walipa kodi ili nchi yetu ama wananchi washiriki katika kulipa kodi bila shuruti. Pili, naomba uridhie maswali yote mawili niyajibu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya mlipa kodi na kudhibiti mapato ya Serikali. Serikali imeweka msisitizo kuhakikisha kwamba mifumo yote inasomana na siyo tu kusomana, lakini kufanya mifumo iwe rafiki kwa mlipa kodi. Kwa mfano, leo Serikali kupitia *TRA* inatumia *VFD (Virtual Fiscal Devices)* ambayo mfanyabiashara anaweza kutoa risiti kupitia simu yake ya mkononi. Kwa sababu ya mifumo hiyo kuimarishwa, ndiyo tumeona siku hadi siku mapato yanaongezeka kwa kiasi kikubwa sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na jitihada mbalimbali za Serikali kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* hatimaye inafanya vizuri, lakini bado ipo mipaka ambayo haina *scanner*. Je, Serikali ina mpango gani kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kuiwezesha *TRA* fedha ili iweze kununua *scanner* kwenye mipaka mfano Namanga, Horohoro na Holili? Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Subira ambaye ni Balozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge, lakini Serikali imetenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa midaki mbalimbali *(cargo)* na midaki ya vifurushi vidogo vidogo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu wa fedha tutanunua midaki sita na itasambazwa katika maeneo yote aliyoyataja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Ujenzi wa Gati ya Mto Mnyela – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa gati katika Mto Mnyela, kuunganisha Halmashauri ya Mlimba kupitia vijiji vya Ngalimila na Ngombi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya kivuko eneo la Kikove – Ngoheranga ili kuunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba na Malinyi kupitia vijiji vya Ngalimila na Ngombi ambapo ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 11 Desemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Septemba, 2025. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza (a) na (b).

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii gati ikikamilika itahitaji pantoni, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba gati itakapokamilika na pantoni itakuwa pale?

(b) Barabara inayounganisha hiyo gati inayotoka Mpanda kuja hapa Ngalimila, ni barabara ambayo ina mashimo mengi sana, kwa hiyo, haileti mawasiliano pale. Ni nini mpango wa Serikali kuijenga barabara hii ili gati ikikamilika na barabara iwe imekamilika na pantoni iwe pale? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli kwamba pantoni au kivuko ambacho kitakwenda kwenye eneo hili ni kile kilichokuwa kinafanya kazi pale Kilombero baada ya kujenga daraja. Mkandarasi ambaye amekikarabati hiki kivuko ni Songoro, ambapo baada ya kupata hiyo tenda aliona ni rahisi kwake kufanyia katika karakana yake. Kwa hiyo, alikifungua, na tunavyoongea sasa hivi kipo 95% kukamilika kwa matengenezo na atakileta katika eneo ambalo kitafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara kwa upande wa Mlimba na Malinyi, tayari wenzetu wa *TARURA* walishaambiwa kwa kusaidiana na wenzao wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba, wakati maegesho ya kivuko yanakamilika na pantoni iko pale, kuweza kuwepo barabara za kuwasafirisha wananchi kwa upande wa Malinyi na Mlimba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, natambua Serikali ina mpango wa kujenga Barabara ya Garbabi – Mbulu kwa kiwango cha lami na ninatambua pia mnategemea kumlipa mkandarasi ili afanye hivyo; na kwa kuwa, sasa mvua zinanyesha na mkandarasi hana fedha ya kuchonga barabara hii na haipitiki, je, Serikali ina mpango gani wa kumwambia mkandarasi achonge barabara au *TANROADS* – Manyara? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali linahusu kivuko, lakini sasa kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, aliunganisha gati na ujenzi wa barabara inayoelekea kwenye gati. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa hapo liko sawasawa. Mpatie majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge iko na mkandarasi tayari na ameshapatiwa *advance payment*. Namwelekeza tu Meneja wa Mkoa kwa sababu barabara ikishakuwa na mkandarasi ndiye anayekuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba hiyo barabara inapitika. Kwa hiyo, amsimamie ili huyo mkandarasi aweze kurekebisha njia wananchi waweze kupita, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mgodi wa Shanta Singida**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, lini wananchi waliopisha mwekezaji katika Mgodi wa Shanta Kata ya Mang'onyi Jimbo la Singida Mashariki watalipwa fidia?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Shanta Mining Company Ltd* ilianza shughuli za uzalishaji katika Mgodi wa Dhahabu Singida Machi, 2023 kwa leseni Na. 455/2012. Kabla ya kuanza shughuli za uzalishaji, jumla ya wananchi 284 walikuwa wameshalipwa fidia kwenye maeneo yao yenye ukubwa wa ekari 1,655 ambapo familia 26 zilizohamishwa zilijengewa makazi mapya ikiwemo miundombinu muhimu ya maji na barabara na kupewa ardhi yenye ukubwa wa ekari tano kila familia.

Mheshimiwa Spika, pia, jengo la taasisi ya kidini (Msikiti) lilihamishwa kwa kujengewa msikiti mpya. Jumla ya Shilingi za Kitanzania 4,353,897,083.00 zilitumika kabla ya kuanza shughuli za uzalishaji kwenye eneo hilo kwa ajili ya fidia ya ardhi na maendelezo yake pamoja na gharama za ujenzi wa makazi mapya.

Mheshimiwa Spika, zoezi la utwaaji wa ardhi kwenye leseni Na. ML 456/2012 na ML 457/2012 kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za uchimbaji lilianza mwezi Agosti, 2024 na linaendelea katika hatua ya uthamini na ulipaji fidia ambapo zoezi la ulipaji fidia limeanza mwezi Januari mwaka huu wa 2025 na linaendelea kwa yale maeneo ambayo taarifa za uthamini zimeidhinishwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha zoezi la uthaminishaji katika maeneo yote husika linakamilika mapema na kulipa fidia kwa wahusika pamoja na kuzihamisha familia zinazoguswa na shughuli za uchimbaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, sisi Wananchi wa Singida Mashariki, Mang'onyi na vijiji vyake tunashukuru kwamba Serikali baada ya muda sana wameanza kulipa wananchi na

zoezi kwa kweli linaendelea vizuri kwa sababu mimi nipo kule. Hata hivyo, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza upande wa *CSR*.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji alitakiwa kulipa dola 150,000 kwa ajili ya *CSR* kugharamia miradi muhimu ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Sekondari ya Sambaru ambayo ni muhimu sana na watoto wanatembea kilometa 30 kwenda shuleni; na una watoto takribani 72 wamepata ujauzito mwaka jana, 2024. Sasa, mwaka jana kwenye ile shule ilikuwa inatakiwa dola 40,000 ilipwe lakini mpaka leo haijalipwa hata shilingi. Sasa, nataka kufahamu, Serikali ina jitihada gani za makusudi na za haraka kwa sababu mwaka umeshapinduka na mwaka huu inabidi walipe tena *CSR* ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapatiwa hiyo shule ili waache kukaa magetoni? Maana yake pale kuna wachimbaji na wale watoto wana mazingira magumu sana *especially* watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, upande wa rasilimali, tunategemea wananchi wanufaike sana kwenye *CSR*. Sasa, nataka kufahamu jitihada za makusudi na madhubuti za Serikali kuhakikisha wanawalazimisha wawekezaji kuhakikisha wanalipa *CSR* kwa wakati kwa sababu njia rahisi ya Mtanzania kunufaika kwenye uwekezaji ni kupitia *CSR*.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kufahamu, Serikali ina njia gani madhubuti ikiwezekana kuwapiga faini kwa sababu muda unakwenda na unakuta miradi iliyopangwa ya muhimu haijafanikiwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa suala la *CSR* ambayo kampuni husika inapaswa kutoa, kampuni hii imekuwa ikitoa *CSR* kila mwaka, kwa mfano mwaka 2024 walitenga dola 180,000 na mwaka huu wametenga dola 150,000. Kinachogoma ni kwamba wananchi wanaozunguka migodi kupitia halmashauri zao, zinachelewa katika kuibua vipaumbele

na zinachelewa katika kuthibitisha au kuidhinisha ile miradi ambayo imependekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaasa halmashauri zote nchini zinazopokea fedha za *CSR*, waongeze bidii katika kuhakikisha kwamba wanaibua miradi mapema, lakini pia wanaidhinisha ile miradi, maana mingine ina michoro ambayo lazima halmashauri iidhinishe ili iweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa, ninajibu swali lake la pili, kwamba fedha za *CSR* zinawanufaishaje wananchi? Zinawanufaisha wananchi ambao wameshaibua vipaumbele na mwekezaji atatoa zile fedha kwa kadiri alivyokuwa amepanga kuzichangia kwa mujibu wa Kanuni yetu ya *CSR*.

Mheshimiwa Spika, shida inatokea pale ambapo wananchi hawajakubaliana katika vipaumbele, fedha zipo na zisipotumika katika mwaka husika, zinahamishika kwenda mwaka unaoendelea. Ndiyo maana fedha za mwaka 2024 za Shanta, zinaendelea kutumika katika miradi ambayo ilishakubalika kama Stendi ya Igunga, tayari iko kwenye hatua ya upauzi, lakini pia katika kununua trekta la kufanya usafi wa mazingira na la kuzoa taka ambalo limeshanunuliwa liko njiani limeagizwa na baadhi ya vyoo vya shule aliyoisema vimeshajengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fedha hizi zipo na zinaendelea kutumika bila kujali kwamba mwaka wake umepita au la. Ila wananchi waongeze kasi katika kukubaliana kwenye miradi husika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Kuzuia Usajili Holela wa Laini Za Simu**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuzuia usajili holela wa laini za simu mitaani kutokana na utapeli unaoendelea mitandaoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka miongozo ya kusajili laini za simu kupitia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta. Miongozo hii inahakikisha kuwa laini zote zinasajiliwa kwa alama za vidole, hivyo kutokuwepo kwa mianya ya kusajili laini kiholela. Hata hivyo, wahalifu wa mtandaoni hutumia mbinu kwa kuwalaghai mawakala na watumiaji ili laini zilizokwishasajiliwa zitumike kwenye uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TCRA* na watoa huduma za mawasiliano inaendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu kupitia njia zifuatazo: -

(i) Kutoa elimu kwa umma juu ya uhalifu mtandaoni na njia za kujilinda;

(ii) Kuhakiki taarifa za usajili kupitia namba *106#; na

(iii) Kutoa taarifa za uhalifu kupitia namba 15040, ili kuchukua hatua stahiki dhidi ya vitendo vya udanganyifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu, lakini jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri ana-*admit,* kwa maana ya kukubaliana kwamba kuna ulaghai wa upatikanaji wa laini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Waziri atakubaliana nami kwamba, bado vitendo vya utapeli kupitia laini za simu mitandaoni ni kwa kiwango kikubwa sana na yawezekana hata yeye Mheshimiwa Waziri ameshatumiwa namba za matapeli kwamba tuma fedha kwenye namba hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka 10 sasa hivi tunazungumzia suala la utapeli mitandaoni ambao unafanyika kwa mbinu mbili tofauti. Ya kwanza, ni hiyo ya kutuma meseji, ya pili, kuna watu wanaozunguka vijijini wanasema ni mawakala wanaosajili laini, wanawapa simu wazazi wetu, wanaingiza *PIN* kwenye zile laini, ukituma hela kwenye namba ya mzazi, hela inatoka inaenda kwenye maeneo mengine. Huo wizi umekuwa ukifanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa, nina maswali mawili Mheshimiwa Waziri. La kwanza, ni hatua gani imechukuliwa na Wizara kudhibiti hao watu ambao wanalaghai au wanagawa laini kwa watu ambazo zinatumika kwenye utapeli? Kwa sababu ni zaidi ya laini milioni, mimi nimetumiwa, wewe umetumiwa, yule ametumiwa kwa laini tofauti tofauti, Wizara wameshindwaje kudhibiti hilo?

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara inaona mkakati upi ni rahisi wa kuweka vibanda maalumu kwenye maeneo ama wilayani ama kwenye kata ambako huduma hiyo inapatikana ili mwananchi asipate huduma kutoka kwa mtu anayezurura mitaani na baadaye anaishia kutapeliwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Festo Sanga kwa pongezi na kutambua kwamba tunafanya kazi kubwa sana ya kudhibiti. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Mbunge, hii

ni mara ya pili namjibu swali hili. Nilishajibu tena, aliuliza kama swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda sisi kama Serikali tumeshachukua hatua kali sana kupitia *TCRA*. Utakuwa shahidi pia, wimbi la meseji hizi za utapeli zimepungua kwa kiasi fulani, ilikuwa balaa zaidi ya ambavyo ipo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, *TCRA* wanaendelea na namna mbalimbali za kuona kwamba zinadhibiti hizi laini ambazo zimepatikana kwa njia isiyo sahihi. Kwa hiyo, kama Serikali tumeshachukua hatua na kazi inaendelea. Nampongeza sana *DG* wa *TCRA* kaka yangu Bakari, anafanya kazi kubwa na timu yake nzima na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuona kwamba angalau tunapunguza hawa *freelancers* ambao wanapita huko kuona kwamba tunarahisisha kuwafikia wananchi, lengo lilikuwa zuri, hawa vijana waweze kuwafikia wananchi kule ili kuwapunguzia ugumu wa upatikanaji wa laini, lakini matumizi yamekwenda kuwa mabaya. Kwa hiyo, tayari pia tumepunguza sana namna ya hawa *freelancers* kuzagaa huko kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tutaendelea kuhakikisha tunaongeza udhibiti kuona kwamba laini za simu zitapatikana maeneo maalumu kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza kwamba, matapeli ni kweli wapo, nami ni mmoja wa wahanga, wanatumia majina ya viongozi kutapeli watu. Baadhi ya viongozi wengi hasa wa dini wametapeliwa kwa njia hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hiyo namba 15040 ambayo anasema turipoti, tunaripoti kweli na wanakiri kupokea, lakini hatupati mrejesho wa kujua nini kimefanyika baada ya kuwa tumeripoti.

Je, Serikali haioni kwamba inatujengea mazingira magumu katika jamii pale ambapo majina yetu yanatumika kutapeli watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula kwa namna ya ufuatiliaji. Pia ameshakuwa akifuatilia hili kwangu, lakini matumizi ya majina ya viongozi, hili nalo tunaendelea kulifanyia kazi. Taarifa zote mnazotupatia, hata juzi tu hapa nimepokea karibia Waheshimiwa Wabunge watatu wote wananijia na vithibitisho, majina ya baadhi ya viongozi yanavyoendelea kutumika. Tayari nimeshayaripoti *TCRA*, kazi kubwa sana inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, suala la mrejesho wa nini kimefanyika, tutaendelea kusisitizana na Watendaji kuona kwamba wewe uliyeleta taarifa yako, basi uweze kupata mrejesho. Iwe kiongozi, iwe mwananchi wa kawaida, wote waweze kupata mrejesho namna ambavyo suala limeweza kushughulikiwa. Sisi kama Serikali, tutahakikisha hatuweki mazingira magumu ya kuona kwamba jamii inaendelea kutapeliwa kwa sababu siyo jambo jema. Sisi kama Serikali, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha jamii inapata maendeleo na mazingira rafiki ya kuona kila mmoja anakuwa salama akiwa anatumia mtandao wa simu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na shukurani kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, lakini tatizo kwa kweli ni kubwa na ni kwa watu wengi. Mimi hapa leo nikisema ni watu wangapi nchi hii wametapeliwa kwa jina langu, yaani mimi mwenyewe napata hizo jumbe mpaka sasa hivi nimeshachoka na kutoa taarifa. Kwa nini? Kwa sababu nawaza, utapeli nimesharipoti, lakini unaendelea na haya matangazo yao hayawekwi kifichoni, watu wanatangaziwa kwenye sijui mitandao ile ya kijamii: *Facebook* kuna matangazo, sijui *Instagram* kuna matangazo. Huko kote wanatangaza, na wapo wameweka namba za simu, wanapigia watu simu na sasa hivi kuna ile akili nini? Akili mnemba imebadilishwa jina inaitwa sijui akili kufanyaje...?

Mtu anasema umenipigia wewe simu, na ninaongea na wewe. Sasa mimi Spika naweza kumpigia simu mwananchi kwamba nakopesha hela? Lakini ndiyo hivyo watu wanatapeliwa kila siku.

Sasa, sijajua yaani kama Wizara ama ni *TCRA*, kama ni juhudi, basi nchi yetu jambo hili mbona limekuwa kubwa sana! Yaani huko kwingine tunakosafiri hatusikii mambo haya, kwa nini Wananchi wa Tanzania wanatapeliwa kiasi hiki na sisi tuna *TCRA*? Yaani kama shida ni *TCRA*, shida iko wapi ili tuifanyie kazi? Maana utapeli umezidi hasa wa jina langu mimi. Yaani hata sasa hivi ninavyoongea, kuna watu huko wanatapeliwa.

Mheshimiwa Waziri, naona umesimama.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri kwamba tunayo maendeleo makubwa ya teknolojia ya habari na mawasiliano, na maendeleo haya yametokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi kubwa inafanyika. Jana nilipata Waheshimiwa Wabunge wengi wakionesha hata ujenzi wa kasi wa minara ile 758 inafanyika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kila maendeleo yana changamoto. Maendeleo ya ukuaji wa teknolojia yamekuja na watu ambao wanatapeli. Utapeli ulikuwepo, sasa utapeli umekuwa *digitalized*. Ukisoma Taarifa ya Takwimu za Mawasiliano inayotolewa na *TCRA* kwa kila robo ya mwaka, kwa robo ya pili ya mwaka, ni kweli kazi kubwa imefanyika na ukisoma ukurasa wa 40, utapeli umepungua kwa 19% ingawa bado upo.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinafanyika na Serikali? Tarehe 22 Novemba, 2024 Wizara yangu ilikaa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na iko mikakati ilifanyika kwa sababu ili suala mtambuka…

**SPIKA:** Sekunde moja Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu hakukuwa na Mheshimiwa Mbunge mwingine aliyesimama, unaweza kwenda kuketi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Novemba, 2024, Wizara yangu iliratibu kikao cha sekta mbalimbali ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Benki Kuu ya Tanzania kwa sababu miamala ya fedha inasajiliwa na Benki Kuu, Ofisi ya *DPP,* Jeshi la Polisi, kampuni za Simu, *TCRA,* na wadau wengine. Kikao kile kimezaa *taskforce* ya wataalamu ambao imeshaanza kazi, na hivi ninavyozungumza, tumeshakubaliana na Mheshimiwa Bashungwa, mapema mwezi wa Pili tutakaa kikao tena cha *high level* kuangalia njia za kufanya.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo tumeelekeza kampuni za simu ni kutoa elimu kwa sababu ukiangalia utapeli wa aina zote una *element* kubwa ya ulaghai. Kupitia Bunge lako, nawaomba Watanzania, kwa kuwa maendeleo ya teknolojia yanakwenda kwa kasi, na sisi tuongeze umakini. Umakini wa kwanza, hata leo asubuhi kuna mtu nimemsaidia, tusibonyeze *link* ambazo tunatumiwa tukiambiwa ni bahati nasibu, umeshinda, kuna mkopo wa Mheshimiwa Spika au wa kiongozi mwingine.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tusitoe namba zetu za siri pale tunapopigiwa simu na mtu tusiyemfahamu. Namba tatu, ni kuongeza umakini.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako, naendelea kutoa maelekezo kwa kampuni zote za simu, ziendeleze kampeni za kutoa elimu kwa watumiaji wa simu ya kuongeza umakini wa mitandao ya simu. Sisi kama Serikali kama nilivyoahidi hapa, tutaendelea kufanya kazi ya kuhakikisha tunawasaidia wananchi na kupunguza uhalifu huu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kupitia mkutano ule wa tarehe 22 Novemba, 2024 liliahidi kufanya operesheni hasa kwa mikoa ya Rukwa na Morogoro ambapo ukisoma zile takwimu za utapeli wa mtandao, inaongoza kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo, unatusaidia, lakini Waheshimiwa Wabunge na sisi kama sehemu; kuna sehemu ya Serikali, lakini kuna sehemu yetu sisi kama Wawakilishi wa Wananchi. Ni muhimu kuendelea kuwaelimisha wananchi kwamba hakuna fedha za bure zinazopatikana kirahisi namna hiyo. Hakuna mtu atakupa wewe hela hakujui, hajakutana nawe, umetuma tu kitambulisho akaanza kukupa hela, haiwezekani.

Kwa hiyo, nasi ni kazi yetu kuwaelimisha wananchi kwamba huwa hakuna fedha rahisi namna hiyo. Kwa hiyo, hiyo ni kazi yetu lakini upande wa Serikali na wenyewe wachukue hizo hatua kwa wale ambao wanatumia vibaya haya maendeleo ya teknolojia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 65

**Uwepo wa Aina Nyingi za Viuatilifu Kwenye Zao la Korosho**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa uwepo wa aina nyingi za viuatilifu kwenye zao la korosho ni kuwachanganya wakulima?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, viuatilifu mbalimbali vimeidhinishwa katika kudhibiti visumbufu vya zao la korosho kulingana na aina za magonjwa yanayoathiri mimea. Viuatilifu hivyo, vimesajiliwa kwa majina tofauti ya kibiashara bila kuathiri viambata amilifu *(Active Ingredients)* vyenye uwezo wa kudhibiti vimelea na wadudu

waharibifu katika zao hilo. Hivyo, zao la korosho linaonekana kuwa na viuatilifu vingi kutokana na majina ya kibiashara yanayotumika katika usajili.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, *TARI* Naliendele, Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(TPHPA),* Sekretarieti za Mikoa na wasambazaji wa viuatilifu imeendelea kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa viuatilifu, Maafisa Ugani na wakulima kuhusu matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, uhifadhi pamoja na viwango vya uzimuaji *(Pesticide application rate)*, ili kuwezesha ufanisi wa viuatilifu vinavyosambazwa kwa wakulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na kwa namna ya pekee kabisa, nawapongeza Wizara kwa jitihada zao. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliunda Tume iliyokwenda kufanya utafiti kuhusiana na masuala mbalimbali kwenye kilimo, kuna baadhi ya mapendekezo yalitolewa yameshatekelezwa, lakini kuna mapendekezo mengine bado hayajatekelezwa. Nataka kufahamu ni lini mapendekezo yote yaliyotolewa na tume aliyounda Waziri yatafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, aina mbalimbali za viuatilifu vimekuwa vinafanya kazi kwenye maeneo tofauti, na jambo hili limekuwa linaathiri sana wakulima kwa sababu, kutokana na hali ya hewa utakuta viuatilifu vinavyotumika eneo la Masasi vina viambata tofauti kidogo na vile vinavyotumika maeneo ya Tandahimba na kuathiri uzalishaji. Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti na kuelekeza matumizi sahihi ya viuatilifu kutokana na mabadiliko ya tabia nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, Cecil Mwambe,

kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake wa Jimbo la Ndanda na kwa kufuatilia hii taarifa ambayo inatokana na Tume ambayo Mheshimiwa Waziri aliiunda.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika taarifa ya tume, tayari kuna baadhi ya mapendekezo yaliyofanyiwa kazi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, yote ambayo yalipendekezwa na watalaam kwenye ile Tume yatafanyiwa kazi, likiwemo hili la kuangalia vile viuatilifu ambavyo havifanyi kazi katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni kwamba, linaenda kwenye sekta nzima ya mazao yote kwenye viuatilifu na wala siyo korosho peke yake. Kwa hiyo, nimuagize Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mimea Tanzania kwamba, katika yale mapendekezo yaliyotolewa ambayo bado hayajafanyiwa kazi, likiwemo la kufuta leseni kwa wale wenye viuatilifu feki, lifanyike kabla ya mwezi wa Nne mwaka 2025, kabla ya Bunge la Bajeti halijaanza. Kwa hiyo, hili nimeona nilitoe kama maelekezo maalum kwa Mkurugenzi wa Afya ya Mimea Tanzania. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, je, Serikali ina mpango gani wa kununua viuatilifu au viuadudu vinavyozalishwa na kiwanda cha *Plant Bio-Defenders* cha Moshi ambavyo ni salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge anafahamu, nami nilishafika katika hiki Kiwanda cha *Plant Bio-Defenders* ambacho wao wanatengeneza viuatilifu salama kwa kutumia *natural resources.* Serikali tulishakubali kwamba, tutaweka ruzuku katika viuatilifu vile ili viweze kupatikana kwa wakulima wote. Kwa hiyo, mpango ule bado upo, na tunaendelea kuutekeleza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mtwara ambao ndiyo *giant* kwa korosho, magonjwa yaliyozoeleka ni ubwiri unga na kukauka kwa maua. Je, Serikali haioni iko haja ya kuondoa huo utitiri wa dawa unaowachanganya wakulima na kubakiza dawa zake ambazo ndiyo magonjwa yamekuwa yakijitokeza ili korosho iwe na tija? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu katika swali la msingi, ni kwamba; moja, sisi kama Serikali tulishapokea mapendekezo yote na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri aliunda tume kupitia viuatilifu vyote vinavyohusika katika zao la korosho, vikiwemo vile ambavyo havifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alishaelekeza maeneo yote ambayo kuna viuatilifu feki wafutiwe leseni, ili wasifanye biashara katika mnyororo mzima wa mazao hapa chini. Kwa hiyo, nasi tunaendelea kufanya tafiti kuhakikisha kwamba, haya aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge yanaondoka katika maeneo yote likiwemo lile swali ambalo Mheshimiwa Mwambe alikuwa ameuliza hapa kuhusu kwamba, tunawezaje kupeleka viuatilifu kulingana na maeneo husika? Jambo hilo sisi tulishalipokea kama pendekezo na tumekuwa tukiwashauri wataalam kuhakikisha wanafanya hivyo, ili kuondoa hizi adha ambazo zimekuwa zikitokea kila mara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali iko kazini na tutahakikisha hizi changamoto zinaondoka kabisa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji – Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji, Ifumbo, Chunya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026 Serikali, kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, itatenga fedha, kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili kujua gharama halisi za ujenzi wa Skimu ya Ifumbo. Kazi hii ikikamilika taratibu za manunuzi za kumpata mkandarasi, kwa ajili ya ujenzi wa skimu hizi zitafuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Skimu ya Ifumbo ni ya muda mrefu na ilianza toka Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa fedha na mradi huu ulianza, lakini haukufika mwisho. Kwa hiyo, kwa sababu, majibu ya Serikali yanasema itafanya tena upembuzi. Ni lini upembuzi huu utakamilika ili skimu hii iweze kukamilika na iweze kunufaisha wananchi wa Chunya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, tumeweza kufanya upembuzi wa awali na kuweza kugundua mabonde manne mazuri yanayofaa kujenga skimu ambayo inapatikana maeneo ya Sipa, Mafyeko, Luwalage, pamoja na Mkola. Hivyo, tumeandika andiko kuleta Wizarani na kuweza kuomba fedha, kwa ajili ya upembuzi wa kina. Ni lini Serikali itatupatia fedha hizi ili upembuzi wa kina uweze kufanyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge Masache Njelu Kasaka kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Lupa. Nimthibitishie tu kwamba, kwanza tumepanga katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026, upembuzi yakinifu utamilika kwa sababu jambo hili tumeshalipa kipaumbele. Kwa hiyo, aondoe shaka, litakamilika na tutahakikisha tunamtangaza mkandarasi ili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha ambazo wameziomba kwenye maeneo hayo manne, nimeongea na Mkurugenzi wa Tume na amenihakikishia kwamba, tumeweka kwenye bajeti hii inayokuja, yaani lipo ndani ya bajeti. Kwa hiyo, tukishamaliza kupitisha bajeti, maana yake ni sisi kudhibiti hizo fedha ili sasa tukamalize hiyo kazi ili wananchi wake waweze kunufaika na miradi yote ambayo halmashauri imekusudia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ooh, samahani, kumbe kuna Wabunge wamesimama. Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mradi wa Umwagiliaji wa Ngiba ya Ngusero ulishakuwa kwenye bajeti iliyopita. Mradi huo unaanza lini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuko kwenye hatua za mwisho, kama Mheshimiwa Mbunge alivyokuwa ameeleza. Tukishamaliza tu, maana yake tutamkabidhi Mkandarasi *site* ili aweze kufanya kazi. Kwa hiyo, tuko kwenye hatua za mwisho na anafahamu utaratibu wa kazi jinsi Serikali ambavyo tunafanya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Skimu ya Umwagiliaji ya Makware itaanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, natambua kazi nzuri inayofanyika pale Kyela. Kuhusu Mradi wa Makwale na wenyewe tumeshautangaza ili kuhakikisha tunapata Mkandarasi uweze kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, tukae tu mkao tayari, kwani baada ya Bunge kwisha, ninaamini miradi yote ambayo Serikali ilikuwa imepanga kuitekeleza itakuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake ili sasa wananchi waweze kupata matunda kutokana na kazi ya Daktari Samia Suluhu Hassan. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Skimu ya Mawala, Skimu ya Soko na Kimanga Mau, pale kwenye Kata ya Kahe Magharibi na Mashariki zimetengewa fedha kwenye Bajeti ya 2023 na 2024 zile fedha hazikuja na kwa hiyo, ukarabati haukufanyika. Pia, kwenye mwaka 2024/2025 mpaka sasa hivi afisa mhusika anasema iko kwenye ngazi ya manunuzi. Je, itakamilika lini ili tuweze kupata ukarabati wa skimu hizi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Kama alivyouliza Mheshimiwa Kimei, Mbunge wa Vunjo, ni kweli skimu zote alizozitaja ziko katika hatua ya manunuzi. Hatua za manunuzi ni mchakato. Tukishamaliza mchakato wa manunuzi, tunapeleka katika hatua inayofuata ya kufanya *vetting* kupitia Ofisi ya CAG.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza *vetting,* ndiyo tutakwenda katika hatua ya mwisho ya kumkabidhi mkandarasi *site*. Kwa hiyo, kwa sababu ni taratibu, Bunge liliziweka nasi inabidi tuzifuate ili tuweze kukamilisha. Kwa hiyo, tukimaliza hizi taratibu ambazo zina muda wake, maana yake miradi hii itakwenda kukamilika. Kikubwa ni kwamba, ziko kwenye mchakato wa

ukamilikaji ili ziweze kufuata sheria. Kwa hiyo, hili litafanyika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Kutenga Maeneo ya Biashara Njiapanda ya Machame.**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kutenga maeneo maalum ya biashara kwenye Eneo la *NDC,* Kiwanda cha *KMTC,* Njiapanda ya Machame?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati wa matumizi ya eneo la *KMTC* chini ya *NDC* ulikuwa ni kujengwa viwanda mbalimbali, makazi ya wafanyakazi wa viwanda na mahitaji mengine. Kwa sasa, kimejengwa Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Vipuri cha *KMTC* kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 16.

Mheshimiwa Spika, eneo lenye ukubwa wa jumla ya ekari 639 linaandaliwa mpango wa uwekezaji, kwa ajili ya kujenga mji wa viwanda *(Smart Industrial City)*. Mpango huo umewekwa katika Vipaumbele vya Mwaka wa Fedha 2025/2026 vya Sekta ya Viwanda na Biashara, ambapo utahusisha ujenzi wa miundombinu ya msingi ikiwemo barabara, mifumo ya majisafi na majitaka, umeme na *industrial shades* ambapo kukamilika kwake kutawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine, ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na mpango huo mzuri wa kujenga viwanda na miundombinu mingine kutokana na adha kubwa wanayopata wananchi wa Ukanda wa Machame kwenda kufuata bidhaa Moshi Mjini au maeneo mengine, je, Serikali haioni iko haja ya kuweka mji mdogo wa kibiashara ambao bidhaa na vitu vingine vitapatikana Njiapanda ya Machame?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Serikali iliahidi kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Losaa, ili kianze kutoa huduma. Je, ni lini ujenzi na ukamilishaji wa kiwanda hiki utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwa ufatiliaji wa maendeleo ya viwanda katika Jimbo lake la Hai, hasa hilo mahususi la Machame.

Mheshimiwa Spika, ni kweli amekuwa akifatilia kwa umuhimu wa mji huu mdogo ambao unatakiwa kuwa na maeneo ya kufanya biashara ambao upo karibu na eneo la *KMTC*. Kama nilivyosema, Serikali tayari imeshaweka *masterplan,* tumeshamnunua Mshauri Mwelekezi, *City Plan Consultant Ltd,* ambaye atapanga vizuri eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge anataka kwa ajili ya eneo la biashara na tumeshakubaliana tutapanga, ili tuone eneo hilo linakuwa na maeneo ya makazi na huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo maeneo ya kufanyia biashara ambayo ndiyo hasa, lengo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie, katika Mji Mdogo wa Machame kutakuwa na maeneo ya biashara vikiwemo vituo vya mafuta, nakadhalika, ambavyo vitasaidia wananchi wa pale kuweza kupata maeneo ya kufanya biashara katika eneo hilo la *KMTC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la pili la Kiwanda cha Losaa. Tayari Serikali, kupitia Shirika la Kuendeleza Viwanda

Vidogo vidogo *(SIDO)*, tumeshaweka kwenye bajeti ya mwaka huu. Tutapanga mwaka huu ili kwenda kukiendeleza kile kiwanda kidogo, wananchi wa Losaa waweze kunufaika na uwepo wa kiwanda hicho. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Swali lake litaulizwa, kwa niaba yake, na Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 68

**Kutafuta Soko la Asali**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kutafuta soko la asali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mkakati wa kutafuta soko la asali ambao unajumuisha mafunzo ya uzalishaji bora katika mnyororo wa thamani wa asali. Ujenzi wa viwanda vya pamoja *(common facilities)* vya uchakataji bora wa asali, utangazaji wa bidhaa za asali zinazozalishwa nchini katika maonesho ya ndani, kikanda na kimataifa na kujumuisha fursa ya asali ya Tanzania katika majadiliano ya nchi na nchi, kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zimewezesha kampuni ndogo *(SMEs)* 46 zinazozalisha asali kuuza tani 337.3 katika masoko ya nje, hususan soko la Ulaya, ambapo nchi zinazonunua kwa wingi ni Ujerumani, Uholanzi na Poland, ikifuatiwa na Soko la Afrika Mashariki *(EAC);* Kenya, Rwanda na Uganda na katika Soko la *SADC,* ikiwemo nchi ya Botswana. Jumla ya mauzo katika masoko hayo kwa mwaka 2023 yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 2.0.

**SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha shamba la nyuki la mfano kwa ajili ya ufugaji nyuki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha upatikanaji wa zana za ufugaji nyuki kama mizinga na nguo za warina asali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Maige kwa maswali yake ambayo yanalenga kusaidia wananchi katika sekta hii ya asali.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ilishaanza kufanya kazi za kuwasaidia wafugaji nyuki kupata maeneo ya kufugia nyuki ili kupata asali. Mojawapo ni katika Mashamba ya *TFC,* kwa maana ya wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, ambao wana mashamba mengi ikiwepo kule Rufindi, Itigi na maeneo mengine ya Tabora, kule Sikonge, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, yote haya yanalenga kuwasaidia wananchi ili wapate mashamba darasa na maeneo mazuri ya kufugia nyuki ambayo itasaidia kupata asali nzuri. Pia, katika maeneo hayo kuna viwanda vya kukamua asali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika maeneo hayo pia, kuna taasisi mbalimbali ambazo zinatoa mizinga ya kisasa ambayo inasaidia kuvuna asali nyingi kwa maana ya kufuga kisasa nyuki ambao wanatoa asali ya kutosha ili ziwe na tija kwa wafugaji wa nyuki ambao wamelenga kupata uchumi kupitia kuuza asali, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, Swali

lake litaulizwa, kwa niaba yake, na Mheshimiwa Janejelly James Ntate.

Na. 69

**_EAC_ Kuwa na Sarafu Moja**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, utekelezaji wa Azimio la kuwa na Sarafu moja ifikapo 2024 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dennis Londo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DENNIS L. LONDO)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kujibu swali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa imani yake kwangu. Vile vile nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Bunge lako kwa malezi na usimamizi wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Tarimba Gulam, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sarafu ya Afrika Mashariki ni moja ya kati mambo muhimu ya utekelezaji katika hatua za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliojikita katika nguzo nne ambazo ni Soko la Pamoja, Umoja wa Forodha, Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama zilikubaliana kutekeleza mpango wa miaka 10 ili kufikia azma ya Umoja wa Fedha na Sarafu Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ifikapo 2024. Katika kipindi cha miaka 10 kabla ya kufikia umoja wa fedha na sarafu nchi jumuiya zilitakiwa kutekeleza kikamilifu hatua za awali za mtangamano ambazo ni ushirikiano katika soko la pamoja na umoja wa forodha.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuanzisha taasisi muhimu za kusimamia utekelezaji wa umoja wa fedha na kutimiza au kufikia vigezo vya kuoanisha uchumi mpana. Vigezo vya kuoanisha uchumi mpana vilivyokubalika ni kiwango cha juu cha mfumuko kisizidi asilimia nane; kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti kisizidi asilimia tatu ya pato la Taifa; kiwango cha juu cha deni la Taifa kisizidi 50% ya pato la Taifa; na akiba ya fedha za kigeni ya kutosheleza mahitaji ya miezi minne na nusu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako, tathmini ya mwaka 2022 ilionesha kuwa, nchi Jumuiya za Afrika Mashariki bado zilikuwa hazijatekeleza kikamilifu hatua za awali za mtangamano. Aidha, tathmini hiyo ilibainisha kuwa nchi nyingi zilishindwa katika vigezo vya kuoanisha uchumi mpana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania chini ya Uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, hadi sasa Tanzania ni nchi pekee katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyokidhi vigezo vinne kati ya vitano vya kuoanisha uchumi mpana ambavyo vimekubaliwa na Jumuiya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko na changamoto za kiuchumi duniani na uhaba wa miundombinu muhimu, nchi wanachama zimeshindwa kufikia malengo ya kuwa na sarafu moja katika mwaka uliopita 2024. Kutokana na tathmini hiyo, mpango wa awali umehuishwa na muda wa utekelezaji umeongezwa hadi ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na Tanzania imeweza kufikia viwango vya uchumi mpana:-

(a) Je, ni nchi gani nyingize Afrika Mashariki zimeweza kufikia?

(b) Je, kama zipo hizo nchi, kwa nini sasa hizo zisianze halafu nyingine zitajiunga baadaye?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DENNIS L. LONDO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, hakuna nchi mwanachama iliyokidhi vigezo vyote vya kuoanisha uchumi mpana. Tanzania ndiyo pekee ambayo imekidhi vigezo vinne kati ya vitano vya kuoanisha uchumi mpana kama inavyoelekezwa na Ibara ya Sita ya Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya Sita ambayo inahusu uanzishaji wa uchumi mpana, nchi nne ambazo ni Tanzania, Kenya, Rwanda na Uganda ndiyo nchi pekee ambazo zimetimiza vigezo vya kuwa na wastani wa mfumuko wa bei usiyozidi asilimia nane tangu mwaka 2021. Aidha, nchi tatu ambazo ni Tanzania, Rwanda na Kenya ndizo ambazo zimekidhi kigezo cha kuwa na akiba ya fedha za kigeni ambazo zinatosheleza mahitaji ya ununuzi wa bidhaa ambazo zinamudu ndani ya kipindi cha miezi minne na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nchi tatu wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Sudani ya Kusini na Uganda ndizo ambazo zimefikia kigezo cha Deni la Taifa kutozidi 50% ya pato ghafi la Taifa. Hivyo, hakuna nchi mwanachama ambayo imekidhi kigezo cha kuwa na kiwango cha juu cha nakisi

ya bajeti ikijumuisha misaada isiyozidi asilimia tatu ya pato ghafi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo mambo matatu. Jambo la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara wakati anajibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, alimtaja kama Mbunge wa Same.

Huyu ni Mbunge wa Hai. Same ina Wabunge wawili humu ndani; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Dkt. David Mathayo. Kuna Majimbo mawili huko Same Magharibi na Mashariki. Isije ikaonekana amehama Jimbo lake la Hai anaenda kugombea huko. Kwa hiyo, huyu ni Mbunge wa Hai. Kwa hiyo, nafikiri hilo tutalirekebisha vizuri kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge. Katibu inabidi kulifanyia hilo kazi.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni tangazo linalohusu wageni. Tutaanza na wageni wa Spika, (wageni wangu).

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wawili kutoka Jijini Dar es Salaam. Mgeni wa kwanza ni Ndugu Haji Manara, Mkurugenzi wa *Manara TV* na Mwenyekiti wa Manara *Foundation*. *(Makofi)*

Sasa leo makofi kama yamevurugana hivi, kwa sababu zamani yalikuwa yanapigwa ya Simba, baadaye yakawa yanapigwa ya makofi ya Yanga, sasa leo naona yamekuwa machache, sijajua kama Yanga ni wachache humu ndani leo ama namna gani? Yanga wamezidiwa! Haya basi, Simba wasaidieni Yanga kupiga makofi, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa, umeona ni jambo zuri. *(Kicheko/Makofi)*

Ndugu yetu Manara leo ameongozana na mke wake, ndugu Zainabu Bakari ambaye anajulikana kama Zaylisa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine, ndugu yetu huyu anafanya kazi nzuri na hii *TV* yake, lakini ana mchango mkubwa kwenye soka la nchi hii. Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa uchambuzi mzuri wa soka na mambo mengine, na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapo sijamwuliza Mheshimiwa Sanga kama amekuja kwa ajili ya jambo la kesho kama sehemu ya familia ya Yanga ama! Sasa naambiwa kesho atakuwepo kwenye Bunge Bonanza, kwa hiyo, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia ninao wageni wengine, na hawa ni wanafunzi 100 na walimu 20 kutoka Shule ya Msingi Jerusalemu ya KKKT Kimara, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni, tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Pamoja na mambo mengine, shule hii inasomesha watoto wengi zaidi ambao ni watoto yatima kuliko wale ambao wanapelekwa na wazazi wao. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kulipongeza sana sana Kanisa la KKKT Kimara likiongozwa na Mchungaji Mastai kwa sababu linafanya kazi nzuri ya kuihudumia jamii yetu hasa watoto wasiojiweza. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana Bungeni na tunawashukuru kwa kuja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hawa ni wanafunzi na walimu kutoka shule mbalimbali za msingi na sekondari Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 84 wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni walimu wa shule za msingi na sekondari kutoka Jimbo la Ukonga, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ambaye ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni Wawili wa Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi. Hawa ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni Saba wa Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete. Hawa ni Wasaidizi wa Ofisi ya Mbunge, kutoka Jimbo la Busokelo Mkoani Mbeya, karibuni sana. Eeh, Mheshimiwa Mbunge ana kikosi cha wasaidizi. Haya, karibuni sana wasaidizi wa Mbunge. *(Makofi/Kicheko)*

Pia tunao wageni 78 wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, ambao ni Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Arusha Mjini, wakiongozwa na Katibu wao Ndugu Emmanuel Msemwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linahusu Bunge Bonanza litakalofanyika kesho tarehe 01 Februari, 2025. Mnatangaziwa na Mwenyekiti wa Bunge Bonanza, Mheshimiwa Festo Richard Sanga kwamba Bunge Bonanza litafanyika kesho Jumamosi tarehe 01 Februari, 2025 kuanzia saa 12.00 asubuhi kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango kuelekea Shule ya Sekondari ya John Merlin iliyopo Miyuji Dodoma. Michezo mbalimbali ya mashindano na mingine mingi ya kufurahisha itakuwepo.

Bonanza litafanyika kwa mfumo wa ushabiki wa timu za Simba na Yanga. Timu mbalimbali zimealikwa kutoka Azania Benki, Wizara ya Maji, *DUWASA, TRA, NSSF,* TAMISEMI, Chuo cha Mipango, Benjamini Mkapa *Hospital* pamoja na Viongozi wa Yanga na Simba kutoka Makao Makuu. Viongozi wa *TFF, Jogging Clubs* zote za Dodoma na Mashabiki wa Simba na Yanga wa Dodoma na Kauli Mbiu ya Bonanza la Safari hii ni "Utani Wetu ni Umoja Wetu". *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya bonanza, jioni kutakuwa na tafrija ambayo itakuwa na burudani mbalimbali. Kwa hiyo, wote mtakaoshiriki bonanza mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Pia Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kwamba vifaa vya michezo (bonanza hilo) viko tayari kwa kila mchezo unaohusika na mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge, basi tuwatafute wale Makatibu wetu wa Kamati ili watukabidhi vifaa hivi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnahimizwa kwamba kesho ni muhimu kuhudhuria na msisahau kuna maelekezo ya Spika ya kudumu ya Wabunge wote kuwepo hiyo siku ambayo tunakuwa huko tukijihimiza wenyewe kufanya mazoezi, lakini pia kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye mazoezi ili kuondokana na magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, hilo lilikuwa ni jambo la pili. Jambo la tatu, kwa mujibu wa ratiba yetu ambayo tumegawiwa kwa maana ya Orodha ya Shughuli za leo hapa tutaruka namba nne kwanza, tutaanza na namba tano.

Kwa hiyo, nimeona nilizungumze kwa sababu siyo kawaida yetu. Orodha ikishatoka tunafuata ile orodha, lakini sasa tunaweza kuanza na namba tano kisha tutarejea namba nne baada ya kumaliza namba tano.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusoma Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, hee! Leo mbona mmejipanga hivyo? Hii taarifa nilikuwa sina. Ofisi ya Waziri Mkuu haina Waziri? Ama ni Waziri anayehusika? Ama sasa kwa sababu hapa hakuna mazungumzo mpaka useme na kisemeo, aidha niandikie, maana sijaelewa kwa nini anawasilisha Naibu Waziri badala ya Waziri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, imetokea changamoto hapo kwa sababu siyo kawaida Naibu Waziri kuwasilisha Hoja ya Wizara. Kwa hiyo, alipaswa Waziri ndiyo aje awasilishe lakini kama mlivyoona nilikuwa nashangaa hapa, kwa sababu mimi mwenyewe sina taarifa. Yaani nilikuwa naangalia Naibu Waziri kwamba anakuja hapo kukaa kwa sababu ndiyo eneo la kukaa na kwamba anakuja Waziri ambaye ni *caretaker* ama namna nyingine. Sasa aliposimama yeye nikapata kidogo wasiwasi nikataka maelezo.

Sasa nimeambiwa *Caretaker Minister* atakuja kuwasilisha Mheshimiwa Mavunde. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote hapa kushiriki katika huu Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge la Kumi na Mbili na kuniwezesha kusimama

mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi Namba 13 wa Mwaka 2024 *[The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024]*, unaopendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu zilizoainishwa katika sehemu ya pili hadi sehemu ya nne ya Muswada. Vilevile nichukue nafasi hii kuwatakia wote heri ya mwaka mpya wa 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa Kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Rais mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kugombea nafasi ya Urais, Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa

kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Aidha, naishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu na Bunge, Bwana Baraka Ildelphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidani Mwaluko Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Abdallah Hamisi Ulega kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Ashatu Kachambwa Kijaji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Jerry William Silaa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu nawatakia heri katika kutekeleza majukumu yao mapya na ninawaahidi kuendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu wakiongozwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini; Katibu Mkuu, Mary Ngelela Maganga; na Naibu Katibu Mkuu, Zuhura Yunus Abdallah; pamoja na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuahidi kwamba, mimi na ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yote.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bwana Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Kuteuliwa kwa ushirikiano na ushauri wanaotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo. Aidha, kwa kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu, imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta jedwali la marekebiso kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na. 13) wa Mwaka 2024 kama ulivyowasilishwa, unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366 *(The Employment and Labour Relation Act Cap. 366)*

(ii) Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300 *(The Labour Institution Act Cap. 300)*

(iii) Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 *(The Non-Citizen Employment Regulation Act Cap. 436)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namma ambavyo masharti ya sheria mbalimbali yanapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366, ambapo Kifungu cha Nne kinapendekeza kurekebishwa ili kuboresha na kuongeza tafsiri ya baadhi ya misamiati iliyotumika katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati ambayo imetumika katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tisa kinapendekeza kurekebishwa kwa uongeza wigo wa tafsiri ya msamiati *"Senior Management Employee"*. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ufafanuzi wa nafasi ya Mfanyakazi Mwandamizi katika menejimenti kwenye utekelezaji wa haki ya kujiunga katika vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14 kinapendekeza kurekebishwa ili kubainisha aina ya mikataba ya muda maalumu. Lengo la marekenisho haya ni kuongeza wigo wa mazingira ambayo mtu anaweza kuajiriwa kwa mkataba wa kipindi maalumu, ikiwemo mkataba ambao mwajiriwa anaajiriwa kwa muda ili kuendana na ongezeko la wingi wa kazi. Pia, kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi nyingine za msimu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 16A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mazingira ambayo mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuingia katika makubaliano ya namna watakavyofanya kazi katika hali ya dharura inayoweza kuathiri uzalishaji mahali pa kazi. Lengo la maerekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi wa ajira na usalama wa mfanyakazi mahali pa

kazi, kuwezesha uzalishaji na kupunguza athari kwa waajiri wakati wa magonjwa ya milipuko na matukio ya dharura.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mwajiriwa ambaye atajifungua mtoto njiti kwa kujumuisha katika likizo yake ya uzazi muda uliobaki kufikia wiki 40 za ujauzito. Lengo la marekebisho haya ni kulinda ustawi na afya za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati ambao wanahitaji muda wa kutosha wa uangalizi wa mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali katika Muswada, ilipendekezwa muda wa wiki 36 za ujauzito kama ukomo wa mtoto kutimia. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Kamati, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kuongeza muda huo hadi kufikia wiki 40. Vile vile, Serikali ilikubaliana na pendekezo la Kamati la kuongeza muda wa likizo ya baba ambaye atapata mtoto njiti ambapo badala ya likizo ya muda wa kawaida ya siku tatu, atapata siku saba. Mapendekezo haya yamejumuishwa katika Jedwali la Marekebisho la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 34A kinapendekeza kuongezwa ili kumwezesha mwajiri kumpatia mwajiriwa wa likizo bila malipo isiyozidi siku 30. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mwajiriwa kupata likizo bila malipo kutokana na majanga au dharura zinazoweza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayozuia mwajiri kutokuanzisha au kuendelea na shauri la nidhamu dhidi ya mwajiriwa pale ambapo mgogoro huo upo mbele ya Tume au Mahakama ya Kazi. Lengo la merekebisho haya ni kuzuia uingiliaji wa mchakato wa ushughulikiaji wa migogoro inayowasilishwa kwenye Tume au Mahakama ya Kazi na kulinda haki za waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 40 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha fidia kulingana na aina ya mgogoro na ukomo wa chini na wa juu wa fidia inayotolewa kwa mwajiriwa

aliyeachishwa kazi isivyo halali. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mwongozo wa utoaji fidia na kudhibiti utoaji wa fidia kwa kiwango kisicho na uhalisia pale inapothibitika kuwa mwajiriwa aliachishwa kazi isivyo halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 41A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu afua kwa uvunjaji wa mkataba wa ajira ya muda maalum. Lengo la marekebisho haya ni kutoa mwongozo wa utoaji wa fidia kwa mwajiriwa pale ambapo mwajiri atakiuka vipengele muhimu vya mkataba vinavyoweza kupelekea mwajiriwa kuacha kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha 71 kimependekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya utaratibu wa kuanza kutumika kwa mikataba ya hali bora, iliyoingiwa na Wakuu wa Taasisi za Umma. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha masharti ya sheria hii na utaratibu uliowekwa na sheria zinazosimamia Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha vyama vya wafanyakazi kwa pamoja kuingia mikataba ya hali bora na mwajiri au vyama vya waajiri, kwa ajili ya kuanzisha majukwaa ya ushiriki wa waajiriwa mahali pa kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa waajiriwa katika masuala yanayohusu maslahi yao na kuboresha mahusiano eneo la kazi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 86 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa la pande zote katika shauri kuwepo wakati wa usuluhishi na kuzuia mwajiri kuwakilishwa na mwakilishi binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha migogoro kumalizika katika hatua ya usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka ukomo wa muda kuwasilisha mgogoro kwa hatua ya uamuzi baada ya usuluhishi kushindikana. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha migogoro ya kazi inashughulikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 87 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzuia msuluhishi kuamua mgogoro uliopo katika hatua ya usuluhishi na badala yake kubainisha kwamba, usuluhishi umeshindikana. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia utaratibu unaohusika katika usuluhishi na kuondoa ukinzani kati ya usuluhishi na uamuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa mamlaka Tume kurejea shauri na kulisikiliza ambapo mwombaji ametoa sababu za msingi za kutohudhuria awali wakati wa usikilizwaji wa mgogoro. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha haki ya kusikilizwa inalindwa kwa pande zote.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 88 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu utaratibu wa utoaji wa tuzo, ikiwa upande mmoja utakubali madai au sehemu ya madai, utaratibu wa kufanya maombi ya kutengua amri au uamuzi uliofanywa kwa kusikilizwa upande mmoja na wajibu wa mwamuzi kuwataarifu wahusika wa mgogoro endapo atashindwa kutoa tuzo ndani ya siku thelathini. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utaratibu wa usikilizaji na uamuzi wa mgogoro katika Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 94 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kuzuia wahusika wa mgogoro kuwasilisha maombi ya mapitio kwa maamuzi madogo ya Tume isipokuwa kama maamuzi hayo yana athari ya kumaliza mgogoro. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Tume kusikiliza na kuamua migogoro kwa wakati kwa kuzuia taratibu zinazoweza kutumika kusababisha ucheleweshaji usio na tija.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 97 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu utakaowezesha nyaraka za Tume kusambazwa na msambazaji nyaraka wa Mahakama. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa nyaraka zinapelekwa kwa wakati na kwa kutumia utaratibu unaoaminika na wenye uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300, ambapo kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri za baadhi ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati ambayo imetumika katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tisa kinapendekezwa kurekebishwa ili kubadili utaratibu wa vikao vya Baraza kutoka katika utaratibu wa mwaka wa kalenda na badala yake kutumia utaratibu wa mwaka wa fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha vikao vya Baraza vinaendana na kalenda ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kumzuia msuluhishi aliyehusika katika usuluhishi wa mgogoro katika ngazi ya usuluhushi kuamua katika ngazi ya uamuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mgongano wa maslahi katika uamuzi na kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki asili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya utaratibu kwa Mwenyekiti kuongoza vikao vya Tume, na kama hatakuwepo, wajumbe waliopo watateua mjumbe mmoja kuongoza kikao. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa utendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa masharti yanayoruhusu msuluhishi aliyehusika katika usuluhishi wa mgogoro kusikiliza mgogoro huo katika ngazi ya uamuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mgongano wa maslahi katika uamuzi na kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki asili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Tume kumwita tena shahidi ambaye ameshatoa ushahidi ili kumdadisi na kumtaka kutoa ushahidi zaidi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ufanisi kwa Tume katika kuamua mashauri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kurekebisha makosa ya kiuandishi. Vifungu vya 43 na 44 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa cheo cha Naibu Kamishna wa Kazi na kutambua maafisa elimu kazi waliopo chini ya Kamishna wa Kazi kwa lengo la kuendana na muundo wa taasisi unaotumika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha majukumu ya maafisa kazi na kuongeza majukumu ya maafisa elimu kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii na kuendana na muundo unaotumika katika Ofisi ya Kamishna wa Kazi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 45A kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa kwa kuongeza takwa la fedha zinazolipwa katika ufifilishaji wa makosa kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa fedha za Serikali na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mamlaka Jaji Mkuu kwa kushauriana na Waziri kutengeneza kanuni za kusimamia mienendo ya wawakilishi binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu bora wa kusimamia utendaji wa wawakilishi binafsi katika Mahakama ya Kazi na Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 56 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzuia mwajiri kuwakilishwa na mwakilishi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436. Kifungu cha Tisa cha Sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kumtaka raia wa kigeni mwenye kibali cha kazi Daraja A anayekusudia kujihusisha na kampuni nyingine anayomiliki hisa kupata idhini ya Kamishna wa Kazi badala ya kibali kingine cha kazi.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuondoa usumbufu na kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa mwekezaji ambaye ni raia wa kigeni, mara baada ya kupata kibali cha kazi kwa kampuni moja hatahitajika kupata kibali kingine kwa kampuni nyingine atakayomiliki hisa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti ya kuzuia urejeshwaji wa ada ya maombi ya kibali cha kazi. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi kwa waombaji wa vibali vya kazi kuhusiana na ada zinazolipwa wakati wa maombi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha wakimbizi wenye hadhi stahiki kuendelea kufanya kazi bila kubanwa na sharti la ukomo wa muda wa kibali cha kazi. Vile vile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuwezesha maombi ya kuhuisha kibali cha kazi kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kazi angalau miezi miwili kabla ya kwisha kwa muda wa kibali. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na. 13) wa Mwaka 2024, *(The Labour Laws (Amendments) (No. 13) Bill, 2024)* ujadliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (MB), WAZIRI WA NCHI – OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU, AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA KAZI (NA.13) WA MWAKA 2024 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge la Kumi na Mbili; na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na. 13) wa Mwaka 2024 (The Labour Laws (Amendments) (No. 13) Bill, 2024), unaopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tatu (3) zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Nne ya Muswada. Vilevile, nichukue nafasi hii kuwatakia wołe heri ya mwaka mpya 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Rais Mwaka 2025. Pia, nampongeza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuteuliwa kugombea nafasi ya Urais Zanzibar. Pia, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Aidha, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bw. Baraka Ildelphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavukatika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee napenda kumpongeza Mh. Mhandisi Hamadi Yusuf Masauni kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa na Mh. Rais kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mh. Dkt Damas Daniel Ndumbaro kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mh. Innocent Lugha Bashungwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mh. Abdallah Hamisi Ulega kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi, Mh.Ashatu Kachwamba Kijaji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, na Mh. Jerry William Silaa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ninawatakia heri katika kutekeleza majukumu yenu mapya na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu wakiongozwa na Naibu Waziri, Mhe. PatrobasPaschal Katambi, (Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini), Katibu Mkuu Mary Ngelela Maganga na

Naibu Katibu Mkuu Zuhura Yunus Abdallah pamoja na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika aidha, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bw. Hamza Johari na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mbunge wa Viti Maalum) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Riziki Saidi Lulida (Mbunge wa Kuteuliwa) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati hiyo. Kamati hij ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo. Aidha, kwa kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na.13) wa Mwaka 2024, kama ulivyowasilishwa unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 (The Emp/oyment and Labour Re/ations Act, Cap. 366);

2. Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 (The Labour /nstitutions Act, Cap. 300); na

3. Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 (The Non-Citizen (Employment Regulation) Act, Cap. 436).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti ya Sheria mbalimbali yanapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 ambapo kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha na kuongeza tafsiri ya baadhi ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati hiyo ambayo imetumika katika Sheria. Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa tafsiri ya msamiati "senior management employee". Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ufafanuzi wa nafasi ya mfanyakazi mwandamizi katika menejimenti kwenye utekelezaji wa haki ya kujiunga katika vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha aina ya mikataba ya muda maalum. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa mazingira ambayo mtu anaweza kuajiriwa kwa mkataba wa kipindi maalum, ikiwemo mikataba ambayo mwajiriwa anaajiriwa kwa muda ili kuendana na ongezeko la wingi wa kazi, kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo ili kuwajengea uwezo na kufanya kazi nyingine za misimu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 16A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mazingira ambayo mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuingia katika makubaliano ya namna watakavyofanya kazi katika hali ya dharura inayoweza kuathiri uzalishaji mahali pa kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi wa ajira na usalama wa mfanyakazi mahali pa kazi, kuwezesha uzalishaji na kupunguza athari kwa waajiri wakati wa magonjwa ya milipuko na matukio ya dharura.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mwajiriwa ambaye atajifungua mtoto njiti kwa kujumuisha katika likizo yake ya uzazi muda uliobaki kufikia wiki arobaini za ujauzito. Lengo la marekebisho haya ni kulinda ustawi na afya za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati ambao wanahitaji muda wa kutosha wa uangalizi wa mama. Awali, katika Muswada ilipendekezwa muda wa wiki thelathini na Sita za ujauzito kama ukomo wa muda wa mtoto kutimia. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Kamati, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kuongezwa muda huo hadi kufikia wiki arobaini. Vilevile, Serikali ilikubaliana na pendekezo la Kamati la kuongeza muda wa likizo ya Baba ambaye atapata mtoto njiti, ambapo, badala ya likizo ya muda wa kawaida wa siku 3 atapata siku saba. Mapendekezo haya yamejumuishwa katika Jedwali la Marekebisho la Serikali. Kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha mwajiri kumpatia mwajiriwa likizo bila malipo isiyozidi siku thelathini. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mwajiriwa kupata likizo bila malipo kutokana na majanga au dharura zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayozuia mwajiri kutoanzisha au kuendelea na shauri la nidhamu dhidi ya mwajiriwa pale ambapo mgogoro huo upo mbele ya Tume au Mahakama ya Kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia uingiliaji wa mchakato wa ushughulikiaji wa migogoro iliyowasilishwa kwenye Tume au Mahakama ya Kazi na kulinda haki za waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 40 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha fidia kulingana na aina ya mgogoro na kuweka ukomo wa Chini na wa juu wa fidia inayotolewa kwa mwajiriwa aliyeachishwa kazi isivyo halali. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mwongozo wa utoaji fidia na kudhibiti utoaji wa fidia kwa kiwango kisicho na uhalisia pale inapothibitika kuwa mwajiriwa aliachishwa kazi isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 41A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu afua kwa uvunjaji wa mkataba wa

ajira ya muda maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kutoa mwongozo wa utoaji wa fidia kwa mwajiriwa pale ambapo mwajiri atakiuka vipengele muhimu vya mkataba vinavyoweza kupelekea mwajiriwa kuacha kazi. Aidha, kifungu cha 71 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya utaratibu wa kuanza kutumika kwa mikataba ya hali bora inayoingiwa na wakuu wa taasisi za umma. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya Sheria hii na utaratibu uliowekwa kwenye sheria zinazosimamia utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha vyama vya wafanyakazi kwa pamoja kuingia mikataba ya hali bora na mwajiri au vyama vya waajiri kwa ajili ya kuanzisha majukwaa ya ushiriki wa waajiriwa mahali pa kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa waajiriwa katika masuala yanayohusu maslahi yao na kuboresha mahusiano eneo la kazi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 86 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa la pande zote katika shauri kuwepo wakati wa usuluhishi na kuzuia mwajiri kuwakilishwa na mwakilishi binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha migogoro kumalizika katika hatua ya usuluhishi. Vilevile, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka ukomo wa muda wa kuwasilisha mgogoro kwa hatua ya uamuzi baada ya usuluhishi kushindikana. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha migogoro ya kazi inashughulikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 87 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzuia msuluhishi kuamua mgogoro uliopo katika hatua ya usuluhishi na badala yake kubainisha kwamba usuluhishi umeshindikana. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia utaratibu unaohusika katika usuluhishi na kuondoa ukinzano kati ya usuluhishi na uamuzi. Vilevile, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa mamlaka Tume kurejesha shauri na kulisikiliza pale ambapo mwombaji ametoa sababu za msingi za kutohudhuria awali katika usikilizwaji wa mgogoro. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha haki ya kusikilizwa inalindwa kwa pande zote.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 88 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu utaratibu wa utoaji wa tuzo ikiwa upande mmoja utakubali madai au sehemu ya madai, utaratibu wa kufanya maombi ya kutengua amri au uamuzi uliofanywa kwa kusikilizwa upande mmoja na wajibu wa mwamuzi kuwataarifu wahusika wa mgogoro endapo atashindwa kutoa tuzo ndani ya siku thelathini. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utaratibu wa usikilizaji na uamuzi wa mgogoro katika Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 94 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kuzuia wahusika wa mgogoro kuwasilisha maombi ya mapitio kwa maamuzi madogo ya Tume isipokuwa kama maamuzi hayo yana athari ya kumaliza mgogoro. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Tume kusikiliza na kuamua migogoro kwa wakati kwa kuzuia taratibu zinazoweza kutumika kusababisha ucheleweshaji usio na tija.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 97 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu utakaowezesha nyaraka za Tume kusambazwa na msambazaji nyaraka wa mahakama. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa nyaraka zinapelekwa kwa wakati na kwa kutumia utaratibu unaoaminika na wenye uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300, ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri za baadhi ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati hiyo ambayo imetumika katika Sheria. Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubadili utaratibu wa vikao vya Baraza kutoka katika utaratibu wa mwaka wa kalenda na badala yake kutumia utaratibu wa mwaka wa fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha vikao vya Baraza vinaendana na kalenda ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kumzuia msuluhishi

aliyehusika katika usuluhishi wa mgogoro katika ngazi ya usuluhushi kuamua katika ngazi ya uamuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mgongano wa maslahi katika uamuzi na kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki asili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya utaratibu kwa Mwenyekiti kuongoza vikao vya Tume na kama hatakuwepo, wajumbe waliopo watateua mjumbe mmoja kuongoza kikao. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa utendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa masharti yanayoruhusu msuluhishi aliyehusika katika usuluhishi wa mgogoro kusikiliza mgogoro huo katika ngazi ya uamuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mgongano wa maslahi katika uamuzi na kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki asili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Tume kumwita tena shahidi ambaye ameshatoa ushahidi ili kumdadisi na kumtaka kutoa ushahidi zaidi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ufanisi kwa Tume katika kuamua mashauri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kurekebisha makosa ya kiuandishi. Vifungu vya 43 na 44 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa Cheo cha Naibu Kamishna wa Kazi na kutambua maafisa elimu kazi waliopo Chini ya Kamishna wa Kazi kwa lengo la kuendana na muundo wa taasisi unaotumika kwa sasa. Aidha, kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha majukumu ya maafisa kazi na kuongeza majukumu ya maafisa elimu kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii na kuendana na muundo unaotumika katika ofisi ya Kamishna wa Kazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45A kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa kwa kuongeza takwa la fedha zinazolipwa katika ufifilishaji wa

makosa kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa fedha za Serikali na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mamlaka Jaji Mkuu kwa kushauriana na Waziri kutengeneza kanuni za kusimamia mienendo ya wawakilishi binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu bora wa kusimamia utendaji wa wawakilishi binafsi katika Mahakama ya Kazi na Tume, Kifungu cha 56 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzuia mwajiri kuwakilishwa na mwakilishi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436. Kifungu cha 9 cha Sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kumtaka Raia wa kigeni mwenye kibali cha kazi daraja A anayekusudia kujihusisha na kampuni nyingine anayomiliki hisa kupała idhini ya Kamishna wa Kazi badała ya kibali kingine cha kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa usumbufu na kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa mwekezaji ambaye ni Raia wa kigeni ambapo mara baada ya kupała kibali cha kazi kwa kampuni moja hatahitajika kupała kibali kingine kwa kampuni nyingine atakayomiliki hisa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti ya kuzuia urejeshwaji wa ada ya maombi ya kibali cha kazi. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi kwa waombaji wa vibali vya kazi kuhusiana na ada zinazolipwa wakati wa maombi. Aidha, kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha wakimbizi wenye hadhi stahiki kuendelea kufanya kazi bila kubanwa na sharti la ukomo wa muda wa kibali cha kazi. Vilevile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuwezesha maombi ya kuhuisha kibali cha kazi kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kazi angalau miezi miwili kabla ya kuisha kwa muda wa kibali. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka

2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na. 13) wa Mwaka 2024 (The Labour Laws (Amendments) (No. 13) Bill, 2024) ujadliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa spika, NINAOMBA KUTOA HOJA.

Ridhiwani Jakaya Kikwete
WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
……….2025

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri wa Madini ahsante sana kwa wasilisho hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Fatma Toufiq, aje awasilishe maoni ya Kamati kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ye Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba Taarifa hii ya Kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Acts, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu, kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu kuletwa. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo na Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo na ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya mkutano na kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali *(Public Hearing)*, tarehe 15, Januari, 2024 na kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu. Nachukua fursa hii kuwatambua kwa uchache wao kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)*, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*, Vyama vya Wafanyakazi 19 ambavyo vipo nje ya Shirikisho la Wafanyakazi *(TUCTA)* kama vilivyoorodheshwa katika taarifa yetu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)*, Chama cha Wafamasia na Wakunga, na wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 17 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika, na kila Ibara ya Muswada, na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika Ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi, wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Acts, 2024)*, ukiwa umegawanyika katika sehemu nne, na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu, kwa madhumuni ya kuondoa upungufu na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo, kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 *(The Employment and Labour Relation Act, Cap. 366)*;

(b) Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 *(The Labour Institution Act, Cap. 300)*; na

(c) Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 *(The Non-Citizens Employment Regulation Act, Cap. 436)*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu Masharti ya Utangulizi, inajumuisha Ibara ya Kwanza inayohusu jina la Muswada, na Ibara ya Pili inayoelezea marekebisho yatakayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ajira na Uhusianao Kazini, Sura ya 366 *(The Employment and Labour Relation Act, Cap 366)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya tatu hadi Ibara ya 19 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo, ni matumizi ya msamiati mahususi katika tasnia ya kazi. Mathalani, sheria hii inapendekeza kufuta neno '*Sunday*', lililopo katika tafsiri ya neno '*Basic Wage*', na badala yake kuweka neno '*Rest Day*', ili kuainisha kuwa, mshahara wa mwajiriwa hautahusisha malipo ya nyongeza atakayolipwa kwa kufanya kazi siku za mapumziko.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya yameongeza sharti kwenye kifungu kinachohusu haki ya waajiriwa kuanzisha vyama vya wafanyakazi vyenye lengo la kuongeza kigezo cha mfanyakazi wa ngazi ya juu ya uongozi *(Senior Management Employee)*, kuwa itahusisha pia mfanyakazi mwenye mamlaka ya kuajiri, kusimamia nidhamu ya watumishi, au kusitisha ajira ya mtumishi.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza sifa ya watumishi wa ngazi ya juu ya uongozi, na hivyo kwa mujibu wa Kifungu cha 9(2)(c) cha sheria, hawaruhusiwi kuingia kwenye Chama cha Wafanyakazi kinachowakilisha wafanyakazi wasio kwenye ngazi za juu za uongozi wa mwajiri.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyojitokeza katika mapendekezo ni masharti mapya yanayoainisha sifa za mkataba wa ajira kwa muda maalumu *(Fixed Term Contract)*. Moja ya sifa hizo ni mhitimu wa shahada ambaye ameajiriwa kwa lengo la kupata mafunzo au uzoefu wa kazi ili aweze kuajiriwa, endapo mafunzo haya hayazidi miezi 24, na ameajiriwa na mwajiri ambaye shughuli zake zinategemea kupata zabuni.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapendekezo mengine yanalenga kuweka masharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa ya wakati wa mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza, au kutokea hali ya dharura. Kifungu kinaeleza kwamba, kunapotokea mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza au uwezekano wa kutokea kwa mlipuko wa magonjwa hayo, au kunapotokea hali nyingine ya dharura ambayo ina uwezekano wa kuathiri usalama wa watumishi, au kuathiri kazi au uzalishaji katika eneo la kazi, mwajiri na mwajiriwa watakubaliana kuhusu namna nzuri ya kukabiliana na hali hiyo. Makubaliano haya yatapaswa kuzingatia maslahi ya pande zote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine jipya katika Muswada huu ni kuweka masharti kuhusu likizo ya wazazi kwa mtumishi aliyejifungua mtoto kabla ya wakati (mtoto njiti). Kifungu kinaeleza kuwa, mtumishi atakayejifungua mtoto njiti ana haki ya kupewa

likizo ya malipo ya uzazi kutokea tarehe ya kujifungua hadi kufikia kukamilika kwa wiki 36 za ujauzito.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mtumishi huyo ana haki ya likizo ya uzazi ya kawaida itakayotolewa kwa Kifungu Kidogo cha Sita, katika mzunguko wa likizo yake. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mwongozo wa kisheria kuhusu haki za mtoto aliyezaliwa kabla ya muda wake, na mama aliyejifungua mapema zaidi, kwa ustawi wa mama husika na mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, vilevile, marekebisho haya yanalenga kuweka masharti kuhusu likizo isiyokuwa na malipo. Kifungu kinaeleza kuwa, baada ya kupokea maombi ya kimaandishi, na kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye kanuni, mwajiri anaweza kumpatia mtumishi likizo isiyokuwa na malipo kwa muda wa siku zisizozidi 30. Aidha, muda wa likizo isiyokuwa na malipo unaweza kuongezwa kwa kipindi kingine kwa makubaliano baina ya mwajiriwa na mwajiri. Lengo la marekebisho ni kuainisha aina ya likizo na masharti yake, na hivyo kuondoa migogoro baina ya mwajiri na mwajiriwa kuhusu likizo hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu malipo ya fidia kwa mwajiriwa aliyesitishiwa ajira bila ya kuwepo kwa sababu zinazokubalika, na bila kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa. Kifungu kinaeleza kwamba, endapo uamuzi au Mahakama ya Kazi itaamua kuwa usitishwaji wa ajira haukuwa wa haki kwa kutokuwa na sababu au kwa kutokufuatwa kwa taratibu za kusitishwa kwa ajira, maamuzi ya Mahakama yanaweza kuamuru mwajiri kulipa fidia ya ujira usiozidi miezi 12. Vilevile, endapo usitishwaji wa ajira utatokana na sababu za kibaguzi au unyanyasaji, fidia isiyozidi miezi 24.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyopo sasa, endapo mwajiri atamwachisha kazi mwajiriwa wake bila ya kuwa na sababu za msingi za kutokufuata taratibu, atamlipa fidia ya ujira usiopungua miezi 12.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa ina maoni kuwa, marekebisho yanayokusudia kuweka ukomo wa kulipwa ujira

usiozidi miezi 12, yawekwe pale tu itakapothibitika kuwa mwajiri alikuwa na sababu za msingi za kusitisha ajira ya mwajiriwa, ila alikosea tu kwa kutokufuata taratibu za kusitishwa kwa ajira. Ushauri huu ulitokana na uzoefu katika nchi nyingine ikiwemo Afrika Kusini, pamoja na maamuzi mbalimbali ya Mahakama za Tanzania, ambayo yamekuwa na mtazamo kama Kamati.

Mheshimiwa Spika, kifungu kinachohusu adhabu ya kusitisha ajira kwa sababu ya kibaguzi au unyanyasaji, kitakuwa na maoni kuwa, mapendekezo haya yawekewe adhabu ya chini ya fidia isiyopungua miezi 12, au ya juu isiyozidi miezi 24, kwa lengo la kukidhi dhana iliyokusudiwa na kuwekwa adhabu kubwa kwa kila kosa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanahusu kuweka masharti ya mwajiri kutokuanzisha au kuendelea na shauri kinidhamu dhidi ya mtumishi, endapo suala hilo limepelekwa kwenye tume au Mahakama kwa ajili ya uamuzi. Lengo la marekebisho ni kuondoa mgongano katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu ili kuzingatia utawala wa kisheria, ambapo Mahakama ndiyo chombo chenye mamlaka dhidi ya mtu mwingine katika utoaji wa haki kwa mujibu wa Ibara ya 107(A) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 *(The Labour Institutions Act, Cap. 300)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 20 – 33 ya Muswada. Katika sheria hii, yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo ni pamoja na kuweka sharti la kuwaondolea wasuluhishi mamlaka ya kuamua mgogoro wa kikazi ambao walishiriki katika hatua za usuluhishi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano kwa kimaslahi katika utatuzi wa migogoro, ili kuendana na msingi wa utawala na sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuweka masharti kuwa, sheria hii au Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini haitazuia mtu

kuteuliwa kwa vyeo viwili kwa Pamoja; kuwa msuluhishi na kuwa mwamuzi. Lengo la marekebisho ni kuakisi marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 23, ambapo licha ya mtu kuteuliwa katika vyeo viwili, hatakuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri ambalo alikuwa msuluhishi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanaweka masharti kuwa, fedha itakayolipwa kama faini kutokana na amri ya Afisa Kazi baada ya kufifilisha kosa, italipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, fedha hizo zinaweza zisilipwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, endapo Waziri mwenye dhamana ya fedha ataelekeza vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuchochea usimamizi wa utii wa sheria na kuongeza usimamizi wa fedha za Umma. Vilevile, marekebisho mengine yanahusu kumwezesha Jaji Mkuu baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya kazi, kutunga kanuni zinazohusu taratibu zilizotumika Mahakama Kuu ya Kazi, na kusimamia mienendo ya wawakilishi binafsi wanaowakilisha wadaawa Mahakama Kuu ya Kazi na Tume.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanaweka masharti kwa mwajiriwa anayehusika na shauri lililopo kwenye Tume au Mahakama Kuu ya Kazi, kuwa na uhuru wa kuchagua mwakilishi binafsi wa kumwakilisha kwenye shauri hilo. Lengo ni kuendeleza misingi ya haki kwa kuwa na mwakilishi anayeaminika na mwajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 *(The Non-Citizens Employment Regulation Act, Cap. 436)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 34 – 37 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii ni pamoja na kuweka masharti yanayomtaka mgeni aliyepewa kibali cha kufanya kazi Daraja A, pale ambapo mgeni huyo akihitaji kushirikiana na kampuni nyingine kwa kuwa

mwanahisa, anatakiwa kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna wa Kazi. Lengo la marekebisho ni kudhibiti matumizi mabaya ya vibali vya kufanya kazi nchini, vinavyotolewa kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuweka masharti kuwa, kibali cha kufanya kazi kitakachotolewa kwa mkimbizi kitakuwa hai kwa muda wote ambao mtu huyo ataendelea kuwa na hadhi ya ukimbizi kwa mujibu wa sheria husika. Lengo la marekebisho ni kuwatofautisha wakimbizi na wageni wengine wa kawaida nchini, katika masharti ya vibali vya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, marekebisho haya yanalenga kuweka masharti kuwa, maombi ya kuhuisha kibali cha kazi yatawasilishwa kwa Kamishna wa Kazi, angalau siku 60 kabla ya kwisha muda wake wa matumizi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika kushughulikia maombi ya kuhuisha vibali vya kufanya kazi nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada uliowasilishwa na mtoa hoja. Aidha, baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo, na kupendekeza kufanyike marekebisho ya msingi ili kuboresha Muswada huu, kama ilivyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 *(The Employment and Labour Relation Act, Cap. 366)*, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha Nne kinachohusu tafsiri ya maneno. Muswada unapendekeza kufanya tafsiri ya neno "*Basic Wage*" kwa kufuta neno "*Sunday*", na badala yake kuweka neno "*Rest Day*". Kamati ilijadili kwa kina suala hili, pamoja na kupata maoni ya wadau waliofika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka kuwa, licha ya kuongezwa kwa neno "*Rest Day*"

kubakia kwenye mapendekezo ya marekebisho, vilevile neno "*Sunday*" libaki katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa, kwa kawaida, ni utamaduni wa Kitanzania kuwa Siku ya Jumapili ni siku ya mapumziko, ambapo jamii za Kitanzania hukutana kwa ajili ya masuala mbalimbali ya kijamii. Endapo itaondolewa, itakuwa na athari na kufuta utaratibu huo, kwa kuwa mwajiri atakuwa na hiari ya kumchagulia mwajiriwa wake siku ya kupumzika.

Mheshimiwa Spika, aidha, ilikubalika kuwa, neno "*Rest Day*" ambalo linapendekezwa kuongezwa kwenye sheria litafsiriwe ili kuepuka mwajiri kuwa na tafsiri yake, na hivyo kupunguza mgogoro kati ya mwajiri na mwajiriwa. Serikali imezingatia ushauri huo katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 9(6)(B) kwa kuongeza tafsiri ya maneno "*Senior Management Employee*", kuwa litahusisha pia mwajiriwa mwenye mamlaka, au anayeweza kuruhusiwa kuajiri kusimamia nidhamu ya mwajiriwa, au kusitisha ajira ya mwajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri kuwa, neno "*Discipline*" linaweza kuwa na utata kwa kuwa kwenye Sekta Binafsi watumishi ambao sio sehemu ya *management* kama vile wasimamizi *(supervisors)* kwenye maeneo mbalimbali ya uzalishaji, hususan viwandani, wanayo mamlaka ya kusimamia nidhamu za waajiriwa walio chini yao, isipokuwa watumishi hao siyo sehemu ya watumishi wa ngazi ya juu ya uongozi kwenye kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kampuni ilishauri kuwa, neno "*Discipline*" lifutwe katika tafsiri hiyo, kwa kuwa neno hilo linawagusa wafanyakazi wa kawaida. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kufanya marekebisho kwenye kifungu husika kama ilivyoshauriwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Sita inafanya marekebisho ya Kifungu cha 14(1) cha Sheria kinachoainisha sifa za mkataba wa ajira ya muda maalumu. Kamati ilishauri kuwa, Kifungu cha

14(1)(b)(ii) kimetumia neno *"Employed"* na kuwa na maoni kuwa, kutumika kwa neno hilo kunaweza bila kukusudia kuwakatiza waajiri kuendelea na programu za mafunzo au kutoa nafasi za mafunzo kwa wahitimu, kwani kinaweka mahitaji ya ziada ya kufuata sheria nyingine kama vile Sheria za Kodi na Kanuni za Hifadhi ya Jamii. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kufuta kifungu hicho katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Saba inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria, ili kuweka sharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa wakati wa mlipuko wa magonjwa, au kutokea hali ya dharura. Kamati ilikuwa na maoni kuwa, kiongezwe kifungu kidogo ambacho kitashughulika na kutoa mwafaka pale ambapo pande zote mbili zitashindwa kukubaliana.

Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja ya Kamati ni kuwa, suala la kukubiliana lina uwezekano mkubwa wa kugusa maslahi ya mwajiriwa, hivyo kuweka uwezekano wa kutokuafikiana. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kuweka sharti kuwa, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* ndiyo chombo kitakachofanya uamuzi endapo mwajiri na mwajiriwa watashindwa kukubaliana kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nane inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 33 ya Sheria, kinachohusu likizo ya uzazi *(Maternity Leave)* ili kuweka masharti kuhusu likizo ya uzazi wa mtumishi aliyejifungua mtoto njiti. Kamati ilipendekeza kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mama aliyejifungua watoto njiti, kutoka wiki 36 hadi wiki 40.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata maoni kutoka kwa wataalamu wa afya, na inaamini kuwa kiafya mtoto anakuwa yuko vizuri zaidi ikifikia wiki ya 40. Hivyo, ikiwa mtoto atazaliwa njiti, mama mzazi atapaswa kupewa likizo ya utangulizi hadi pale atakapofikisha wiki 40. Hali hii itamsaidia kuweza kumhudumia vizuri mtoto njiti. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kufuta wiki 36, badala yake kuweka wiki 40 katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara hiyo, vilevile Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kinachoweka masharti ya kutoa likizo ya siku saba kwa baba aliyepata mtoto njiti *(Paternity Leave During Pre-Mature Birth of the Child)*. Msingi wa hoja hii ni kutokana na ukweli kuwa, kumekuwa na matukio katika hospitali zetu, ambapo baba mzazi hufanya jukumu la kuwapa joto watoto njiti *(Kangaroo Method)*, ambao bado wapo katika uangalizi wa hospitali.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kufanya maboresho katika kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Katika Ibara ya 11 inayorekebisha Kifungu cha 40 cha Sheria kumwezesha mwamuzi au Mahakama kuamuru mwajiri kumlipa mwajiriwa fidia ya ujira usiozidi miezi 12, kama adhabu ya kusitishwa kwa ajira bila ya kuwepo sababu zinazokubalika, na bila kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa. Kamati ilijadili kwa kina kuhusu mapendekezo hayo, ambayo pia yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na wadau waliofika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa sheria iliyopo sasa inajitosheleza, kwa kuwa inaweka malipo ya fidia ya ujira usiopungua miezi 12, kwa mwajiri kutenda kosa la aina hiyo. Hata hivyo, Serikali ilieleza kuwa ilikusudia kuweka ukomo wa miezi ya fidia ili kuzuia matumizi mabaya ya madaraka kwa baadhi ya waamuzi, kwa kutoa fidia ya miezi mingi bila ya kuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano na Serikali ilikubalika kuwa kifungu hicho kirekebishwe kwa kuwekewa kiwango cha chini na kiwango cha juu cha fidia ili kuondoa dosari ambazo Serikali ilizieleza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilikuwa na maoni kuwa adhabu ya kumwachisha mtu kazi inaweza kuwekwa ukomo usiozidi miezi 12 endapo mwajiri alikuwa na sababu za kumwachisha mwajiriwa kazi, lakini hakufuata taratibu kwa

makosa yanayomtaka kufuata utaratibu, jambo ambalo Mahakama ya Tanzania imeshatoa maamuzi ya aina hii. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kufanya marekebisho katika mapendekezo husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 11 Kamati ilikuwa na maoni kwenye kifungu kinachohusu adhabu ya kusitisha ajira kwa sababu za kibaguzi au unyanyasaji. Kamati ilikuwa na maoni kuwa mapendekezo haya yawekwe adhabu ya chini ya fidia isiyopungua miezi 12 na ya juu isiyozidi miezi 24.

Mheshimiwa Spika, lengo la Kamati ilikuwa ni kukidhi dhana iliyokusudiwa na kuondoa mazingira yanayompatia mwamuzi au Mahakama kuweza kutoa fidia ya miezi atakayoona inafaa ili mradi haizidi miezi 24. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kufanya marekebisho katika jedwali lililowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 86(6) cha Sheria ambacho kinaweka masharti ya ulazima wa mlalamikaji kuwepo wakati wa usuluhishi wa shauri alilolifungua Tume hata kama ana mwakilishi wake au wakili. Kamati ilishauri kuwa kiwekwe kifungu kitakachowezesha walalamikaji wenye sababu maalumu za kutokuwepo wakati wa usuluhishi waruhusiwe kuwakilishwa au na wawakilishi wao au wakili wao kufanya usuluhishi kwa niaba yao. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 inarekebisha Kifungu cha 88 cha sheria ili kuwezesha mwamuzi kutaarifu wadau hawa kuhusu kushindwa kutoa uamuzi wake katika siku 30 na kwamba ataeleza sababu pamoja na kutaja tarehe nyingine ya uamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano na Serikali, ilikubalika kuwa kifungu hiki kirekebishwe kwa sharti la kuwataarifu wadau hawa kifanyike kwa njia ya maandishi "*shall notify parties in writing*". Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho yaliyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 inarekebisha kifungu cha 97 cha sheria kinachoweka sharti linalompatia mpelekaji wa nyaraka za Mahakama mamlaka ya kuwasilisha nyaraka chini ya sheria hii. Kamati ilipendekeza kifungu hiki kirekebishwe kwa kuongeza utaratibu wa kusambaza nyaraka za Mahakama za kazi kwa njia ya barua pepe *(e-mail)* ikizingatiwa kuwa Mahakama imeanza kutumia mfumo wa kidijiti katika kazi yake. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kuweka mapendekezo hayo katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 *Labor Institution Act Cap 300,* katika marekebisho ya sheria hii Kamati ilikuwa ina maoni kama ifuatavyo: Ibara ya 35 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha Tisa cha sheria kinachoweka masharti yanayomtaka mgeni aliyepewa kibali cha kufanya kazi Daraja *A* pale ambapo mgeni huyu akihitaji kushirikiana na kampuni nyingine, kwa kuwa mwanahisa atatakiwa kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna wa Kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kifungu kiboreshwe kwa kuwa mabadiliko yanayopendekezwa yanaweza kuwa na athari hasi kwa sekta ya usimamizi wa kodi, kwani yanaweza kurahisisha mikakati ya kukwepa kodi kama vile uundaji wa makampuni kwa lengo la kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri maboresho kama ifuatavyo:- *By adding the following words, "after presenting the task clearance certificate from the relevant authority regarding tax administration", after the word "commissioner" appearing in the proposed subsection three*. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri kwa ujumla, pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri kwa ujumla ambao ni vyema Serikali ikauzingatia kwa kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na masuala ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iboreshe Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ambacho kitazuia mazingira ya mwajiri kulipa waajiriwa mshahara bila kupitia benki zilizosajiliwa nchini. Changamoto iliyopo ni waajiriwa wengi wa sekta binafsi wamekuwa wanalipwa mishahara bila kutumia mifumo ya benki na kupelekea Serikali kukosa takwimu sahihi za waajiriwa wanaolipwa viwango stahiki katika mfuko rasmi. Aidha, utaratibu huu umekuwa ukitumika kuwakandamiza waajiriwa wakati wa malipo ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta maboresho yanayotoa likizo ya uzazi kwa mama aliyejifungua njiti. Aidha, Kamati inashauri Serikali namna ya kufanya maboresho katika sheria hii ili kuruhusu akina mama wanaojifungua watoto wenye mahitaji maalumu kama vile usonji, vichwa vikubwa, mgongo wazi, mdomo sungura, matundu kwenye moyo, seli mundu na kadhalika waweze kupewa likizo maalumu ya uzazi pindi wanapojifungua.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira ya Wageni Sura 436 ili kuweka sharti la kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kurithisha ujuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika maboresho yanayopendekezwa kwa umuhimu wa mchango wao kushughulikia Muswada huu. Naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Mwandishi Mkuu wa Sheria za Serikali, Ndugu Onorius Njole pamoja na Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kufanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA KAZI WA MWAKA 2024 *[THE LABOUR LAWS (AMENDMENTS) ACT, 2024]* - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI
1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 (*The Labour Laws (Amendments) Act, 2024*), kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023,

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Saba, Kikao cha Tisa kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 08 Novemba, 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na

Maendeleo ya Jamii ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2. Namna Uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika

**Mheshimiwa Spika**, hatua za kuufanya muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 24(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuhusu madhumuni na sababu za Muswada kuuleta huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 15 Januari, 2024 na kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kwa uchache wao kama ifuatavyo: -

1. Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*);
2. Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);
3. Vyama vya Wafanyakazi 19 ambavyo vipo nje ya Shirikisho la Wafanyakazi TUCTA ambavyo ni TUPSE, TASIWU, IGWUTA,

NUMET, DOSHITWU, TPTU, MPETU, TMDPWU, TAROTWU, TAREWU, CHAWAMATA, JOWUTA, TAFIMU, TAWUTA, PRIPPAWUTA, CHAKUHAWATA, FIBUCA, THTU na TADWU;

4. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
5. Chama cha Wafamasia na Wakunga; na
6. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu. Mnamo tarehe 17 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila Ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika Ibara zilizo onekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tulikujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *[The Labour Laws (Amendments) Act, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu Nne (4) na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tatu (3) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 (*The Employment and Labour Relation Act, Cap. 366*)

(b) Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 (*The Labour Institution Act,) cap 300* na

(c) Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 (*The Non-Citizens (Employment Regulation) Act, Cap. 436*)

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina la Muswada na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

**2.2 Sheria zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu unaofanya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Kazi. Kwa kiasi kikubwa Kamati imeridhishwa na maudhui ya Muswada huu kwakuwa yamezingatia maslahi mapana ya Wafanyakazi na Waajiri, aidha ni wito wa Kamati kwa Serikali kuendelea kufanya maboresho ya Sheria kwa mtazamo wa kuongeza tija na ukuaji wa sekta mbalimbali.

**2.2.1** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini**, **Sura ya 366 (*The Employment and Labour Relation Act, Cap. 366*)**. Sehemu hii inahusu Ibara ya 3 hadi 19 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni Matumizi ya misamiati mahususi katika tasnia ya kazi mathalani Sheria hii inapendekeza kufuta neno "**Sunday"** lililopo katika tafsiri ya neno "**basic wage"** na badala yake kuweka neno "**rest day"** ili kuanisha kuwa mshahara wa mwajiriwa hautahusisha

malipo ya nyongeza yatakayolipwa kwa kufanya kazi siku za mapumziko.

Aidha marekebisho haya yameongeza sharti kwenye Kifungu kinachohusu haki ya waajiriwa kuanzisha vyama vya wafanyakazi chenye lengo la kuongeza kigezo cha Mfanyakazi wa ngazi ya juu ya uongozi "***senior management employee***" kuwa itahusisha pia mfanyakazi mwenye mamlaka ya kuajiri, kusimamia nidhamu ya watumishi au kusitisha ajira ya mtumishi. Lengo la marekebisha haya ni kuongeza sifa za watumishi wa ngazi ya juu ya uongozi na hivyo kwa mujibu wa kifungu cha 9(2) (c) cha Sheria hawaruhusiwi kuingia kwenye chama cha wafanyakazi kinachowakilisha wafanyakazi wasio kwenye ngazi ya juu ya uongozi wa mwajiri.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine yaliyojitokeza katika mapendekezo ni masharti mapya yanayoanisha sifa za mkataba wa ajira ya muda maalumu (***fixed term contract***), moja ya sifa hizo ni mhitimu wa shahada ambaye ameajiriwa kwa lengo la kupata mafunzo au uzoefu wa kazi ili aweze kuajiriwa, endapo mafunzo hayo hayazidi miezi ishirini na nne na ameajiriwa na mwajiri ambaye shughuli zake zinategemea kupata Zabuni.

Aidha Mapendekezo mengine yanalenga kuweka masharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa wakati wa mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza au kutokea kwa hali ya dharura. Kifungu kinaeleza kwamba, kunapotokea mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza au uwezekano wa kutokea kwa mlipuko wa magonjwa hayo au kunapotokea hali nyingine ya dharura ambayo inauwezekano wa kuathiri usalama wa watumishi au kuathiri kazi au uzalishaji katika eneo la kazi, mwajiri na mwajiriwa watakubaliana kuhusu namna nzuri zaidi ya kukabiliana na hali hiyo. Makubaliano hayo yatapaswa kuzingatia maslahi ya pande zote.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo lingine jipya katika Muswada ni kuweka masharti kuhusu likizo ya uzazi kwa mtumishi aliyejifungua mtoto kabla ya wakati wake (Mtoto Njiti).

Kifungu kinaeleza kuwa, mtumishi atakayejifungua mtoto Njiti ana haki ya kupewa likizo ya malipo ya uzazi kutokea tarehe ya kujifungua hadi kufikia kukamilika kwa wiki thelathini na sita za ujauzito. Vilevile mtumishi huyo anahaki ya likizo ya uzazi ya kawaida inayotolewa katika kifungu kidogo cha (6) katika mzunguko wa likizo yake. Lengo la marekebisho ni kuweka mwongozo wa kisheria kuhusu haki za mtoto aliyezaliwa kabla ya muda wake na mama aliyejifungua mapema zaidi kwa ustawi wa mama husika na mtoto wake.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Marekebisho haya yanalenga kuweka masharti kuhusu likizo isiyokuwa na malipo. Kifungu kinaeleza kuwa, baada ya kupokea maombi ya kimaandishi na kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye kanuni, mwajiri anaweza kumpatia mtumishi likizo isiyokuwa na malipo kwa muda wa siku zisizozidi thelathini. Aidha, muda wa likizo isiyokuwa na malipo unaweza kuongezwa kwa kipindi kingine kwa makubaliano baina ya mwajiriwa na mwajiri. Lengo la marekebisho ni kuainisha aina za likizo na masharti yake na hivyo kuondoa migogoro baina ya mwajiri na mwajiriwa kuhusu likizo hizo.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ni kuhusu malipo ya fidia kwa mwajiriwa aliyesitishiwa ajira bila ya kuwepo kwa sababu zinazokubalika na bila kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa. Kifungu kinaeleza kwamba, endapo muamuzi au Mahakama ya kazi itaamua kuwa usitishaji wa ajira haukuwa wa haki kwa kutokuwa na sababu au kutokufuatwa kwa taratibu za kusitishwa kwa ajira, muamuzi au mahakama inaweza kumuamuru mwajiri kumlipa fidia ya ujira **usiozidi miezi kumi na mbili**. Vilevile, endapo usitishwaji wa ajira utatokana na sababu za kibaguzi au unyanyasaji, fidia isiyozidi miezi ishirini na nne.

**Mheshimiwa Spika,** sheria ilivyo sasa, endapo mwajiri atamuachisha kazi mwajiriwa wake bila ya kuwa na sababu za msingi na kutokufuata taratibu, atamlipa fidia ya ujira **usiopungua miezi kumi na mbili**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na maoni kuwa, marekebisho yanayokusudia kuweka ukomo wa kulipwa ujira usiozidi miezi kumi na mbili, yawekwe pale tu itakapothibitika kuwa mwajiri alikuwa na sababu za msingi za kusitisha ajira ya mwajiriwa, ila alikosea tu katika kufuata taratibu za kusitishwa kwa ajira. Ushauri huu ulitokana na uzoefu katika nchi nyingine ikiwemo Afrika ya Kusini pamoja na maamuzi mbalimbali ya Mahakama ya Tanzania ambayo yamekuwa na mtazamo kama wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kifungu kinachohusu adhabu kwa kusitisha ajira kwa sababu za ubaguzi na unyanyasaji, Kamati ilikuwa na maoni kuwa mapendekezo hayo yawekewe adhabu ya chini ya fidia isiyopungua miezi kumi na mbili na ya juu isiyozidi miezi ishirini na nne kwa lengo la kukidhi dhana iliyokusudiwa ya kuwekwa adhabu kubwa katika kosa hilo.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho mengine yanahusu kuweka masharti kwa mwajiri kutokuanzisha au kuendelea na shauri la kinidhamu dhidi ya mtumishi endapo suala hilo limepelekwa kwenye Tume au Mahakamani kwa ajili ya uamuzi. Lengo la marekebisho ni kuondoa mgongano katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu ili kuzingatia utawala wa kisheria, ambapo Mahakama ndio chombo chenye mamlaka dhidi ya mtu mwingine katika utoaji wa haki nchini kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300; (*The Labour Institutio Act, cap 300*).** Sehemu hii inahusu ibara ya 20 hadi 33 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Katika sheria hii yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kurekebishwa. Mambo hayo ni pamoja na kuweka sharti la kuwaondolea wasuluhishi mamlaka ya kuamua migogoro ya kikazi ambayo walishiriki katika hatua ya usuluhishi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano wa kimaslahi katika utatuzi wa migogoro ili kuendana na misingi ya utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ni kuweka masharti kuwa Sheria hii au Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini haitazuia mtu kuteuliwa kwa vyeo viwili kwa pamoja, kuwa Msuluhishi na kuwa Muamuzi. Lengo la marekebisho ni kuakisi marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 23, ambapo licha ya mtu kuteuliwa katika vyeo viwili, hatakuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri ambalo alikuwa msuluhishi.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho mengine yanaweka masharti kuwa fedha itakayolipwa kama faini kutokana na amri ya afisa kazi baada ya kufifilisha kosa, italipwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fedha hizo zinaweza zisilipwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali endapo Waziri mwenye dhamana ya fedha ataelekeza vinginevyo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea usimamizi wa utii wa sheria na kuongeza usimamizi wa fedha za umma.

Vilevile marekebisho mengine yanahusu kumuwezesha Jaji Mkuu, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya kazi, kutunga Kanuni zinazohusu taratibu zitazotumika Mahakama Kuu ya Kazi na kusimamia mienendo ya wawakilishi binafsi wanaowawakilisha wadaawa Mahakama Kuu ya kazi na Tume.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho mengine yanaweka masharti kwa mwajiriwa anayehusika na shauri lililopo kwenye Tume au Mahakama kuu ya kazi kuwa na uhuru wa kuchagua mwakilishi binafsi wa kumuwakilisha kwenye shauri hilo. Lengo ni kuendeleza misingi ya haki kwa kuwa na mwakilishi anayeaminika na mwajiriwa.

**2.2.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 (***The Non- Citizens (Employment Regulation Act. 436*)**.** Sehemu hii inahusu ibara ya 34 hadi 37 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii ni pamoja na kuweka masharti yanayomtaka mgeni aliyepewa kibali cha kufanya kazi daraja A, pale ambapo mgeni

huyo akihitaji kushirikiana na kampuni nyingine kwa kuwa mwanahisa atatakiwa kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna wa Kazi. Lengo la marekebisho ni kudhibiti matumizi mabaya ya vibali vya kufanya kazi nchini vinavyotolewa kwa wageni.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ni kuweka masharti kuwa kibali cha kufanya kazi kitakachotolewa kwa mkimbizi kitakuwa hai katika muda wote ambao mtu huyo ataendelea kuwa na hadhi ya ukimbizi kwa mujibu wa sheria husika. Lengo la marekebisho ni kuwatofautisha wakimbizi na wageni wengine wa kawaida nchini katika masharti ya vibali vya kazi.

Vilevile Marekebisho haya yanalenga kuweka masharti kuwa maombi ya kuhuisha kibali cha kazi yatawasilishwa kwa Kamishna wa Kazi angalau siku sitini kabla ya kuisha muda wake wa matumizi. Lengo la marekebisho ni kuongeza ufanisi katika kushughulikia maombi ya kuhuisha vibali vya kufanya kazi nchini.

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Aidha, baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kupendekeza kufanyike marekebisho ya msingi ili kuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1 *Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366 (The Employment and Labour Relation Act, Cap. 366).*

**Mheshimiwa Spika,** katika sheria hii Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

(a) Ibara ya 4 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 kinachohusu Tafsiri ya Maneno. Muswada unapendekeza kufanya tafsiri ya neno "***basic wage***" kwa kufuta neno "***Sunday***" na badala yake kuweka neno "***rest day***". Kamati ilijadili kwa kina suala hili pamoja na kupata maoni ya wadau waliofika mbele ya Kamati. Majadiliano ya

Kamati na Serikali yalifikia mwafaka kuwa licha ya kuongezwa kwa neno "***rest day***" kubakia kwenye mapendekezo ya marekebisho, vilevile neno "***Sunday***" libaki katika sheria. Kamati ilikuwa na maoni kuwa, kwa kawaida ni utamaduni wa Kitanzania kuwa siku ya Jumapili ni siku ya mapumziko ambapo jamii za Kitanzania hukutana kwa ajili ya masuala mbalimbali ya kijamii. Endapo litaondolewa, litakuwa na athari za kufuta utaratibu huo kwa kuwa mwajiri atakuwa na hiyari ya kumchagulia mwajiriwa siku ya kupumzika.

(b) Aidha ilikubalika kuwa neno "**rest day**" ambalo limependekezwa kuongezwa kwenye sheria, litafsiriwe ili kuepuka kila mwajiri kuwa na tafsiri yake na hivyo kupunguza migogoro kati ya mwajiri na mwajiriwa. Serikali imezingatia ushauri huo katika jedwali la marekebisho.

(c) Ibara ya 4 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 9(6)(b) kwa kuongeza tafsiri ya maneno "***Senior Management Employee***" kuwa litahusisha pia mwajiriwa mwenye mamlaka au anayeweza kuruhusiwa kuajiri, kusimamia nidhamu ya mwajiriwa au kusitisha ajira ya mwajiriwa. Kamati ilishauri kuwa neno "***discipline***" linaweza kuwa na utata kwa kuwa kwenye sekta binafsi watumishi ambao sio sehemu ya Menejimenti kama vile wasimamizi (*supervisors*) kwenye maeneo mbalimbali ya uzalishaji hususani viwandani wanayo mamlaka ya kusimamia nidhamu za waajiriwa walio chini yao ijapokuwa watumishi hao sio sehemu ya watumishi wa ngazi ya juu ya uongozi kwenye Kampuni.

Kwa msingi huo, Kamati ilishauri neno "**discipile**" lifutwe katika tafsri hiyo kwakuwa neno hilo linawagusa wafanyakazi wa kawaida. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kufanya marekebisho kwenye kifungu husika kama ilivyoshauriwa.

(d) Ibara ya 6 inafanya marekebisho katika Kifungu cha 14(1) cha Sheria kinachoainisha sifa za Mkataba wa ajira ya muda Maalumu. Kamati ilishauri kuwa Kifungu cha 14(1)(b)(ii) kimetumia neno "*employed*", na kuwa na maoni kuwa

kutumika kwa neno hilo kunaweza, bila kukusudia, kuwatatiza waajiri kuendesha programu za mafunzo au kutoa nafasi za mafunzo kwa wahitimu, kwani kinaweka mahitaji ya ziada ya kufuata sheria nyingine kama vile sheria za kodi na kanuni za hifadhi ya jamii. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kufuta kifungu 14(1)1(b)(ii) katika Jedwali la Marekebisho.

(e) Ibara ya 7 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 16 cha sheria ili kuweka sharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa wakati wa mlipuko wa magonjwa au kutokea kwa hali ya dharura. Kamati ilikuwa na maoni kuwa kiongezwe kifungu kidogo ambacho kitashughulika na kutoa mwafaka pale ambapo pande zote mbili zitashindwa kukubaliana. Msingi wa hoja ya Kamati ni kuwa suala la kukubaliana linauwezekano mkubwa wa kugusa maslahi ya mwajiriwa, hivyo kuweka uwezekano wa kutokuafikiana. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kuweka sharti kuwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ndio chombo kitakachofanya uamuzi endapo mwajiri na mwajiriwa watashindwa kukubaliana kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

(f) Ibara ya 8 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 33 cha Sheria kinachohusu likizo ya uzazi (*Matenity Leave*) ili kuweka masharti kuhusu likizo ya uzazi kwa mtumishi anayejifungua mtoto Njiti. Kamati ilipendekeza kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa Mama aliyejifungua watoto njiti kutoka wiki 36 hadi 40. Kamati ilipata maoni toka kwa Wataalamu wa Afya na inaamini kuwa kiafya mtoto anakuwa yupo vizuri zaidi akifikia wiki 40, hivyo ikiwa mtoto atazaliwa Njiti, mama mzazi atapaswa kupewa likizo ya utangulizi hadi pale atakapofikisha wiki 40. Hali hii itamsaidia kuweza kumhudumia vizuri mtoto njiti. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kuwa kufuta namba 36 na badala yake kuweka namba 40 katika jedwali la marekebisho.

(g) Aidha, katika Ibara hiyo, vilevile Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kitakachoweka masharti ya kutoa likizo ya siku saba (7) kwa Baba aliyepata mtoto njiti (*paternity leave*

*during premature birth of child*). Msingi wa hoja hii ni kutokana na ukweli kuwa kumekuwepo na matukio katika hospitali zetu ambapo baba mzazi hufanya jukumu la kuwapa joto watoto njiti (Kangaro Method) ambao bado wapo katika uangalizi hospitalini. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kufanya maboresho katika Kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(h) Katika Ibara ya 11 inayorekebisha Kifungu cha 40 cha Sheria ili kumuwezesha muamuzi au Mahakama kumuamuru mwajiri kumlipa fidia ya ujira **usiozidi miezi kumi na mbili** mwajiriwa kama adhabu ya kusitishwa kwa ajira bila ya kuwepo kwa sababu zinazokubalika na bila kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa. Kamati ilijadili kwa kina kuhusu mapendekezo haya ambayo pia yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na wadau waliofika mbele ya Kamati. Kamati iliona kuwa, sheria ilivyo sasa inajitosheleza kwa kuwa inaweka malipo ya fidia ya ujira **usiopungua miezi kumi na mbili** kwa mwajiri kutenda kosa la aina hiyo. Hata hivyo, Serikali ilieleza kuwa ilikusudia kuweka ukomo wa miezi ya fidia ili kuzuia matumizi mabaya ya madaraka kwa baadhi ya waamuzi kwa kutoa fidia ya miezi mingi bila ya kuwa na sababu za msingi. Katika majadiliano na Serikali, ilikubalika kuwa kifungu hicho kirekebishwe kwa kuweka kiwango cha chini na kiwango cha juu cha fidia ili kuondoa dosari ambazo Serikali ilizieleza.

Vilevile Kamati ilikuwa na maoni kuwa, adhabu za kumuachisha mtu kazi inaweza kuwekewa ukomo usiozidi miezi kumi na mbili endapo mwajiri alikuwa na sababu za kumuachisha mwajiriwa kazi lakini hakufuata taratibu kwa makosa yanayomtaka kufuata taratibu jambo ambalo tayari Mahakama ya Tanzania imeshatoa maamuzi ya aina hii. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kufanya marekebisho katika mapendekezo husika.

(i) Aidha, katika Ibara ya 11, Kamati ilikuwa na maoni kwenye kifungu kinachohusu adhabu kwa kusitisha ajira kwa sababu za ubaguzi na unyanyasaji, Kamati ilikuwa na maoni kuwa mapendekezo hayo yawekewe adhabu ya chini ya fidia

isiyopungua miezi kumi na mbili na ya juu isiyozidi miezi ishirini na nne. Lengo la Kamati lilikuwa ni kukidhi dhana iliyokusudiwa na kuondoa mazingira yanayompatia muamuzi au Mahakama kuweza kutoa fidia ya miezi atakayoona inafaa ilimradi haizidi miezi ishirini na nne. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kufanya marekebisho katika Jedwali lililowasilishwa.

(j) Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 86(6) cha Sheria ambacho kinaweka masharti ya ulazima wa mlalamikaji kuwepo wakati wa usuluhishi wa shauri alilolifungua Tume hata kama ana mwakilishi wake au wakili wake. Kamati ilishauri kuwa kiwekwe kifungu kitakachowezesha walalamikaji wenye sababu maalum za kutokuwepo wakati wa usuluhishi waruhusiwe kuwakilishwa na wawakilishi wao au mawakili wao kufanya usuluhishi kwa niaba yao. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya maboresho katika Kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(k) Ibara ya 17 inarekebisha Kifungu cha 88 cha Sheria ili kuwezesha muamuzi kuwataarifu wadaawa kuhusu kushindwa kutoa uamuzi wake katika siku thelathini, na kwamba ataeleza sababu pamoja na kutaja tarehe nyingine ya uamuzi. Katika majadiliano na Serikali, ilikubalika kuwa Kifungu hiki kiboreshwe kwa sharti la kuwataarifu wadawa kufanyike kwa njia ya maandishi *(shall notify parties in writing)*. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya maboresho yaliyopendekezwa.

(l) Ibara ya 19 inarekebisha Kifungu cha 97 cha Sheria kinachoweka sharti linalompatia mpelekaji wa nyaraka za mahakama mamlaka ya kuwasilisha nyaraka chini ya sheria hii. Kamati ilipendekeza Kifungu hiki kirekebishwe kwa kuongeza utaratibu wa kusambaza nyaraka za Mahakama za Kazi kwa njia ya barua pepe *(email)*, ikizingatiwa kuwa Mahakama imeanza kutumia mifumo ya kidigitali katika kazi zake. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kuweka mapendekezo hayo katika Jedwali la Marekebisho.

**3.2 Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 (Labour Instituion Act, Cap. 300)**

**Mheshimiwa Spika,** katika marekebisho ya Sheria hii, Kamati ilikuwa na oni moja tu kama ifuatavyo: -

(a) Ibara ya 35 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 cha Sheria kinachoweka masharti yanayomtaka mgeni aliyepewa kibali cha kufanya kazi daraja A, pale ambapo mgeni huyo akihitaji kushirikiana na kampuni nyingine kwa kuwa mwanahisa atatakiwa kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna wa kazi.

Kamati inapendekeza kifungu kiboreshwe kwa kuwa mabadiliko yanayopendekezwa yanaweza kuwa na athari hasi kwa sekta ya usimamizi wa kodi, kwani yanaweza kurahisisha mikakati ya kukwepa kodi, kama vile uundaji wa Makampuni yenye lengo la kukwepa kodi. Kamati ilishauri maboresho kama ifuatavyo- *by adding the following words "after presenting tax clearance certificate from the relevant authority regarding tax administration" after the word commissioner appearing in proposed sub section (3)*. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama iliyopendekezwa.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na masuala ya kazi.

(a) Serikali iboreshe kifungu cha 27 cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ambacho kitazuia mazingira ya mwajiri kulipwa waajiriwa mshahara bila kupitia benki zilizosajiliwa nchini. Changamoto iliyopo ni wajiriwa wengi wa Sekta Binafsi wamekuwa wanalipwa mishahara bila kutumia mifumo ya Kibenki na kupelekea Serikali kukosa takwimu sahihi za

waajiriwa wanaolipwa viwango stahiki katika mifumo rasmi. Aidha, utaratibu huu umekuwa ukitumika kuwakandamiza waajiriwa wakati wa malipo ya mishahara yao;

(b) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta maboresho yanayotoa likizo ya uzazi kwa mama anayejifungua mtoto njiti. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuona namna ya kufanya maboresho katika Sheria ili kuruhusu pia akina mama wanaojifungua watoto mwenye mahitaji maalum kama vile usonji, vichwa vikubwa, mgogo Wazi, mdomo sungura, matundu kwenye moyo, seli mundu n.k waweze kupewa likizo maalum ya uzazi pindi wanapojifungua.

(c) Kamati inaishauri Serikali kufanya maborekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 ili kuweka sharti la kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Kurithisha Ujuzi.

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohammed Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.

12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
13. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
16. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
18. Mhe. Neema Kachiki Lugangira, Mb.
19. Mhe. Khamis Yussuf Mussa, Mb
20. Mhe. January Yussuf Makamba, Mb
21. Mhe. Khadija Shaban Taya, Mb

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Paschal Patrobass Katambi (Mb) Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Leornad na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
31 Januari, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa wasilisho hilo kwa niaba ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshasikia pande zote mbili kwa maana ya upande wa mtoa hoja Serikali, lakini pia maoni ya Kamati kwenye Hoja hii ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali zinazohusu kazi.

Sasa kama ilivyo ada, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja, lakini kuna jambo moja limesemwa kwenye taarifa hii ya Kamati, ni jambo la Kiswahili kwa maana ya Kiswahili Sanifu. Neno "maoni", nadhani huwa halina umoja. Ni neno "mapendekezo", ndilo lina umoja wa "pendekezo." Kwa hiyo, hamna "oni", huwa ni "maoni", ama ukitaka, unatumia neno lingine, hakuna "oni" moja, sawa.

Sasa hapa ninayo majina. Tutaanza na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi nami siku ya leo niweze kuchangia katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Kazi wa mwaka 2024. Kwanza, kabisa nami naungana na wenzangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea pekee wa Urais mwaka 2025. Pia, kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi naye pia nampongeza sana kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba hawa ndio Marais wetu wa 2025. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Kazi, Ajira na pamoja na Makatibu Wakuu, Naibu Waziri na Watendaji wao wote. Kwa kweli tumepata ushirikiano mkubwa katika majadiliano juu ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kukupongeza wewe kwa jinsi unavyotuelekeza na unavyotufundisha. Kwa kweli unapokaa hapo kwenye Kiti, wewe ni Mwalimu. Tunajifunza mengi sana kutoka kwako hata sisi wengine ambao ni Walimu wa Shule ya Msingi, sasa tunakuwa wanasheria. Unafanya kazi kubwa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, mchango wangu utajikita katika Ibara ya Tano, Sita, Saba, Nane na ya 31 na iwapo muda utaniruhusu nitachangia Ibara ya 35. Nikianza na Ibara ya Tano Kifungu cha Tisa, pale kuna neno la "*Senior Management*". Kwa mujibu wa sheria, umeongezwa Kifungu cha 9(2) hawa ma-*senior* kuingia kwenye vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, hili suala tulijadiliana katika Kamati, lakini tunaipongeza Serikali ililichukua ombi hili. Tunajua katika utendaji wa kazi, sheria hizi zinahusu sana kwenye sekta binafsi, sekta binafsi Vyama vya Wafanyakazi ndiyo mtetezi wao. Sasa tunapomchukua kiongozi ambaye ni *senior* kuingia tena kwenye vyama hivi, yeye huyo anaingia kwenye kikao cha menejimenti, huyo huyo anapanga mambo, yeye tena aje kwa wafanyakazi, ila watakuja kuchanganya wafanyakazi wetu. Hilo tuliligomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunaishukuru sana Serikali ililipokea suala hilo, tunajua umuhimu wao, wao wanaingia kwenye menejimenti, lakini pia wawaache wafanyakazi wa-*play part* na vyama vyao na wenzao kama wafanyakazi, siyo tena kuja kuwachanganya na uongozi na wafanyakazi, siyo jambo sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya Sita, Kifungu cha 14 kifungu hiki kimeboresha kuwasaidia wanaohitimu waweze kupata ajira za muda. Kwa kweli tunatambua nchi yetu tumekuwa na wahitimu wengi sana wa vyuo vikuu, lakini wahitimu hawa wengi wapo mitaani. Kwa marekebisho haya, sheria hii inakwenda kuwapa nguvu sasa wale wahitimu wakipata ajira za muda kwenye mashirika au makampuni haya binafsi waweze

kuchukuliwa kama ni watumishi au ni kama ambao wanaendeleza programu ya kukuza ujuzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunatambua wanakuja waajiri wengi na wengine makampuni mengine yanaendeshwa na waajiri wa kigeni, lakini pale wanapotoka hatuna wengine ambao walikwenda kujifunza na wao kuchukua ujuzi ule. Sasa kwenye kifungu hiki kitawaruhusu wale wahitimu wetu waende kama *field* kule kwa kipindi kisichozidi miaka miwili si jambo dogo. Tunaishukuru sana Serikali na tunaipongeza sana kwa kutambua haja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua yapo maeneo kama *TaESA* yanaendelea kutafuta, kuwachukua, kuwafanyia wanafunzi kuwaanda kwenda kwenye ajira za kujifunza, lakini sasa kipengele hiki cha sheria kitampa nguvu hata *TaESA* naye ili ile programu yao ya kuwatafutia vijana ajira iende sambamba na kwenye haya makampuni. Ni suala kubwa tunaipongeza sana Serikali kwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye Ibara ya Saba, ibara hii inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 16(a) kuweka makubaliano kati ya mwajiri wakati wa hali ya dharura inapotokea. Hawa wafanyakazi katika maeneo hasa kwenye haya makampuni au kwenye viwanda, kunaweza kukatokea magonjwa ya dharura. Tumeona hapa *Corona*, jambo ambalo likasababisha mtambo au kiwanda kile kufungwa, lakini watumishi wale kukaa kiholela bila kujielewaelewa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sheria hii ambayo imeongeza kifungu kidogo cha Tatu itakuwa na uwezo wa mwajiriwa na mwajiri wake kukaa kujadiliana, lakini pia kujua kwa jinsi gani utendaji wao utakwenda katika kipindi hicho cha mpito. Vinginevyo, mwajiri pasipo sheria hii kumlinda mfanyakazi angeweza kufunga na akasema mimi basi naondoka na wale wasijue kesho yao. Hivyo basi, sheria hii imekwenda kutibu matatizo ya wafanyakazi pale itakapotokea matukio yote ya kidharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Ibara ya 31, ibara hii imeongeza Kifungu cha 45A kuweka fedha zinazotakiwa na ufifilishaji wa makosa zinaweza zisilipwe kwenye mfuko mkuu endapo Waziri wa Fedha ataekeleza hivyo. Tunajua umuhimu wa ufifilishaji wa makosa hawa sekta binafsi, lakini pia hata wafanyakazi na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, unakuta mtu ana kosa la kulipa shilingi 200,000 inamfanya ashindwe kufanya kazi au afunge kiwanda au afunge mtambo. Kwa hiyo, sheria hii ya ufifilishaji wa makosa itamsaidia yule ambaye amekosea kufanya kitu chochote, atalipa faini na ataendelea na kufanya majukumu yake ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa basi kwa kifungu hiki kitawasaidia, pia hizi za ufifilishaji wa makosa zitakwenda, iwapo Waziri wa Fedha ataelekeza, zinaweza zikaenda kwenye Wizara husika au sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kwamba, fedha hizi inategemea ni fedha za kiasi gani? Napenda Waziri mhusika huyo anayeambiwa atoe kibali, aangalie na wingi wa hiyo fedha. Vinginevyo isiwe kwamba mlango sasa wa kufungulia fedha ya Serikali ikaanza kutumika bila utaratibu mzuri. Jambo ni jema na nia ya Serikali ni njema ila tuwe waangalifu katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia tena Ibara ya Nane, kuongeza muda wa likizo kwa mama aliyejifungua mtoto njiti, haya yalikuwa ni kilio cha Wabunge wengi akina mama na akina baba, lakini leo kimepatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru na kuipongeza Serikali yetu, kwa kuwa wale watumishi wa Serikali na mashirika ya umma angalau wao walikuwa na nafasi ya kusikilizwa, lakini wale wanaofanya katika sekta binafsi hizi, utakuta mama analia na kichanga chake, amepewa likizo yake ya *maternity* hiyo hiyo likizo akae nayo, hiyo hiyo ndiyo alee njiti, hiyo hiyo anajikuta amemaliza likizo na mtoto ana mwezi mmoja au ana siku 10 jambo ambalo lilikuwa linatesa sana akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa hii sheria iliyoletwa inakwenda kumsaidia mama, lakini kama haitoshi wameweka siku saba za baba. Tunajua mama anapoingia kwenye matatizo hata baba naye anaingia kwenye matatizo, hawezi akapewa siku zote naye baba kama za mama, lakini angalau kwa zile siku saba za mwanzo, basi naye awe sehemu ya kumsaidia mama huyu hata kumpelekea uji hospitalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza sana Serikali yetu kwa jambo hili. Jambo hili ni muhimu kwa maisha ya akina mama, lakini muhimu katika kuokoa maisha ya vichanga wetu. Tunajua vichanga vinakaa hospitali kwenye kangaroo kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wakati mama yupo pale analea kichanga, ni kwamba yeye yupo hospitalini, lakini atakapotoka pale ndipo likizo yake ianze kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naipongeza tena Serikali yetu. Kwa kweli naipongeza Wizara hii, imekuwa Sikivu, tumeenda vizuri katika kujadili Muswada huu, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima na afya njema. Nami nampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa mgombea pekee wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza, na pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kuwa mgombea wa Urais kule Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza na wewe kwa kazi kubwa unayoifanya, hata hivyo nakupongeza kwa juhudi uliyoifanya kuiunda Kamati hii ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Ni Kamati muhimu sana, kwa sababu ni Kamati mtambuka. Jambo lolote kwenye jamii inagusa kwenye Kamati hii. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati, kwani tulivyopitia Miswada hii na sisi tumekuwa ni *learned sisters and brothers,* tumejifunza. Mpaka kumaliza Bunge hili tumekuwa na sisi Wanasheria. Kwa kweli tunashukuru sana kwa juhudi zako kwa Kamati hii ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza kwenye Ibara ya Nane ya Muswada inayopendekeza marekebisho katika likizo ya uzazi *(maternity leave)* kwa mama anayejifungua mtoto njiti *(pre-mature baby)*. Kwenye Kamati tumependekeza likizo hiyo ianze pale mtoto atakapotimiza zile wiki 40 ambazo angepaswa kuzaliwa nazo akiwa *full term*.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali, wamekuwa wasikivu, Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Patrobass Katambi, timu yao yote, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia Kazi, Ajira na Watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia pia maoni ya wadau mbalimbali kama ilivyoelezwa kwenye taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Toufiq. Pia, mimi mwenyewe ni mtaaluma, ni Muuguzi, mkunga lakini pia ni Mwalimu Muuguzi. Kwa hiyo, eneo hili ninalifahamu na ni eneo langu la kazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukafahamu mtoto njiti ni nani? Mtoto njiti *(pre-mature baby)* kutokana na tafsiri ya Shirika la Afya Duniani ni mtoto aliyezaliwa akiwa hai kabla ya wiki 37 za ujauzito. Tatizo la watoto njiti nchini Tanzania ni kubwa. Tunaona tafiti zilizofanyika na Shirika la Afya Duniani, kati ya kila watoto milioni

mbili na zaidi wanaozaliwa katika nchi yetu ya Tanzania,16.6% ni watoto njiti. Hivyo, tatizo nchini Tanzania ni kubwa na ndiyo maana Kamati pamoja na wadau mbalimbali tulikuja na ombi la kufanya marekebisho kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hawa watoto njiti wana changamoto kubwa. Kwa kuwa hata mtoto akiwa amezaliwa kwenye wiki ya 39 au 40 tunasema mtoto aliyekomaa anakuwa na tatizo, lakini kwa mtoto njiti tatizo linakuwa mara mbili au mara tatu zaidi. Kwa nini ninasema hivyo? Watoto hawa pamoja na mambo mengine yote, lakini unakuta ubongo wao haujakomaa, mapafu bado hayajakomaa *(immature lungs)* na vile vile ini linakuwa halijakomaa. Kunakuwa na changamoto pamoja na sehemu nyingine zote za mwili wa mtoto huyu kwa sababu anakuwa bado haijakomaa, lakini maeneo hayo matatu ni nyeti zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na changamoto hizo, watoto hawa hawana uwezo wa kutunza joto mwilini. Kila wakati hali yao ya joto inakuwa chini ya *centigrade degree 35*. Kwa hiyo, ni rahisi sana watoto hawa kuhangaika na hata wanaweza wakapoteza maisha. Vilevile, kwa sababu ubongo unakuwa bado haujakomaa, uwezo wa kunyonya na hata kumeza yale maziwa inakuwa bado ni changamoto, kwa sababu *sucking* na *swallowing reflex* zinakuwa bado hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, natumia Kiingereza kwa sababu nashidwa kuleta kwenye Kiswahili chake sasa. Kwa lugha ya kawaida tu kwamba bado hata uwezo tu wa kupambana na magonjwa unakuwa haupo, kila wakati wanapata maambukizi. Pia, kwa watoto hawa kwa kuwa ini linakuwa bado halijakuwa linafanya kazi vizuri, kila wakati wanakuwa na upungufu wa damu, na mwili wao unabadilika, unakuwa njano kwa sababu ya changamoto ya uyeyushaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali yote hii, tumeona, kwa hiyo, sisi kama Kamati tumekaa pamoja tukasema ni vizuri huyu mama anayejifungua mtoto njiti na kwa sababu tayari tatizo limeshaonekana ni kubwa nchini Tanzania, basi pale

anapojifungua, yule mama aendelee kupewa mapumziko kwanza mpaka pale mtoto huyu atakapofikisha wiki 40 ndipo hapo likizo ya uzazi *(maternity leave)* ianze, tukitegemea kwamba mama ameshampa maangalizi mazuri huyu mtoto na ameshakuwa na uwezo hata wa kuongeza uzito na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndipo hapo tulipofikia kwamba, hata akina baba wapate likizo ya uzazi angalau zile siku saba. Kweli Serikali ikawa Sikivu, imekubali ili wasaidiane na mama kumtunza huyu mtoto kwa kupeana zamu. Imeonekana mara nyingi tu, kuna hospitali kadhaa huko Dar es Salaam na kwingineko, wababa nao wanapata zamu ya kumtunza yule mtoto kwa ile njia inayoitwa *kangaroo method* ya kumshika mtoto na kumfunga ili apate joto la mzazi ili kumtunza apate kuwa na joto ili aweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tuliona kwamba kwa kuwa changamoto hii nayo ni kubwa na tunaona Serikali imekuwa sikivu ikakubali, tukasema hivi, ni vyema sasa tunavyoleta humu ndani hili jambo na Waheshimiwa Wabunge wote mnalijua, kwamba ni kilio cha familia, na cha jamii nzima tunaona ni tatizo kubwa. Tunaomba tuungane wote tuunge mkono hoja hii ipite katika Bunge hili ili kusaidia jamii yetu inayohangaika na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonesha kwamba watoto hawa njiti wakiangaliwa vizuri, wanakuja kuwa watoto wazuri, wanakuja kuwa na afya njema, na wanakuja kumudu hata maisha yao wenyewe na kuchangia kwenye jamii na hata nchini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuna tafiti mbalimbali na hata historia inaonesha *Sir* Isaack Newton naye alizaliwa akiwa njiti, lakini unaona ameendelea kuwa mwanasayansi mzuri, mwanamahesabu mzuri na kila kitu mpaka sasa katika historia na katika sayansi yetu tunaendelea kumtumia kwa *reference* zake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba katika hili tushirikiane wote katika kupitisha huu Muswada na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nawaza hapa, je, huyu baba akipewa hii likizo halafu asiende kufanya hii kazi, kuna mahali pa kumshataki?

Mheshimiwa Athuman Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya Sheria za Kazi ya mwaka 2024. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu kuwa mgombea pekee wa Uraisi kwa mwaka 2025, na pia Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza, na pia kule Zanzibar nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussen Mwinyi kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu nami kuniruhusu kusimama leo hapa nikiwa na afya nzuri, niweze kuchangia Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo ambayo nafikiri ni muhimu katika Muswada huu unaopendekeza marekebisho ya Sheria ya Kazi *Cap. 366 (The Employment and Labor Relation Act Cap. 366)*

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha Tatu, marekebisho yanaletwa ili kutofautisha makosa mawili ya mwajiri aliyemwachisha mfanyakazi aliyefanya makosa, lakini hakufuata kanuni na kosa la pili mwajiri aliyemfukuza kazi mwajiriwa ana makosa, lakini hakufuata kanuni.

Mheshimiwa Spika, sheria inarekebisha kuweka makosa mawili tofauti na kuweka adhabu tofauti kwa mwajiri kutoa fidia ya ujira tofauti kwa makosa yote mawili. Hili limekuwa jambo

muhimu sana na sheria imerekebisha na kuweka kiwango cha chini cha adhabu chini ya miezi 12 na isizidi miezi 24.

Mheshimiwa Spika, lipo suala lingine katika Ibara ya Saba, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 16 kwa lengo la kuweka sharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa katika hali ambayo ni ya dharura. Tulipata tatizo la *Corona* hapa na ofisi zikafungwa na wafanyakazi wakaenda majumbani. Mwajiri aliendelea kuwalipa mishahara wafanyakazi kwa sababu hapakuwa na makubaliano tufanye nini katika hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, sheria hii inatoa unafuu sasa kwa mwajiri kukaa na mwajiriwa ili kujadiliana wafanye nini? Kazi zimesimama, mwajiri alipe au asilipe au alipe kiasi gani na kama watashindwana imewekwa nafasi ya *CMA* awe msuluhishi aingilie kati kuwapatanisha ili kufikia mwafaka nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 86(6) cha Sheria ambacho kinaweka ulazima wa mlalamikaji kuwepo kwenye Tume ya Usuluhishi wakati wote suala linapojadiliwa na kama asipokuwepo basi suala lisijadiliwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati imependekeza na Sheria hii inarekebisha sasa uwakilishi wa mtu anayelalamika ili kesi ziendelee badala ya kusimama kama ilivyokuwa huko nyuma kwamba waliolalamika lazima wawepo Mahakamani hata kama wana Mawakili, lakini nao wapo; lakini kama hawapo kwa sababu yoyote kama vile kuumwa au wana sababu yoyote, kesi inasimama. Sasa kesi zitaenda, masuala yatajadiliwa kwa sababu sheria inaruhusu uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 97 cha Sheria kinaweka sharti la kupeleka nyaraka za Mahakama kwa mkono. Katika hali ya sasa ya dunia ya *digital* na Mahakama yenyewe imekwenda *digital.* Tumependekeza na sheria imependekeza sasa kutumia hata *email* au aina yoyote ya kidijiti kuwakilisha nyaraka zozote za

Mahakama kwa anayehusika. Hali ile ya kutumia barua kwa mkono tumeiacha na tumependekeza sasa ipelekwe barua ile kwa *email* au kwa njia yoyote ya kidijiti.

Mheshimiwa Spika, mimi niliona maeneo haya muhimu ndiyo niyajadili na ninakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, atafuatiwa na Mtoa hoja.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya kuhusu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi za Mwaka 2024 *(The Labor Laws Amendment Acts, 2024)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fursa kubwa ambayo ameipata katika ule Mkutano wetu Mkuu Maalum ya kuwa mpeperusha bendera ambaye ataipeperusha bendera yetu katika kukitetea Chama cha Mapinduzi. Sambamba na hilo nampongeza pia mgombea mwenza, Dkt. Nchimbi; halikadhalika, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi ambaye pia atakuwa mpeperushaji bendera Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Rais na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, bila kukusahau wewe jinsi unavyoliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naona wenzangu wamezungumza sana, lakini nami pia kwa msisitizo naomba nizungumzie kuhusu Ibara ya Saba ya Muswada ambayo inaweka sharti kuhusu makubaliano ya mwajiri na mwajiriwa wakati wa hali ya dharura. Hili kweli lilibainika pale lilipotokea kuanzia mwaka 2019 ambapo ulitokea ule ugonjwa wa *Covid*, pale ulitokea mtihani mkubwa sana kwa sababu baadhi ya viwanda na baadhi ya ofisi zilifungwa, na ikatokea kuna baadhi ya wafanyakazi walikuwa hawalipwi na

wengine wakawa wanalipwa, kwa hiyo, ikawa kuna tafrani kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imeonyesha kabisa kwamba katika hali ya udharura, basi itabidi mwajiri na mwajiriwa waweze kukaa pamoja waone namna bora ya kuleta ustawi kwa ajili ya watu wote. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Sheria hii ili kusudi itakapotokea changamoto yoyote, mwajiri na mwajiriwa waweze kukaa pamoja. Hii itasaidia katika ufanisi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo napenda nizungumzie pia ile Ibara ya Nane ambayo wenzangu wote wamezungumzia kuhusiana na wale akina mama waliozaa watoto njiti waweze kukaa wiki zile 40 halafu baadaye ndiyo waweze kupata likizo ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema sana, lakini pia miongoni mwa wadau ambao ni Chama cha Madaktari na Wafamasia, wao walienda mbali zaidi, wakasema kwamba, kitabibu hata mama ambaye amejifungua mtoto njiti naye pia ana tatizo la kiafya au ana changamoto ya kiafya. Kwa hiyo, ina maana kwamba watu wote hawa wanahitaji wapate muda wa kupumzika ili mwisho wa siku sasa, baada ya zile siku 40 mama huyu aweze kupata ile likizo yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na Wajumbe wenzangu na kuipongeza Serikali kwa kukubali kwamba zile siku saba za *paternity leave* kwa ajili ya akina baba ambao wake zao au wenza wao wamejifungua njiti. Mimi ninaamini…

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Nani amesimama kwa Taarifa? Anha, Mheshimiwa Fatma Toufiq kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mama yangu kwamba wanapokuwa wanawaombea siku saba hao wanaume wenye watoto njiti, nilitamani waifanye iwe kwa wanaume wote wanaopata watoto wadogo. Kwa sababu gani? Siku tatu zimekuwa ni changamoto kwa wazazi ambao wamepata watoto ambao wake zao wanakuwa hospitali, halafu wao wanatakiwa wa-*attend* kazini. Kwa hiyo, isiwe tu kwa watoto njiti, ionekane kwamba ni kwa wafanyakazi wote wanaume ambao wamepata watoto wadogo, ndani ya hizo siku saba, wapewe angalau likizo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nimeipokea hiyo Taarifa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naendelea kusema kwamba tunaishukuru sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza hizi siku saba. Tunaamini kwamba akina mama wengi wakijifungua, wanahitaji sana wenza wao na hicho ndicho kipindi muhimu sana cha kumhitaji mwenza ili kusudi aweze kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa kukubaliana na maoni ya Kamati. Naamini kwamba wanaume wote wema; ninarudia tena, wanaume wale wote wema, watakaa na wake zao katika hizi siku saba na ikiwezekana katika siku za *weekends* ili kusudi waweze kuwasaidia wake zao pale watakapokuwa wamejifungua watoto njiti.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni katika sheria ya usimamizi wa ajira kwa wageni Ibara ya 35 ya Muswada ambayo inamtaka mgeni aliyepewa kibali Daraja A ambaye anahitaji kushirikiana na kampuni nyingine kuwa mwanahisa katika kampuni kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna wa Kazi, lakini Kamati imeshauri kwamba, mgeni huyu ambaye amepata Kibali A, ni budi sasa kama

atataka kuingia ubia katika kampuni nyingine ni budi apeleke *tax clearance certificate* kabla ya idhini ya Kamishna ili kuepuka suala zima la ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nilipenda pia nichangie kuhusu wale wanawake ambao wanazaa watoto wenye changamoto mbalimbali, changamoto za ulemavu, pengine wale watoto wana midomo wazi na pia sheria ingewaona kwamba na hawa nao wanahitaji kupata *special treatment* ili kusudi waweze kuwahudumia watoto wao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni ni budi basi, kuna lile suala la urithishwaji wa ujuzi, sasa huu urithishwaji wa ujuzi umekuwa ukitathminiwa vipi? Kwa hiyo, tunatamani kwamba uwekwe mfumo maalumu ikiwezekana kisheria ili kusudi sasa ule utaratibu au mfumo wa urithishwaji wa ujuzi kwa Watanzania uweze kufanyika kwa utaratibu na ikiwezekana tathmini ifanyike ili mwisho wa siku sasa, wale wageni au wawekezaji wanapoondoka tujue idadi ya Watanzania ni wangapi ambao wamerithishwa ujuzi huo?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niendelee kuipongeza sana Serikali, na kuunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa fursa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuzungumza machache kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Mtoto Njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naanza tu kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya ndani ya Bunge letu Tukufu na kama Rais wa Mabunge ya Dunia huko duniani, unafanya kazi nzuri sana. Tuna matumaini makubwa sana nawe, na hii hata wale unaowaongoza kule jimboni wanasema hawana mwingine zaidi ya Mheshimiwa Tulia

Akson. Hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri unazozifanya kila kona na hakuna atakayeweza kuvaa viatu vyako. Hili tunajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa au kuchaguliwa na Mkutano wetu Mkuu kuwa mgombea pekee wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2025, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na yeye kuwa mgombea pekee.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa upande wa Bara, nampongeza Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunasema, tunawatakia kila la heri na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye suala zima la Muswada kuhusu mtoto njiti. Watoto hawa ni watoto wa aina yake; ni watoto ambao wanazaliwa kabla ya muda wao. Pia, ni watoto ambao wanapozaliwa wanakuwa na changamoto nyingi sana. Kwa muktadha huo, Muswada huu utamsaidia sana mama ambaye anazaa mtoto huyu au mama ambaye anazaa watoto hawa, kwa sababu anaweza akazaliwa mtoto mmoja au wakazaliwa wawili au zaidi ya wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi mara mtoto huyu anapozaliwa, kwa kuwa, siku zake zinakuwa hazijatimia, mtoto huyu uangalizi wake ni tofauti na mtoto yule ambaye amezaliwa katika wakati wa kawaida. Jambo la kwanza, kwa sababu, sasa hivi dunia imepiga hatua kubwa za maendeleo, mtoto huyu anakaa kwenye kile kitotozi *(incubator)*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini anakaa pale? Ni kwa sababu ya kumtengenezea mazingira kana kwamba yuko ndani ya tumbo la mama yake, kumwongezea kiasi cha joto. Isipofanyika hivyo, mtoto huyu baada ya muda mfupi mazingira yake yanabadilika. Inapojitokeza hivyo, hata kunyonya anakuwa hawezi. Ndiyo inabidi wakamue maziwa ya mama, wampe mtoto anyonye au

watengeneze maziwa mengine ili wampe mtoto anyonye na hizo zote ni changamoto tofauti na mtoto wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoto wa kawaida anapozaliwa, kitu cha kwanza ni kulia. Akishalia, anaanza kutafuta nyonyo ya mama yake. Hakuna mtu anayemfundisha kutafuta nyonyo isipokuwa ukishamweka hapa tu, basi mtoto anaanza kuhangaika kutafuta nyonyo na ananyonya, anaendelea na maisha. Kwa hiyo, ni tofauti na mtoto njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine huyu mtoto njiti kama hakuna hizo *incubator* maana yake ndiyo amezaliwa, na zamani ndiyo walikuwa wanazaliwa tu huko majumbani, mpaka wamkimbize hospitali ni kazi. Ndiyo maana yule mtoto anatakiwa akumbatiwe. Anachukuliwa, anakumbatiwa hapa, mtoto anakaa hapa kifuani, ndiyo ile kangaroo. Lengo la kumkumbatia hapa ni kumpatia joto la mama yake. Sasa baada ya hapo, kama ndiyo kwa mazingira ya sasa, mtoto akiwa kwenye ile *incubator* hatimaye atakaa pale mpaka muda utafika, mzazi ataruhusiwa kurudi nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kazi inaanza hapo anaporudi nyumbani. Huyo mtoto anaporudi nyumbani, chumba chake anachokaa inabidi kwanza kiwe chumba maalum na chumba kile kinatakiwa kuwe na taa saa 24. Hakuna kuzima taa ili kumjengea mazingira yale ya joto. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kwenye kile chumba zaidi ya mama na huyo baba, hakuna mtu mwingine anayetakiwa aingie kwa sababu, huenda mkapeleka maambukizi *(infections),* kwa sababu kila mtu anatoka eneo lake analolijua yeye mwenyewe. Kwa hiyo, uangalizi unakuwa ni mkubwa sana. Sasa ni nini ninachotaka kukisema hapa?

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, hata katika Muswada huu kuwapa hawa akina baba hizo siku saba, nalo ni muhimu. Nikirejea nyuma, kuanzia siku ile ambayo mama amejifungua, kumpa nafasi ya likizo yake mpaka ufike ule muda wake rasmi wa

kujifungua, nayo ina umuhimu mkubwa sana. Baada ya hapo sasa ndiyo kumwongezea ile likizo yake ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza na kusema kwamba, hii wiki moja nayo ni muhimu, lakini ushauri unaotakiwa hapa ni kwamba, akina baba ndani ya Bunge hili na kote wanakonisikia Tanzania huko, msipewe ile wiki moja mkafanya shughuli zenu binafsi. Mmepewa ile wiki moja, ili mumsaidie mama kumlea huyo mtoto ambaye amezaliwa. Kama ni mapumziko subiri wakati mwingine na siyo katika kipindi tu cha juma hilo moja, hata ukiwa mfanyakazi, ukirudi kazini jua kwamba, mke wako amejifungua watoto njiti, anahitaji msaada.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, bila baba hakuna mtoto, na bila mama hakuna mtoto. Mimba haiwezi kutungwa peke yake, ni lazima wote tunakuwa na kazi ya kufanya ili mtoto aje duniani. Kwa hiyo, hilo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naipongeza sana Wizara kwa kuleta huu Muswada na umekuja kwa wakati mwafaka. Jambo letu kubwa sisi kama wanawake, kama wanaume na kama wawakilishi wa Watanzania, tupitishe Muswada huu kwa maslahi mapana ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtoa hoja, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi ya kuja kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi za mwaka 2024 *[The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024]*.

Mheshimiwa Spika, katika uchangiaji, jumla ya Waheshimiwa Wabunge watano wamepata nafasi ya kuchangia Muswada huu. Kipekee kabisa nachukua fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa namna ambavyo amekuwa nasi karibu wakati wote wa kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati walitoa maoni na ushauri ambao umekuwa na tija kubwa kwenye kuboresha Muswada huu. Pia Serikali ilipokea maoni na ushauri kwa jicho la kipekee na ikaona umuhimu mkubwa wa kuweza kuyapokea na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana utaona yale yote ambayo Kamati ya Bunge ilishauri kwa kiwango kikubwa, Serikali tumeyapokea na tumeyafanyia kazi na ni sehemu ya Muswada. Tafsiri yake ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge walisimamia vizuri suala hili na wameshauri katika namna ambayo itasababisha kuboresha vema sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika miaka yake ya uongozi amevutia uwekezaji mkubwa sana nchini na kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji wa biashara. Hii imesababisha uanzishwaji wa miradi mingi na mikubwa ambayo imeleta pia uwepo wa mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa. Hivyo, ilikuwa ni wakati muhimu kwa hivi sasa kuweza kupitia sheria zetu na kuzifanya ziwe rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania siyo kisiwa, tunashindana na watu katika maeneo mengi. Moja kati ya eneo kubwa hivi sasa katika kuvutia uwekezaji ni suala la nguvu kazi. Marekebisho haya ya sheria yanatusababisha kuwa washindani katika eneo hili kwa kuwa na nguvu kazi ambayo inaweza ikaaminika na sheria zetu pia zikaaminika kuweza kuvutia uwekezaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mizuri. Nimesikiliza hoja, asilimia kubwa sana walijielekeza katika Ibara ya Saba ya Muswada, ambayo imetufanya tufanye marekebisho kwa

sababu, tulikutana na *situation* ambayo haikuwahi kutokea awali hasa wakati wa ugonjwa wa *Covid* ambapo changamoto ilikuwa kubwa na sheria yetu ilikuwa kimya. Marekebisho haya yanatupa nafasi iwapo itatokea changamoto kama hii, tuna namna ya kuweza kuenenda na kuweza kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, tumepokea pongezi na Maoni ya Kamati juu ya muda ulioongezwa kwa mzazi ambaye anajifungua mtoto ambaye ni njiti na zile siku alizoongezwa baba. Haya yalikuwa ni sehemu ya michango yenu ya kuona namna nzuri ya kuliweka sawasawa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, imezungumzwa hoja ya Sheria ya Ajira kwa wageni, hasa katika eneo la utoaji wa kibali cha kazi Daraja A ambapo, moja kati ya changamoto kubwa ilikuwa ni mtu anayepewa kibali cha kazi cha Daraja A inapotokea ana jambo lingine la kufanya ndani ya nchi katika uwekezaji wake alikuwa anatakiwa kuomba kibali kingine. Hii ilikuwa ni moja kati ya changamoto kubwa na ilikuwa ni *red tap* katika *investment* ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Marekebisho haya yanalenga kwenda kutatua changamoto hiyo na hivi sasa akishapatiwa kibali cha kazi, basi ataendeleanacho kwa utaratibu ambao Kamishna ameelekezwa kuufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha siyo Muswada tu, bali hata masharti mengine ya sheria mama. Kwa ujumla, maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba, suala la Marekebisho ya Sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili na ni jambo endelevu. Ndiyo maana kila mwaka Serikali inakuja na Muswada wa aina hii ili kuboresha masharti ya Sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Bill 2024)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 7, kina marekebisho ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, hii *state of emergency* hapa, hebu fafanua kidogo. Kwa nini *marginal note* inasomeka kama *state of emergency?*

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika *spirit* ya *provision* hii, lengo kubwa ni kuweka utaratibu katika mazingira ambayo yatakuwa yana udharura na neno ambalo linaonekana lingeweza kutumika hapo lilikuwa ni hii *state of emergency*. Maana yake ime-*cover* matukio mengi zaidi ukiacha hata hayo mengine ya ugonjwa na milipuko mingine ambayo imekuwa *stated* ndani ya *provision.*

**MWENYEKITI:** Mnaiona changamoto ya kutumia haya maneno? Labda tutafute mengine, kwa sababu, mtu pekee nchini anayeweza ku-*declare state of emergency* ni Mheshimiwa Rais na hata Katiba ndivyo inavyosema na pia sheria yetu inayohusu *emergency* inasema hivyo. Kwa hiyo, hapa tukisema kwamba kutakuwa na *agreement* kati ya mwajiri na wale waajiriwa kuhusu *state of emergency,* yaani hii lugha kidogo inaleta changamoto. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana nawe kwa sababu, neno hili pia limetafsirika katika baadhi ya sheria likimaanisha hicho ambacho umekisema. Ili kutokuharibu maana iliyokusudiwa, bado tunaweza tukaweka maneno "*agreement in case of emergency*" badala ya kuweka ile "*state of emergency*".

Mheshimiwa Spika, lengo kuu kwenye ule udharura ni kutafuta neno ambalo litakuwa lina-*encompass* neno udharura. Kwa hiyo, tunaona kwamba, badala ya kuweka "*state of emergency*", inaweza ikabaki "*in case of emergency.*"

**MWENYEKITI:** Huku kwenye *provision* kwenyewe kuna hayo maneno yaliandikwa moja kwa moja. Mimi kwangu siyaoni au kuna aliyeyaona? Nadhani ni kwenye *marginal note* tu yalikuwa yanasomeka hivyo, si ndiyo?

Sawa. Kwa hiyo, *marginal note* itasomeka kama "*agreement in case of emergency.*" Haya, ahsante sana.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na narekebisho yake)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kupanga upya kifungu cha 9 hadi 37 na kuwa kifungu cha 10 hadi 38.

*(Mpangilio Mpya wa vifungu vya Muswada Uliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa mwaka 2024 *(The Labor Laws (Amendments) Bill, 2024]* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba (Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labor Laws Amendments) Bill 2024)*, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kuhusu

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 (The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki, ahsante sana. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Husika *(A Bill for an Act to Amend Labour Laws in order to address Challenges Observed during Implementation of Various Provision in the Relevant Rules)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusomwa mara ya tatu, inaashiria kwamba upande wa Bunge tumeshamaliza kazi ambayo tulipaswa kufanya, ambayo ililetwa mbele yetu inayohusu Muswada huu wa Sheria. Sasa nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, nitumie fursa hii kuishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri ambao anafanya nao kazi hasa ambao walikuwa wanasimamia Muswada huu, Mheshimiwa Naibu Waziri na pia Mheshimiwa Waziri ambaye leo amapata nafasi ya kumwakilisha Waziri anayehusika. Tunakushukuru sana kwa utayari wako na kwa kazi nzuri uliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo, Watendaji wote wa Wizara tunawashukuru kwa ushirikiano wao na kwa Muswada huu, pia ushirikiano kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunawashukuru sana; na Kamati yetu kwa kweli imefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote ahsante sana kwa Mawazo mazuri ambayo mmepata nafasi ya kuwasikiliza wadau na kisha kuwapa Serikali na ninyi wenyewe mawazo yenu na Serikali imeyakubali.

Pia mawazo ambayo mmeyatoa Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata nafasi ya kuchangia hapa ndani, mmechangia mawazo mengi, mengine yalikuwa yanahusu Muswada moja kwa moja na mengine ni ya kiutendaji zaidi. Kwa hiyo, Serikali imechukua yote kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kueleza hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili naye kwa sehemu yake aweze kufanya yale ambayo anapaswa kufanya kwa mujibu wa Katiba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao waliingia Bungeni baada ya tangazo la wageni la awali kupita, niwatangaze hao kabla hatujaendelea na ratiba yetu. Hawa ni wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 100 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi Nzuguni B' Mkoani Dodoma, karibuni sana. Hawa naona wana bahati sana, wamekutana na Mheshimiwa Mbunge wao akiwa ana kazi maalumu hapa Bungeni. Kwa hiyo, ahsante sana kwa kuja na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea sasa na jambo lile ambalo tulikuwa tumelisogeza mbele kwa mujibu wa ratiba yetu ili tumalize hilo, kisha tutaahirisha Bunge.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MAAZIMIO YA BUNGE

## AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUWA MWENYEJI WA MKUTANO WA *MISSION 300* ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM TAREHE 27 - 28 JANUARI, 2025 NA KUHUDHURIWA NA WAKUU WA NCHI 21 ZA AFRIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Asia Halamga ambaye anakuja kuwasilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa Azimio.

Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika, maarufu kama *Mission 300* kwa mwaka 2025 chini ya Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kipekee kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 27 – 28 Januari, 2025 katika Jiji la Dar es Salaam kulifanyika Mkutano mkubwa wa Nishati Afrika *Mission 300* na umewakutanisha Wakuu wa Serikali na nchi za Afrika, Viongozi wa Biashara, Washirika wa Maendeleo, Wakuu wa Taasisi za Kimataifa ikiwemo *World Bank, IMF, IFDB* na *Rockefeller Foundation* pamoja na wadau wakuu

kwenye nyaja mbalimbali katika juhudi kubwa za kuwafikishia umeme watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo 2030.

Mheshimiwa Spika, Tanzania chini ya Rais wetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ilikuwa mwenyeji wa Mkutano huo mkubwa zaidi uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam huku ukihudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wapatao 21. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulilenga kutafuta majawabu ya tatizo la nishati Barani Afrika na kuharakisha ufikiwaji wa maendeleo endelevu katika Bara la Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa na kwa jitihada, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikijivunia kuwa Mtanzania na kuongozwa na Mheshimiwa Rais mwenye maono endelevu yanayolenga kuwanufaisha Watanzania wote, kiongozi wa mfano Barani Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoandaa Mkutano na kuuendesha mkutano, pamoja na hayo, vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, vilitekeleza majukumu yake kwa weledi na hivyo kuwa mfano kwa mataifa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tumeona na kushuhudia mkutano huo ulivyoandaliwa kwa weledi na viwango vya hali ya juu katika sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naweza kuuliza Bunge hili, nani kama Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Narudia tena, naomba kuliuliza Bunge lako Tukufu, ni nani kama Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nathubutu kutamka wazi hapa kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni zawadi kutoka kwa Mungu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuzawadia Mheshimiwa Rais, na kiongozi kama huyu ndani ya nchi yetu ya

Tanzania, ndani ya Bara letu la Afrika na dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ulikuwa na manufaa makubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu na Bara la Afrika. Nikianza na manufaa kwa nchi yetu: -

(a) Ni wazi wawekezaji katika sekta ya hoteli na malazi, sekta ya usafiri na usafirishaji, wauzaji wa vyakula na vinywaji, wauzaji wa bidhaa mbalimbali na sekta ya utalii wamenufaika sana kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu muhimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

(b) Kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano, wafanyabiashara wameweza kutengeneza mtandao katika biashara zao kwa kufanya mazungumzo ya kibiashara, yaani *business to business* na *business to customer (B2B and B2C)* pembezoni mwa mkutano huo; na

(c) Vilevile kupitia mkutano huo tumeingiza fedha za kigeni, suala ambalo limeleta manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Bara la Afrika na watu wake wamepata manufaa makubwa, kwani kupitia mkutano huo masuala mbalimbali yameazimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Mataifa mbalimbali yametoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yanayolenga kuimarisha nishati mbadala na jadidifu, kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi za kupikia;

(b) Kuzinduliwa kwa Mipango ya Kitaifa ya Nishati kwa lengo la kuvutia wawekezaji na mageuzi ya sera;

(c) Kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka Taasisi za Kifedha za Kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia;

(d) Kuvutia sekta binafsi kuwekeza mitaji katika sekta ya nishati Barani Afrika; na

(e) Kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam ambalo limelenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo 2030.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Dar es Salaam lina manufaa makubwa kwa Bara la Afrika kwani kupitia azimio hilo imekubalika kwamba upo umuhimu wa kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji wa nishati hasa kwa wanawake na wafanyakazi ili kuimarisha mustakabali endelevu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Azimio hili linasisitiza umuhimu wa kuunganisha nishati kati ya nchi za Afrika, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama jua, upepo, umeme wa maji, nishati za joto ardhi ili kuwa na mifumo imara ya nishati.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anafungua mkutano huo aliridhia masuala hayo hapo juu kwa kusema, naomba ninukuu; "Mkutano huu unazungumzia zaidi ya nishati, ni kuhusu kuzipa nguvu familia, kuinua mamilioni ya watu kutoka kwenye umaskini na kuleta matumaini na fursa kwa vijana, ni ahadi yetu kuwa mabadiliko ya kiuchumi, kukuza viwanda, kuunda ajira na kuchochea uvumbuzi Barani Afrika."

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, mafanikio yaliyopatikana na yanayotarajiwa ni makubwa na mazuri kwa Bara la Afrika na watu wake. Ninaweza kulifahamisha Bunge lako kwamba huu ni miongoni mwa mikutano inayohusu maslahi ya Waafrika uliofanyika kwa mafanikio makubwa katika ardhi yetu tukufu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisome Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mwaka 2025, kama ifuatavyo:-

Kwa Kuwa, Mkutano wa Nishati wa Afrika kwa mwaka 2025 umefanyika Jijini Dar es Salaam, nchini Tanzania na kuhudhuriwa na wageni takribani 2,600 wakiwemo Wakuu wa Serikali na nchi takribani 21 kutoka Barani Afrika, Mawaziri na viongozi mbalimbali wa taasisi za Kimataifa pamoja na taasisi za fedha, nishati na wadau wengine;

Na Kwa Kuwa, Mkutano huo ulifanyika kwa siku mbili kwa weledi na viwango vya hali ya juu ya Kimataifa kutokana na uratibu mzuri uliofanywa na Serikali nchini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Na Kwa Kuwa, Mkutano huu ulimalizika salama na mafanikio yake ni utekelezaji wa lengo namba saba la malengo endelevu *(SDGs);*

Na Kwa Kuwa, Mkutano huo umekuwa miongoni mwa Mikutano ya Kimataifa iliyotoa matokeo chanya kwa manufaa ya Bara la Afrika, ikiwemo kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam ambalo limekusudia kuhakikisha kila nchi inatimiza lengo la kufikia wananchi wote wasio na nishati ifikapo mwaka 2030, kujumuisha sekta binafsi kwa kuvutia mitaji kuwekeza kwenye sekta ya nishati, kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka taasisi za kifedha, Kimataifa kama Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia pamoja na Mataifa mbalimbali ya Kiafrika, kutoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yaliyolenga kuimarisha mbadala na jadidifu kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi ya kupikia;

Na Kwa Kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme;

Na Kwa Kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 Watanzania wote watakuwa wafikiwa na miundombinu ya umeme;

Na Kwa Kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 75% ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye…

Mheshimiwa Spika, ninaomba kurudia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 75% ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia, na hatimaye ifikapo 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia; *(Makofi)*

Na Kwa Kuwa, ni wazi kuwa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa mwaka 2025 umefanyika na kukamilika kikamilifu na kwa mafanikio makubwa nchini Tanzania chini ya Rais mwenyeji Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan;

Kwa Hiyo Basi, Bunge hili katika Mkutano wake wa 18, Kikao cha Nne, tarehe 31 Januari, 2025 linaanzimia kwa dhati na kwa kauli moja...

Mheshimiwa Spika, naomba nisome maazimio kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme. *(Makofi)*

- Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme; *(Makofi)*

- Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 75% ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye 2034 Watanzania wote wapate nishati safi ya kupikia; *(Makofi)*

- Kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika dhamira yake ya kuwapatia Watanzania wote nishati ya umeme na nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kurudia tena, kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya kuwapatia Watanzania wote nishati ya umeme na nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa hasa kwa jitihada za Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa ni mfano wa kuigwa kwa Tanzania, Afrika na dunia, naomba kutoa hoja.

**AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUWA MWENYEJI WA MKUTANO WA NISHATI AFRIKA *(MISSION 300)* KWA MWAKA 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023)*

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kipekee ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba tarehe 27 - 28 Januari, 2025 katika Jiji la Dar es Saalam kulifanyika Mkutano mkubwa wa Nishati Afrika au *(Mission 300)* na umewakutanisha wakuu wa Serikali na nchi za Afrika , viongozi wa biashara, washirika wa maendeleo, wakuuu wa Taasisi za Kimataifa ikiwemo *World Bank, IMF , AFDB* na *Rockerfeller Foundation* pamoja na wadau wakuu

kwenye nyanja mbalimbali katika juhudi kubwa za kuwafikishia umeme watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania chini ya Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ilikuwa mwenyeji wa Mkutano huo mkubwa zaidi uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam, huku ukihudhuriwa na Wakuu wa nchi na Serikali wapatao 21. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulilenga kutafuta majawabu ya tatizo la nishati Barani Afrika na kuharakisha ufikiwaji wa maendeleo endelevu katika Bara la Afrika kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa na kwa kujidai nasimama mbele ya Bunge lako tukufu nikijivunia kuwa Mtanzania na kuongozwa na Rais mwenye maono endelevu yanayolenga kuwanufaisha Watanzania wote, Kiongozi wa Mfano Barani Afrika na Dunia kwa ujumla, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoandaa Mkutano na kuendesha Mkutano. Pamoja na hayo, Vyombo vya Ulinzi na Usalama chini ya Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan vilitekeleza majukumu yake kwa weledi na hivyo kuwa mfano kwa Mataifa mengine Barani Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, wote tumeona na kushuhudia Mkutano huo ulivyoandaliwa kwa weledi na viwango vya hali ya juu katika sekta zote. Mheshimiwa Spika, naweza kuuliza Bunge hili nani kama Rais Samia Suluhu Hassan?, nathubutu kutamka wazi hapa kuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni zawadi kutoka kwa Mungu na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuzawadia Rais na Kiongozi kama huyu.

**Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo ulikuwa na manufaa makubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu na Bara zima la Afrika. Nikianza na manufaa kwa nchi yetu:-

a) Ni wazi Wawekezaji katika Sekta ya Hoteli na Malazi, Sekta ya usafiri na usafirishaji, Wauzaji wa Vyakula na vinywaji, wauzaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na sekta ya utalii wamenufaika sana kwa Tanzania kuwa Mwenyeji wa Mkutano huu;

b) Kwa Tanzania kuwa Mwenyeji wa Mkutano, Wafanyabiashara wameweza kutengeneza mtandao katika biashara zao kwa kufanya mazungumzo ya kibiashara yaani *Business to Business* na *Business to Customer* (B2B na B2C) pembezoni mwa Mkutano huo;

c) Vilevile kupitia Mkutano huo tumeingiza fedha za kigeni suala ambalo limeleta manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Bara la Afrika na watu wake wamepata manufaa makubwa kwani kupitia Mkutano huo masuala mbalimbali yameazimiwa kama ifuatavyo:-

a) Mataifa mbalimbali yametoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yanayolenga kuimarisha nishati mbadala na jadidifu, kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi za kupikia;

b) Kuzinduliwa kwa Mipango ya Kitaifa ya nishati kwa lengo la kuvutia wawekezaji na mageuzi ya Sera;

c) Kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka Taasisi za Kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia;

d) Kuvutia Sekta Binafsi kuwekeza mitaji katika Sekta ya nishati Barani Afrika; na

e) Kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam ambalo limelenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo 2030.

**Mheshimiwa Spika,** Azimo la Dar es Salaam linamanufaa makubwa kwa Bara la Afrika kwani kupitia azimio hilo imekubalika kwamba upo umuhimu wa kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji wa nishati hasa kwa Wanawake na Wafanyakazi ili kuimarisha mustakabali endelevu. Vilevile, Azimio

hili linasisitiza umuhimu wa kuunganisha nishati kati ya nchi za Afrika, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama jua , upepo, umeme wa maji, nishati za joto ardhi ili kuwa na mifumo imara ya nishati.

**Mheshimiwa Spika,** katika maelezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anafungua mkutano huo alidhihirisha masuala hayo hapo juu kwa kusema nanukuu ***"Mkutano huu unazungumzia zaidi ya nishati, ni kuhusu kuzipa nguvu familia, kuinua mamilioni ya watu kutoka kwenye umaskini na kuleta matumaini na fursa kwa vijana. Ni ahadi yetu kuwa, mabadiliko ya kiuchumi, kukuza viwanda, kuunda ajira na kuchochea uvumbuzi Barani Afrika".*** kwa msingi huo mafanikio yaliyopatikana na yanayotarajiwa ni makubwa na mazuri kwa Bara la Afrika na watu wake. Ninaweza kulifahamisha Bunge lako kwamba huu ni miongoni mwa Mikutano inayohusu maslahi ya Waafrika uliofanyika kwa mafanikio makubwa katika ardhi yetu tukufu ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisome Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mwaka 2025, kama ifuatavyo:-

**NA KWA KUWA,** Mkutano wa Nishati wa Afrika kwa mwaka 2025 umefanyika jijini Dare es Saalam nchini Tanzania na kuhudhuriwa na wageni takribani 2,600 wakiwemo Wakuu wa Serikali na nchi takribani 21 kutoka Barani Afrika, Mawaziri na Viongozi mbalimbali wa Taasisi za Kimataifa za Fedha na Nishati na wadau wengine;

**NA KWA KUWA,** Mkutano huo ulifanyika kwa siku mbili kwa weledi na viwango vya hali ya juu Kimataifa kutokana na uratibu mzuri uliofanywa na Serikali chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

**NA KWA KUWA,** Mkutano huo ulimalizika salama na mafanikio yake ni kufikiwa kwa malengo ni utekelezaji wa Lengo Na. 7 la Malengo Endelevu *(SDG's);*

**NA KWA KUWA,** Mkutano huo umekuwa miongoni mwa Mikutano ya Kimataifa iliyotoa matokeo chanya kwa manufaa ya Bara la Afrika ikiwemo kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam ambalo limekusudia kuhakikisha kila nchi inatimiza lengo la kufikia wananchi wote wasio na nishati ifikapo mwaka 2030, kujumuisha Sekta Binafsi kwa kuvutia mitaji kuwekeza kwenye sekta ya nishati, kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka Taasisi za Kifedha za Kimataifa kama Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia; pamoja na Mataifa mbalimbali ya Kiafrika kutoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yanayolenga kuimarisha nishati mbadala na jadidifu, kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi za kupikia;

**NA KWA KUWA**, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme;

**NA KWA KUWA,** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia;

**NA KWA KUWA,** ni wazi kuwa Mkutano wa Nishati wa Afrika kwa mwaka 2025 umefanyika na kukamilika kikamilifu na kwa mafanikio makubwa nchini Tanzania chini ya Rais Mwenyeji Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan;

**KWA HIYO BASI,** Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nane, Kikao cha Nne, tarehe 31 Januari, 2025, linaazimia kwa dhati na Kauli moja:-

a) Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Mwenyeji na kufanikisha Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mwaka 2025 kwa weledi na viwango vya Kimataifa;

b) Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme;

c) Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia; na

d) Kumuunga mkono Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika dhamira yake ya kuwapatia Watanzania wote nishati ya umeme na nishati safi ya kupikia.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb.
**VITI MAALUM**
31 Januari, 2025

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii naona hoja imeungwa mkono na watu wote isipokuwa mmoja. Ahsanteni sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, azimio limewasilishwa na sasa nimepokea majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wangependa kuchangia hoja hii kisha mtoa hoja atapewa nafasi ya kuhitimisha na tutahojiwa.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanueli Kingu, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza ajiandae. Kila mchangiaji atachangia dakika tano. Ukichangia pungufu ya hapo, tutashukuru; ukitaka kuendelea itaniwia ngumu sana kukatisha sifa za Mheshimiwa Rais kwa sababu ziko nyingi. Sasa

katika hizo nyingi chagua chache ili umalize ndani ya dakika tano.

Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na kwa unyenyekevu mkubwa naomba kusimama mbele yenu kwa minajili ya kutoa mchango wangu kuhusu Azimio la Kumuunga Mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha Mkutano huu Mkuu kwa kuzungumzia masuala ya nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze maelezo yangu kwa kunukuu maneno mazuri sana ya msomi mmoja na mwandishi wa vitabu mwenye ulemavu wa macho ambaye anaitwa Helen Keller. Aliulizwa na Waandishi wa Habari, ni jambo gani linamsikitisha sana hapa duniani? Alisema anasikitishwa anapowaona watu wenye macho kamili, lakini hawana ndoto katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ndoto zake za kuwakutanisha viongozi wenzake wapatao 21 kutoka maeneo mbalimbali ya Bara la Afrika ili kuzungumzia mustakabali wa nishati hasa katika maeneo ya vijiji Kusini mwa Jangwa la Sahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kwamba nchi yetu kwa miaka mingi sana imekuwa ikitegemewa kutoa mwongozo katika masuala ya kisiasa, maendeleo na uchumi katika Bara la Afrika. Tulifanya hivyo kwa ukombozi wa Kusini mwa Afrika, tukafanya hivyo katika kutetea utamaduni wa Afrika na sasa nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anauendeleza utamaduni huo wa kutetea masuala ya msingi ya mahitaji ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, namshukuru kwa kuturudisha huko. Tunapokuwa na mambo ya msingi, tunapokuwa na matatizo ya msingi ndani na nje ya Bara la Afrika,

sauti ya Tanzania, msimamo wa Tanzania umekuwa ukihitajika sana katika kuwapa faraja hasa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kuna watu wapatao zaidi ya milioni 300 katika Bara la Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao wanahitaji nishati, lakini kwa bahati mbaya sana hawana nishati hiyo muhimu. Matokeo yake ni nini? Wapo Waafrika wenzetu wamepoteza maisha kutokana na matumizi mabaya ya nishati hiyo. Kwa msingi huo, basi tuna kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutoa ukombozi kwa watu hawa niliowataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bara la Afrika lina vyanzo vingi sana vya nishati, kama vile upepo, jua, mawimbi ya bahari, gesi asilia, lakini bado matumizi ya nishati salama katika Bara la Afrika yako chini sana. Kwa msingi huo, naviomba vyuo vikuu vya Tanzania viendeleze mafunzo na utafiti wa teknolojia ya matumizi ya nishati ya upepo, maji ya bahari, gesi asilia, *biogas* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naviomba vyuo vikuu vya Tanzania vitengeneze majiko sanifu ili tupunguze uagizaji wa majiko haya kutoka nje. Mwalimu alitufundisha kujenga Taifa linalojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo basi, ninayo kila sababu ya kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya hizi dakika tano.

Mheshimiwa Spika, Afrika inakadiriwa kuwa na watu bilioni 1.5, kwa maana ya 1,500,000 na katika hiyo 60% ya *population* ya Afrika ni vijana walio chini ya miaka 25. Ukiangalia kwa mujibu wa maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huu wa *Mission* Milioni 300 utagundua kwamba *population* ya watu milioni 185 ambao ni nguvu kazi ya Afrika wanasogezewa miundombinu ambayo itawasaidia kupata ajira katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mchumi William Smith ana kitu anakiita *invisible hand* katika uchumi. Kwa maazimio haya yaliyofikiwa Dar es Salaam, nitumie nafasi hii kama Mbunge ninayetokana na wananchi wapendwa kabisa wa Singida Magharibi kusema kwamba Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliokaa wiki mbili zilizopita haujafanya makosa kumleta Dkt. Samia Suluhu Hassan kama mgombea wao wa nafasi ya kiti cha Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiki alichokifanya Mheshimiwa Rais wetu, haya yalikuwa ni maazimio ya *World Bank Group* na *African Development Group* Aprili, 2024 walipoweka *target* ya kuwafikia watu milioni 300. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameionesha dunia, ameionesha Afrika kwamba yeye ni mwanamke shupavu, Rais jasiri, mwenye uwezo wa kuleta mabadiliko duniani licha ya watu wengine wanaweza wakafikiri kwamba mataifa ya Afrika yanaweza yasioneshe uongozi duniani. Rais wetu ameli-*prove* hilo. Bunge hili hatuna sababu ya kuacha kumpongeza na kutoa azimio la kusimama naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, angalia weledi wa Rais huyu. Ukitaka kuamini kuwa Rais huyu ni mweledi kwa jambo hili kubwa alilolifanya ambalo litakwenda ku-*trigger* kuleta *employment*, litakwenda ku-*trigger* kuongeza *efficiency* ya kazi na zaidi kubwa litakwenda kupunguza *urban-rural migration* kwa sababu watu wengi wa vijijini ambao kwa *statistics* hizi za dunia inaonesha watu milioni 185 watakwenda kufikiwa na huduma hii, wengi wao wakiwa vijana. Kwa hiyo, janga la ajira kwa vijana linakwenda kupatiwa ufumbuzi. Kwa nini Bunge hili lisimpongeze Rais huyu? Kwa nini Bunge hili lisiinuke na kusema ahsante kwa Rais huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuamini kwamba Rais huyu ni mtu makini, ni mwanamke jasiri na shupavu angalia hata safu ya wasaidizi wake wanaomsaidia kazi, kuanzia kwa Mawaziri. Ona alivyo na safu ya Mawaziri walivyo *humble*. Nenda kwenye safu ya Waziri Mkuu na Msaidizi wake Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Angalia unyenyekevu wao namna wanavyomsaidia Rais huyu kufikisha ndoto waliyonayo ya kuwapatia Watanzania na sasa amekuwa mwangwi wa kuitangazia dunia na Afrika kwamba umeme utakwenda kuwasaidia Waafrika wengi na vijana kwenye ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapotaja haya, tusimwache Naibu Waziri Mkuu ambaye ndiye sekta yake ameishikilia. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, hongera sana kaka yangu, wewe umekuwa mnyenyekevu, unamsaidia kaka yangu Mheshimiwa Majaliwa na ndiyo maana mageuzi makubwa ya kiuchumi yanafanyika kwenye Taifa hili kwa sababu mnampa Mheshimiwa Rais utulivu wa kufanya kazi. Mheshimiwa Majaliwa, kaka yangu hongera, Mheshimiwa Dkt. Biteko, kaka yangu hongera na mawaziri wote ninawapa hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ukisoma *data* za dunia zinatuonesha kwamba kwa Tanzania peke yake, idadi ya kaya ambazo hazijafikiwa ambazo tukipiga mahesabu tutakapokuwa tumemaliza kuzifikia kaya zote uchumi wa Tanzania kwa *projection* inaonesha, Bara la Afrika ukianza kumega kidogo kidogo ukija katika ngazi ya Taifa mwaka 2050 Afrika inakwenda kuwa na *population* ya watu *2.5 billion.*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa idadi ya watu milioni 17 ambao watafikiwa na umeme wa uzalishaji hapa Tanzania inaonesha kwamba *stimulation* ya uzalishaji wa umeme kwa Taifa letu itakwenda kuongezeka mara kumi mpaka kufika 2050. Kwa nini tusiinuke na kusema ahsante Mama Samia? Kwa nini Bunge hili lisisimame na kusema pongezi Rais Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa sababu tumesema mama anaupiga mwingi, nasi Wana-CCM

tumesema ndiye mgombea wetu na hilo halina mjadala. Kwa nini sasa Bunge hili pia mwakani tukija mapema tusiseme mitano tena kwa Spika wetu? Ama namna gani jamani? Kwa nini tumemaliza na mama, mwezi wa Kumi tunapokuja tunasema mitano tena kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, pia nami nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kutoa maoni yangu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huu wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitumnie nafasi hii kuieleza dunia juu ya umahiri mkubwa aliyonao Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa katika masuala yote ya kidplomasia.

Mheshimiwa Spika, tutakubaliana tu wote kwamba halikuwa jambo rahisi kuweza kushawishi dunia nzima, kuweza kukubali kwamba Tanzania inaweza kuwa Mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Nishati wa Afrika. Ninasema hivyo kwa sababu Mkutano huo ulijumuisha wakuu wa nchi zaidi ya 20, lakini wako wakuu wa taasisi za kimataifa mbalimbali duniani zilikuja hapa Tanzania. Hiyo ni kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaonesha kwamba Rais wetu mbali na mambo mengi ambayo amefanya katika nchi yetu, ameweka historia nyingine ya kuwa Rais mahiri, Rais mpambanaji, nasi kama Watanzania tuna sababu ya kuendelea kumuunga mkono Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu umefanikiwa katika kipindi ambacho jamii nyingi sana za Afrika zilikuwa na maono hasi juu ya

uongozi unaomhusu mwanamke. Walikuwa hawaamini kwamba mwanamke anaweza akafanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amebomoa hizo kuta na ametuma salamu duniani ili dunia ijue kwamba suala la uongozi halihusiani na suala la jinsia, bali uongozi unahusiana na suala la uwezo alionao mtu. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala kama hili, fursa ya mkutano mkubwa kama huu, ni fursa ambayo nchi nyingi huwa zinatamani kwamba jambo hili lifanyike kwenye nchi yake. Kwa hiyo, sisi kama Tanzania, na kama Afrika ziko faida mbalimbali ambazo kama nchi tumezipata. Kutokana na muda, nitataja chache.

Mheshimiwa Spika, faida mojawapo, tumeweza kukuza fursa za kiuchumi na wafanyabiashara wamenufaika. Faida ya pili ni kwamba, tunafahamu Rais wetu ndiye *champion* mkubwa wa masuala ya utalii ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tumetumia mkutano huu kuweza kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii. Pia, tunafahamu wafanyabiashara wamepata *network* na *connection* mbalimbali kwa ajili ya biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, faida nyingine kubwa ambazo ni za muhimu sana, tunafahamu katika Mkutano huo Rais wa *World Bank* ametoa pongezi kwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na ameitaja Tanzania kuwa ndiyo kinara wa mapinduzi ya nishati vijijini. Pia, hilo limefanikiwa kutokana na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeona katika nchi yetu, tunayo mikoa mingi ambayo ilikuwa bado haijaingizwa kwenye gridi ya Taifa. Tunavyoongea hivi sasa Mkoa wa Kigoma umeingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Tunavyoongea hivi sasa, Mkoa wetu wa Songwe ambao kwa miaka mingi tulikuwa tuna tatizo la kukatikakatika kwa umeme, sasa hivi Mkoa wa Songwe umeingizwa kwenye gridi ya Taifa. Pia, tunavyoongea sasa hivi, tumeweza kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ndani ya Tanzania.

Sasa tunakwenda kuingia kwenye awamu nyingine ya pili ya kusambaza umeme katika vitongoji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ni kubwa na ndiyo maana Rais wa *World Bank* akasema kwamba nchi nyingine za Afrika zina kila sababu ya kuiga kwa Tanzania. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunafahamu kwa muda wa miaka mingi tulikuwa tunatamani kwanza tuwe na umeme ambao utatutosheleza sisi kama nchi. Pia, tulikuwa tunatamani tuwe na umeme ambao tutaweza kuuza katika nchi nyingine. Hata hivyo, kwa kasi hii ambayo Mheshimiwa Rais anayokwenda nayo na kwa mageuzi haya makubwa katika nishati ya umeme, ni wazi kwamba siku siyo nyingi tunakwenda kuanza kuuza umeme katika nchi nyingine za Afrika ikiwepo nchi ya Zambia, Comoro na Mozambique.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sisi kama nchi ya Tanzania muda siyo mrefu tunakwenda kujitosheleza kwa umeme na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amesema kwamba, ana ujasiri kwamba sasa vitongoji vyote ndani ya nchi yetu vinakwenda kupata umeme. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi mazuri ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya, tunaona kwamba muda hautoshi, sisi kama Chama cha Mapinduzi kutokana na kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya, ndiyo maana sisi kama Wajumbe kupitia Mkutano Mkuu tulisema kwamba hatuna dakika za kupoteza zaidi ya kupitisha jina moja la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili aweze kwenda kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Urais katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulifanya hivyo siyo kwamba yale yalikuwa ni maoni yetu Wajumbe wa Mkutano Mkuu, hapana. Sisi tulikuwa ni wawakilishi wa Wana-CCM wengi ambao tumewaacha katika mikoa yetu. Katika kuthibitisha hilo ndiyo maana umeona baada ya lile Azimio la Mkutano Mkuu, tumeona

makundi makubwa ya Wana-CCM na makundi makubwa ya wananchi katika mikoa yetu wakiendelea kuunga mkono Azimio la Mkutano Mkuu na kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anatosha, tuweze kumpa mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi na tunafahamu kwamba nchi yetu Mheshimiwa Rais Samia ameitoa mbali sana na kwa hapa alipofika ni wazi kwamba, wapinzani wana kazi ya kufanya katika uchaguzi wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, wengine walitamani kwamba mambo mengi yasifanyike, lakini mambo mengi yamefanyika, walitamani Bwawa la Mwalimu Nyerere lisikamilike, lakini limekamilika; walitamani umeme usipelekwe vijijini, umepelekwa vijijini na sasa tunakwenda kupeleka umeme kwenye vitongoji; Walitamani kuona kwamba, wanawake wakiendelea kutumia nishati ambazo zinahatarisha afya zao (kuni), lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshasema kwamba ifikapo mwaka 2035 wanawake wote watakuwa wanatumia nishati ambayo ni safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge tunapenda tuchukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na tunasema kwamba Rais wetu anatosha kuweza kutuongoza katika miaka mitano inayofuata, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuunga mkono hoja ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunampongeza? Tunampongeza kwa sababu kwanza katika historia ya Tanzania, mkutano wa aina hii na mkubwa katika eneo la nishati haujawahi kutokea toka tupate Uhuru. Haijawahi! Kama tumewahi kupata mkutano mkubwa kama huu ni kwenye maeneo mengine, lakini

kwenye upande wa nishati ni mkutano wa kwanza katika historia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu kwanza siyo tu anapongezwa, anapongezwa kutokana na kazi ambazo amezifanya, zimeonekana na zimeleta matunda. Katika ujenzi wa Bwawa la Nyerere watu wengi waliamini kwamba lile bwawa halitaweza kukamilika, lakini amelisimamia mpaka limekamilika na sasa hivi Tanzania inasifika kuwa na umeme mwingi ambao hatuna hata mahali pa kuupeleka na sasa tunauuza nchi za nje. Hii ni kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameonesha maono makubwa, uzalendo, uadilifu, umahiri na kusimamia masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika nchi yetu. Kwa namna alivyofanya kazi, ndiyo maana tunayo kila sababu ya kusimama na kumpongeza na kumtia moyo ili aendelee katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya kuandaa mkutano huu, ni mkutano mkubwa wa watu wengi zaidi ya 2,600 kwenye mkutano, wakuu wa nchi zaidi ya 21 kuja kwenye nchi yetu; maana yake nini? Maana yake tumepata fedha nyingi za kigeni, tumepata uchumi mzuri, lakini zaidi ya hapo, unatokana na msimamo wake wa kusimamia nishati safi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ajenda ambazo amekuwa akizisimamia na ambazo tumeona Tanzania toka miaka nenda rudi, ilikuwa inasimamia ajenda mbalimbali na tunafanikiwa. Hii ndiyo ishara kwamba Tanzania ina viongozi wakubwa, waadilifu, wenye maono na wanaotakiwa kuheshimika katika dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii katika hili lililofanyika ni ishara kwamba tunaweza tukawa *champion* wa kuiunganisha Afrika yote tukawa kitu kimoja. Tukiunganisha Afrika na jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amesimamia nishati safi, maana yake nini?

Maana yake itatusaidia kupunguza umaskini wa Watanzania. Kwa sababu umeme ukipatikana na nishati safi ikipatikana kila mahali, umaskini wa Tanzania utapungua, pia uchumi wa nchi za Afrika utapungua, na zaidi ya hapo ajira mbalimbali zitakuwa zimetengenezwa. Kikubwa zaidi, amelinda afya za akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, afya za akina mama zitalindwa vizuri sana, ndiyo maana ameendelea na hiyo kwamba tulinde afya kwa kutumia nishati safi kwa kila mmoja. Kwa kufanya hivyo, tuna kila sababu ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, amesimamia ujenzi wa *SGR* ambayo imeleta mabadiliko makubwa sana. Tulikuwa tunaona magari yote yalikuwa yanatumia mafuta ya kigeni, mitambo mingi ilikuwa inatumia hiyo, *SGR* sasa inatumia umeme unaozalishwa hapa hapa nchini na sasa ni mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukienda tena tukaanza kutumia nishati kwenye kupikia na kila mahali, maana yake fedha za kigeni zitakuwa zimepona na tutazielekeza katika maeneo mengine. Kwa hiyo, hiyo ni kazi kubwa ambayo ameileta na mabadiliko makubwa katika usafirishaji hapa nchini na kuleta maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kwa kazi hii, kwa uzalendo huu, kwa uadilifu huu na mambo ambayo anaendelea kuyasimamia, ndiyo maana sisi Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi tulipokutana Dodoma, tukasema huyu huyu anatosha tena atuongoze kwa miaka mingine mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania, wananchi na Wabunge wenzangu, tumuunge mkono ili maendeleo makubwa ya nchi hii yapatikane na vijana wa nchi hii wapate ajira kutokana na ajenda hizi kubwa ambazo zimetokana na kufanikiwa kwa mkutano huu ambao umeandaliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Naibu wake na Baraza zima kwa kazi kubwa mliyoifanya katika kufanikisha mkutano huu. Tuendelee kumuunga mkono ili tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kupata fursa hii adhimu ya kuchangia katika azimio hili muhimu sana la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ku-*host* mkutano mkubwa sana wa kidunia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuileta Afrika na dunia nchini Tanzania. Tumesikia hapa kwamba Mkutano huu umehudhuriwa na Wakuu wa Nchi zaidi ya 20, lakini umehudhuriwa na Wajumbe zaidi ya 2,000 kutoka duniani kote. Dunia ilikuwa hapa katika siku hizi mbili na nilifuatilia. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Naibu Mawaziri, lakini na Wizara ya Nishati kwa kuratibu vizuri mkutano huu. Wageni wetu wamekuja na wameuona ukarimu wa Kitanzania. Yale ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyaonesha kwenye *Royal Tour,* wameyaona na nina uhakika wamerudi kwenda kuyasema mazuri ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maazimio haya au Azimio la Dar es Salaam, mambo makuu matatu yamewekwa. La kwanza, kuhakikisha kwamba kufikia mwaka 2030 Waafrika milioni 300 watapata *access* ya uhakika ya umeme; la pili, ni kuhakikisha

umeme huu unapatikana kwa gharamna ndogo; na la tatu, ni kuhakikisha Afrika inakuwa kinara wa matumizi ya nishati safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maazimio haya yanakwenda kumgusa moja kwa moja Mtanzania wa chini. Mkutano huu umekuwa na umuhimu mkubwa kwa sababu, tunapozungumzia mapinduzi katika Sekta ya Nishati, tunazungumzia mapinduzi ya viwanda, tunazungumzia uwekezaji mkubwa ndani ya nchi yetu, tunazungumzia mapinduzi makubwa katika uzalishaji wa chakula, tunazungumzia maendeleo vijijini, tunazungumzia maendeleo ya miundombinu, tunazungumzia mapinduzi ya biashara za kimtandao na mapinduzi ya elimu ya kimtandao, tunamzungumzia Mtanzania wa kawaida, na tunazungumzia kwa ukubwa zaidi suala la ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amezungumza vizuri sana kaka yangu Mheshimiwa Kingu, kwamba Bara la Afrika ndilo bara changa kuliko yote katika dunia hii sasa hivi. Kwa vile watu wengi zaidi ndani ya Afrika ni vijana, ninukuu, *World Bank Group* imesema kwamba, "maazimio haya yatakuwa ndiyo *cornerstone* ya kuanza kutatua tatizo la ajira kwa kundi kubwa na linaloongezeka la vijana Afrika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia mapinduzi ya viwanda, hakuna nchi duniani iliyoendelea pasipokuwa na maendeleo makubwa kwenye viwanda na hakutakuwa na viwanda bila kuwa na nishati ya kueleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza sasa, wakati Mheshimiwa Dkt. Adesina anafunga au anatoa wasilisho lake la mwisho alisema; "Ajenda hii siyo mpya katika Bara la Afrika, imekuwa inajadiliwa mara nyingi, lakini utendaji wake umekuwa mdogo. Sasa maazimio haya ya Dar es Salaam yawe ndiyo mwanzo wa utendaji wa uhakika wa utekelezaji wa ajenda hii." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakati wengine wanafikiria kuanza kutenda, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishaanza kutenda, ameshatenda na anaendelea kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kote, nchi zote zilizoendelea zina mchango mkubwa wa viongozi wenye maono ya kesho na unavyozungumza, wakati wengine wanawaza kuanza kutembea au kuanza kufikiri, Mheshimiwa Dkt. Samia ana mawazo ya kesho na alikwishafikiri.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza hivi sasa, Bwawa la Mwalimu Nyerere liko 98%, kumekuwa na kongamano la kuanza kutumia umeme wa jotoardhi ambalo lilifanyika mwaka 2024 mwezi Oktoba na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akatoa *commitment* kwamba mwaka huu wa 2025 umeme wa jotoardhi utaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza sasa hivi, mikataba mingi sana ya kuanza kutumia gesi asilia imesainiwa. Wakati watu wanazungumzia ajenda ya kuanza kutoa nishati yenye gharama nafuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa ruzuku kwenye gesi au nishati safi, 20% kwa walioko Dar es Salaam na 50% kwa mikoa yote. Kwa maana ya kwamba, mama aliyekuwa nyumbani, ambaye alikuwa anakwenda kujaza mtungi wa gesi kwa shilingi 20,000 mpaka 25,000, sasa hivi anakwenda kujaza kwa 10,000 mpaka shilingi 12,000. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza sasa hivi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa mitungi ya gesi zaidi ya 420,000 kwenda kwa akina mama ku-*champion* ajenda hii ya nishati safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza sasa hivi kuna Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mfupa uliokuwa umeshamshinda fisi, leo hii Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameuweka vizuri, wananchi wamelipwa fidia na mkataba ule mtauona hapa Bungeni na mambo yamekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amezungumza vizuri Mheshimiwa Hasunga, leo hii hapa ni kama ndoto. Tuna treni ya umeme inayotumia umeme wetu wenyewe na hapa tunapozungumza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa *commitment* kwamba nchi yetu itahakikisha inaunganisha nchi zote za jirani katika gridi yetu ya Taifa ili tuanze kuwauzia umeme. Nchi yetu imepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wengine wanawaza kuanza, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaitangazia dunia kwamba Tanzania inakuja, *they better watch out*. Tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, Kitabu cha Luka Sura ya 19:40 inasema; "Wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele." Sisi tumeamua kusema, tunasema kwa sababu tuna kila sababu ya kusema, lakini tutahakikisha kwamba sisi vijana wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tuko nyuma yake kumuunga mkono, lakini kubwa zaidi mcheza kwao hutunzwa.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi wametuonesha, lakini yale yalikuwa ni maono ya Wana-CCM wote zaidi ya milioni 12 katika nchi hii kwamba bado tuna imani kwamba nchi yetu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko katika mikono salama, kesho yetu ni bora. Tunaamini kwamba mapinduzi makubwa yatakayofanyika katika nchi hii mpaka ifikapo mwaka 2030 itakuwa mbali sana katika uchumi wa Afrika na dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca David Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nitangulie kwa kushukuru kupata fursa hii, lakini niseme tu kwa heshima na furaha kubwa, nimesimama leo nikiungana na Rais

wa Benki ya Dunia Bwana Ajay Banga, pamoja na Rais wa Benki ya Afrika Dkt. Adesina, wadau wote wa Sekta ya Nishati pamoja na wananchi wote wa Tanzania, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa aliyonayo katika Sekta ya Nishati, Diplomasia na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba, siyo mara ya kwanza Wakuu wa Nchi kuja kwenye Taifa letu. Tunayo rekodi. Ukiangalia mwaka 1999 wakati wa msiba wa Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere, walikuja Wakuu wa Mataifa 19. Siyo hivyo tu, tukiangalia mwaka 2019 kwenye Mkutano wa *SADC* walikuja Wakuu wa Mataifa 15. Hii ya sasa imevunja rekodi kwa kupokea Viongozi Wakuu wa Mataifa 35. Hiyo idadi iliyotajwa pale 21 hao ni Marais, lakini kuna Makamu wa Marais, Mawaziri Wakuu, Naibu Mawaziri Wakuu ambayo inaleta idadi ya karibu 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba mkutano huu umefanyika kwa kuzingatia mambo mengi sana. Haiwezekani mkutano huu ukafanyika, haya mambo hayatokei tu. Tunajua kazi kubwa iliyofanyika kwenye kuimarisha diplomasia ya Taifa hili. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa mstari wa mbele kuimarisha diplomasia.

Mheshimiwa Spika, tuna rekodi, amekuwa akialikwa kwenye mikutano mikubwa ambayo inajadili masuala mazima ya kiuchumi na mahusiano na Mataifa mengine. Mfano tu Novemba, 2024 amehudhuria Mkutano wa Mataifa Tajiri 20 *(G.20)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameshiriki Mkutano unaoitwa *FOCAC*. Mkutano huu yeye ndio aliyeteuliwa kuwa Msemaji wa Bara la Afrika. Fikiria Afrika ina Marais wangapi? Ina Marais wangapi? Lakini Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akateuliwa kuwa Msemaji wa Marais wote katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mambo hayatokei hivi hivi jamani. Ni hivi, niseme nisiseme? Niseme nisiseme? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Semaaa!

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ni hivi, kwa haya yanayofanyika na kwa hiki kilichofanyika, Mkutano Mkuu na mengine yote, haya mambo yamehalalisha maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi yaliyofanyika mwaka huu na mimi naungana kwa 100% na maamuzi waliyofanya Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limesababisha mataifa haya kushiriki Mkutano huu bila kuwa na tatizo lolote ni suala la amani na utulivu katika Taifa hili. Nitumie fursa hii kuvipongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa hili. Ninavyofahamu, hakuna nchi yoyote inayoweza kuleta kiongozi wake wa kitaifa bila vyombo vyake vya ulinzi na usalama kuhakikisha anakokwenda ni salama kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hii ni kwamba vyombo hivi vimejihakikishia kwamba nchi ya Tanzania ni nchi ya amani. Nami naomba kupitia Bunge lako Tukufu, Jeshi la Ulinzi na Usalama kwenye suala la amani wasi-*compromise* na mtu yeyote. Tunawaona wenzetu wa Mataifa mengine wanavyoteseka, tunawaona wamama, watoto na wazee wanavyoangamia. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili lisingefanyika kama ukuaji wa uchumi wa Taifa letu ungekuwa unasuasua, lakini watu hawa watakuwa walijihakikishia kwamba mpaka kufika hapa ni lazima kuna *facilities* za kutosha. Huwezi kuita Mataifa mengine yakaja kwenye nchi yako ukiwa una umeme wa kusuasua. Huwezi kuita Wakuu wa Mataifa mengine ukiwa unajua huna usafiri wa uhakika na ninyi ni mashuhuda, tuna ndege za kutosha na *airport* ya kisasa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia umeme, ndiyo usiseme. Leo tunazungumzia nchi yetu ina Megawati 3,404. Ukiangalia wakati tunapata Uhuru tulikuwa tuna Megawati 21 peke yake. Mama Samia amechukua nchi hii ikiwa ina Megawati 2,100. Sasa kuna ongezeko la Megawati 1,300 zilizoletwa na mama huyu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mkutano huu ni makubwa sana. Najua kwa sababu ya muda na wenzangu wameshayasema, sitaki kuyarudia, lakini kwa kifupi tumeona kwamba kufika mwaka 2,030 ajenda kubwa ambayo mama alizungumza wakati wa hotuba yake, ndoto yake ni kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vilivyobaki 30,000 vipate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo moja la msingi sana kwa watu wote ambao wanapenda kusoma vitu na kufanya *references* wanaweza wakanielewa vizuri zaidi. Mataifa yote kwa sasa Afrika na kwingineko watakapokuwa wanazungumzia masuala ya umeme watafanya *reference* ya *Energy Summit 300; 2025 Tanzania.* Nchi hii itasikika kote duniani kwenye sekta ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napata furaha sana nami kama mtoto wa kike, amesema vizuri sana dada yangu Mheshimiwa Shonza pale, Rais huyu ametutengenezea mazingira ambayo kila mwanamke wa nchi hii Tanzania anapata *precedence* ya kuamini kwamba anaweza akawa lolote katika Taifa hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba nitumie jukwaa hili la Bunge kutaka kumhakikishia Mheshimiwa Rais ya kwamba wanawake wote wa Tanzania hii tunamuunga mkono, tunampenda na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa wanasema kwamba mchawi wa mwanamke ni mwanamke mwenzie, siyo kweli. Wanawake walioko humu ndani wananielewa, uongo, kweli! Sisi tunapendana. Tutashirikiana na Rais wetu mwaka 2025 huu atashinda kwa kishindo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunajua 70% ya wapigakura katika Taifa hili ni wanawake. Kwa hiyo, naomba niendelee kumtia moyo Mheshimiwa Rais na naunga mkono sana Azimio hili ambalo limeletwa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Nakushukuru sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, uzuri niliwatahadharisha tangu mwanzo, kwanza majina ninayo mengi sana hapa, lakini pia majina yanaendelea kuja kwa sababu ya kazi nzuri ambazo Mheshimiwa Rais amefanya kila mtu anaona kwa kweli ana jambo la kusema. Sasa hiyo ndiyo changamoto ya leo, lakini mnajua mimi kama kiongozi wenu, huwa sijali kukesha. Tukisema tunamaliza hapa saa 12 ni sawa, mimi nitaketi nitasikiliza, lakini pia tukisema tuishie mahali pia tutaishia hapo mahali. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hapo hapo, inatosha.

**SPIKA:** Sasa sijaelewa hayo makofi yanaashiria nini?

**MBUNGE FULANI:** Tumetosha!

**SPIKA:** Aah, Wamewawakilisha hawa!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Sasa kuna wale ambao nilikuwa nimewataja majina, ngoja, si mnajua mimi huwa napenda kutenda haki? Nami kuna wale ambao nilikuwa nimeshawataja majina. Hao niliokuwa nimewataja majina hapa ni wawili, kisha Waziri anayehusika na sekta, halafu tuhitimishe, lakini mimi naweza kuruhusu majina zaidi.

Haya basi, niwahoji ili muwe mmekataa ninyi, maana mimi ninao Uradhi, lakini nimeona niwajulishe, maana naona makaratasi yanazidi kuja na majina niko nayo mengi hapa.

Waheshimiwa Wabunge, watachangia kwanza hawa wawili halafu ndiyo mtahojiwa, naona mnasubiri hii hoja ije kwenu. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ukweli ni kwamba ukilitazama Bunge lako lote, ni kwamba wote tunampongeza

Mheshimiwa Rais na maneno yaliyokwishasemwa karibu yote ni maneno ambayo Mheshimiwa Rais anayastahili. Kinachobaki ni kuendelea kulijazia nyama tu Azimio la Bunge ambalo limeletwa hapa mbele yetu kwa ajili ya Mkutano wa Afrika uliopitisha Azimio la Dar es Salaam kwa ajili ya Nishati Safi kwa Bara zima la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ule wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM, lengo la Mkutano Mkuu lilikuwa ni kumfanya Rais atulie na aendelee kuwaza mambo makubwa na matunda yake ni haya. Itazame namna Serikali ilivyojipanga katika kukaribisha ule mkutano, lakini watu wanasema kama timu inacheza, halafu kocha anamwangalia mchezaji mmoja anamwingiza na yule mchezaji anayeenda kufunga goli la ushindi, sifa kubwa zinaenda kwa kocha.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaangalia namna Mheshimiwa Rais jicho lake lilivyomwona Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwamba anafaa kushika Wizara mbili kwa wakati mmoja. Ameingia na ameenda ku-*score* goli mwishoni kabisa zile dakika za jioni Tanzania inang'ara katika dunia na Afrika kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uliwasikia viongozi wa Benki ya Dunia *(World Bank),* ulisikia Benki ya Afrika, Benki ya *East Africa*, jumla kwa pamoja wanakusudia kuchangia shilingi trilioni 110 kwa ajili ya ku-*solve* matatizo ya umeme katika Afrika, lakini haya ni mawazo bora ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini nataka kusema hapa? Kwa sababu pongezi nzito zimetolewa na Bunge hili na kwa mara ya kwanza tumeona Wabunge wa Upinzani wakiunga mkono jambo kubwa linalofanywa na Rais wetu. Tutegemee baada ya mwezi Oktoba malalamiko ya kura kuibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuwe tayari kwa sababu kazi ya uchaguzi Rais ameshaimaliza, kwa hiyo, tutegemee watu wataanza kulalamika tumeibiwa kura, tumeibiwa kura, lakini siyo kuibiwa kura, mchezaji mwenyewe aliyepangwa pamoja na

wasaidizi wake ndiyo hao mliowaona. Baraza zima la Mawaziri lina Mawaziri vijana ambao hawamwangushi Rais, lina wasaidizi wake; Waziri Mkuu pamoja na Naibu Mawaziri wamefanya kazi kubwa kabisa kuhakikisha viongozi wamefika na wameondoka wakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia kabla ya kuanza, naunga mkono Azimio hili mapema kabisa kabla ya muda. Kikubwa ambacho napenda niongelee, tumefikaje hapa mpaka Mkutano Mkuu mkubwa kama huu unafanyika kwenye nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Hayati Rais Benjamin Mkapa alijikita sana kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara na nyote ni mashahidi kipindi kile ndipo Serikali ya Tanzania iliunganisha barabara nyingi zaidi na kuanzia pale tumekuwa *champion*s upande wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapokuja kwenye suala hili la nishati, nishati safi na hii nyingine ambayo tunaitumia ya umeme ni lazima tumpe maua yake Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninayasema haya? Nakumbuka tarehe 15 Februari, 2023 tulishuhudia Mheshimiwa Rais akishuhudia utiaji wa saini ya mikataba ya kupeleka umeme kwa wachimbaji wadogo wadogo zaidi ya 336, lakini pampu za maji kwenye maeneo yetu mara nyingi tulikuwa na visima vya maji vilivyochimbwa, lakini hakukuwa na umeme; mikataba zaidi ya kupeleka pampu 399, vitongoji 1,522. Pamoja na hayo yote, ninapotaka kuelekea, uko mradi mmoja tumeupitisha hapa kitu kinaitwa gridi imara ya *4.4 trillion*.

Mheshimiwa Spika, unapoongelea *4.4 trillion only* kuboresha miundombinu ya umeme ambayo *they are already existing,* inaenda kuimarishwa ili umeme mpya huu unaokuja na huu tunaopelekwa kwa wananchi, wananchi waweze kupata umeme ule katika hali ambayo ni nzuri zaidi bila kukatikakatika na matatizo mengine ambayo yamekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyote ni mashahidi 2022/2023, tulipitisha shilingi bilioni 500 kwa ajili ya mradi wa gridi imara, na ni mradi wa miaka minne. Kwa hiyo, *4.4 trillion* achilia mbali miradi ya *REA* inayoendelea *4.4 trillion* kwa ajili ya uboreshaji tu, siyo fedha ndogo. Kwa hiyo, unaweza kuona *investment* kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya kwenye suala la nishati ya umeme. Siyo kitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024 tarehe 11 Mei amekuwa Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano uliofanyika Paris. Siyo kitu kidogo. Marais wako wangapi Dunia hii, aende yeye akawe Mwenyekiti Mwenza? Kwa hiyo, unayaona haya yamekuwa yana-*flow* mpaka *delegation* hii kubwa inakuja hapa Tanzania. Hayaja-*flow* kwa sababu ya kitu kingine, *there is something* ambacho wamekiona na hata wao wamekuja hapa wameshuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipo kwenye Bunge la Nchi za Maziwa Makuu, *theme* yetu ya mwaka 2024 ambayo tunaendelea nayo sasa hivi ilikuwa ni kuhimiza nchi za Afrika kwenye matumizi bora ya nishati safi ya kupikia, tunajivunia kilichofanyika hapa. Bahati nzuri tumekuwa mfano wa kuigwa kwenye kugawa mitungi ya gesi na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *consultancy* waliokuja kutoa maandiko yao pale walimtaja Rais Samia *specifically* kama mtu ambaye amesimama na mfano wa kuigwa kwenye kuondoa matumizi ya nishati inayohatarisha maisha na hatimaye tupo kwenye nishati safi ambayo ime-*empower* wanawake na wakataja mpaka hiyo mitungi 420,000 ambayo imeshagawiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni kazi kubwa, wote tunajua tuna habari ya barabara, tuna habari ya miradi ya maji, tuna habari ya vituo vya afya, tuna habari ya hospitali za wilaya na mambo mengine lakini kitu hiki ambacho wengi hawakuwa wakikifikiria, leo tumekiona kinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugeni huu mkubwa ambao umekuja kutuletea heshima ya kibiashara na mambo mengine kwa sababu vyombo vya Kimataifa zaidi ya 78 vilirusha *live broadcasting* ya Mkutano huu, vyombo vya Kimataifa siyo kitu kidogo. Nchi imeenda *viral* sana hii na watu wengi wamejua kilichofanyika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, kama Bunge na kama mwananchi ni lazima hili Azimio tulichukue na hata tutakapoenda huko wananchi wote wasimame na Bunge kwa sababu sisi ndiyo wawakilishi wao. Tulichokipitisha hapa tunakipitisha kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kwamba kazi ilifanywa na Mheshimiwa Rais ni kubwa, Serikali ya CCM imefanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama wenzangu waliotangulia kusema, Chama cha Mapinduzi tarehe 19 tulimaliza hili jambo. Kwa hiyo, kikubwa tuombe Watanzania, tunapoongelea 2030 kumaliza habari ya umeme vijijini na vitongojini, ni miaka mitano ijayo ambayo Rais Dkt. Samia ndio atakuwa anamaliza na maua yake tunampa kuanzia mwaka huu mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, ni lazima Watanzania wakubali kumuunga mkono. Wale ambao hawajafikiwa, tumetajiwa ni miaka mitano tu hii umeme utakuwa umefika kila sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishati safi ya kupikia tumeambiwa ni *75% by 2030* itakuwa kila sehemu. Sasa ndugu zangu Watanzania wanaotusikiliza, wanafuatilia Bunge hili, ni kitu gani zaidi unaweza ukamdai mtu ambaye amejitoa kwa kila kitu akajaribu kugusa maisha ya wanawake? Leo kwa sababu *by the way* akiwa

Makamu wa Rais alikuja na ajenda ya kumtua mwana mama ndoo, ajenda imeenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, Waziri Aweso nadhani wakati Rais anahutubia Bunge ndiyo mtu pekee aliyeambiwa, "ukinizingua, nitakuzingua," peleka maji. Tunaona maji yanaenda vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo habari ya umeme na nishati safi ya kupikia, akina mama wametolewa kwenye mikaa na kuni na *by the way* tunaotoka vijijini, tunajua watu wamekuwa wanaitwa wachawi kwa kusingiziwa, kisa tu ule moshi unamwingia mtu, wengine wamepoteza maisha, lakini vitu vyote hivi vinaenda kwisha na kila kitu kinaenda kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Watanzania, azimio tunalipitisha kama Bunge, lakini azimio hili ni lao kwa sababu Bunge ni la Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nami naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hajaja kuhitimisha mtoa hoja, nimpe fursa ya kuchangia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye ndiye kiongozi kwenye hii sekta. Pamoja na hayo, labda nimpe upendeleo aje asemee hapa mbele. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini nakushukuru pia kwa upendeleo. Siyo kawaida mchangiaji wa kawaida kuja kusemea hapa. Nakushukuru sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nami vilevile nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa neema na uzima wa kukutana hapa leo, na kwa kweli nimshukuru sana na kumpongeza sana mtoa hoja ambaye ameleta hoja hii ya pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ya Mkutano huu ambao umefanyika hapa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ni Mkutano ambao ulikuwa ni mkubwa sana na kwa kweli kila mahali na kila sehemu ambapo wakati tunafanya kazi ya kufanya maandalizi, tulikuwa tunaona mazingira ambayo yatakuwa magumu. Moja, watu waliotaka kushiriki kwenye ule mkutano, idadi yao ilikuwa kubwa sana, matokeo yake tumeshindwa hata tu kulaza watu Dar es Salaam, ikabidi wengine wanatokea Zanzibar kuja kwenye mkutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa *delegation* ya Tanzania peke yake, ambaye ndiye mwenyeji, tulikuwa tumepanga kuwa na watu 497 wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge na baadhi ya viongozi, lakini kutokana na mwitikio mkubwa ilishuka kutoka 497 hadi watu 90. Benki ya Dunia ilikuwa imeleta watu karibu 120, ilishuka mpaka watu 26 walioweza kupata nafasi. *AfDB* walikuwa na watu zaidi ya 180 na wao ilishuka mpaka watu 47 ambao tungeweza kuwaweka ukumbini na *Rockefeller* waliweza kupata nafasi tano tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni kwamba mkutano ulipata mwitikio mkubwa sana na kwa sababu hiyo, ninawashukuru sana na ninakushukuru wewe kwa kuwa na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni Bunge ambalo kazi zake kubwa mbili ni kuishauri na kuisimamia Serikali na wakati wote limekuwa likizifanya hizo kazi kwa bidii kubwa. Naomba niwaambie Watanzania kuwa, kama kuna mahali ambapo shida na matatizo ya wananchi yanazungumzwa wakati wote ni kwenye nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili Bunge ukifanya jambo baya watakwambia, na vilevile ukifanya jambo zuri watakwambia. Leo ni kielelezo kuwa Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana na nzuri na ndiyo maana umeona Bunge na wote waliozungumza toka wa mwanzo (mtoa hoja) mpaka wa mwisho aliyemalizia, utaona walikuwa wanazungumza mambo mazuri, kwa ushahidi wa mambo ambayo yanaonekana, wala hayahitaji kupigiwa ramli. Unayaona moja kwa moja yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwani *Energy Summit* ilikuwa ni nini? Ni kitu gani kilichotokea? Jambo kubwa sana ambalo tumelipata ni kuwa na mipango ya kupeleka nishati kwa wananchi milioni 300 katika Bara la Afrika. Kama unavyojua, watu milioni 600 Afrika hawana umeme na kati ya yao 85% wako Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, sasa mpango huu ambao ulipaswa kufanyika ilipaswa apatikane mtu mmoja wa kuusimamia. Mwanzo, Tanzania wala haikufikiriwa. Nataka nieleze hapa sababu mbili tu zilizofanya mkutano huu kuja Tanzania. Sababu ya kwanza, ni kuimarika kwa diplomasia yetu na Mataifa mengine Duniani. Diplomasia hiyo haijaimarishwa na mtu mwingine, imeimarishwa na yeye mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili ni kasi kubwa ya upelekaji wa umeme kwa wananchi hasa vijijini. Benki ya Dunia walivyofanya tathmini mwaka 2024 Tanzania iliongoza na matokeo yake wakasema mahali pekee tunapoweza kupeleka mpango huu basi iwe Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa msukumo mkubwa alioutoa kwenye sekta ya nishati, na pili kwa mahusiano yake yeye mwenyewe binafsi aliyoyajenga na Jumuiya ya Kimataifa na watu wengine wote ambao wana utashi mwema kwa ajili ya Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mkutano huu, kumetokea nini? Hili ni muhimu sana, watu wajue kwamba wakati ule tunapambana kutafuta fedha kwa ajili ya kusukuma miradi ya maendeleo, kuwapelekea watu umeme, kwa kweli changamoto kubwa ilikuwa ni fedha. Mkutano huu ulivyofanyika, moja, wadau wanaohusika kwa ajili ya kuweka fedha kwenye miradi ya umeme, Afrika wameongezeka, achilia mbali wale ambao tumezoea kuwasikia, Benki ya Dunia na *AFDB*.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyozungumza, kumetolewa ahadi mbalimbali za watu ambao wako tayari kushirikia kwa ajili ya kupeleka fedha ili kuweza kupeleka nishati ya umeme kwa wananchi wengi zaidi hapa Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, Benki ya Dunia imeamua kutumia mpango huu ambao tunauita *Energy Compact* kutoa dola bilioni 22, Benki ya Maendeleo ya Afrika imeahidi kutoa Dola za Kimarekani bilioni 18.2; Benki ya Maendeleo ya Kiislamu imeahidi kutoa Dola za Kimarekani bilioni 2.7; Benki ya Maendeleo ya Asia imeahidi kutoa Dola za Kimarekani bilioni 1.5; Benki ya Maendeleo ya Ufaransa imeahidi kutoa Dola za Kimarekani bilioni moja; Mfuko wa Maendeleo wa *OPEC* umeahidi kutoa Dola za Kimarekani bilioni moja; na Serikali ya Ufaransa na Rais wa Ufaransa mwenyewe Macron aliomba nafasi aweze kusalimia kwenye huu mkutano na ile *announcement* ya *pledge* ya Dola za Kimarekani bilioni moja aliitoa mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi zote za Afrika zilizokuwa zimeandaa mipango hii, mwanzo zilikuwa nchi 15, lakini kulikuwa na vigezo vya kufikiwa, baada ya mchakato kuendelea zimebaki nchi 12. Nataka nikuhakikishie kwamba, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye leo Bunge lako limeamua kutoa tamko la kumpongeza, ndiyo mpango pekee ambao Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika wamesema ni mpango pekee ambao umeandaliwa vizuri na unatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kuwa sisi wasaidizi wake tutahakikisha kuwa kazi hii ya kusimamia huu mpango inafanyika kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa huu mpango una jambo gani? Mtoa hoja ameeleza vizuri na ninataka tu nirudie kwa msisitizo. Mpango huu tumewekewa viashiria vitano. Kiashiria cha kwanza, ni upatikanaji wa umeme *(Energy Access)*. Kwa sasa hali tuliyonayo *access* ya umeme hapa nchini ni 78.4%, miaka mitano inayokuja kwenye mpango tulisaini, tutaupeleka umeme kwa 100% kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, uunganishaji umeme na wateja, leo tunavyozungumza hatua tuliyonayo tumeunganisha wateja milioni 5.2. Mpango wetu ni kupeleka kwa wateja milioni 13.5. Hili nataka nilifafanue vizuri, maana mtu mwingine anaweza kusema tuko watu milioni 60, unazungumza milioni 13?

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia wateja, kwa maana ya kwamba zile mita unazounganisha. Ukienda kwenye jeshi utakuta jeshi moja labda lina wanajeshi 2,000 lakini wanatumia mita moja. Sisi huyo tunaita ni mteja mmoja.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba tunapeleka kwa wateja milioni 13 kwa *speed* ambayo kama kusingekuwa na huu mpango tungepambana tunavyoweza tusingezidi milioni 5.2 ambayo tulikuwa nayo. Kwa nishati safi ya kupikia ambako tunataka tutoke 6.9% twende 75% kwa kipindi cha miaka mitano, na mchango wa nishati jadidifu itoke 56% iliyopo twende 65%. Hili tutalifikia bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, ninataka kutoa taarifa kwa sababu nimepata nafasi hii, kama nyongeza kwa Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa msukumo. Lile bwawa tunalozungumzia tungeweza kuwa tumelikamilisha ifikapo mwezi Mei. Ninafurahi kusema mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba mpaka leo asubuhi mitambo yote nane imekwisha kabidhiwa na mtambo mmoja wa tisa utakabidhiwa mwishoni mwa mwezi huu wa pili unaokuja na Mradi wa Julius Nyerere tutakuwa tumemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ninataka nirudie tena kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge historia itaandikwa. Ukisikia Dunia inazungumza *The Dar es Salaam Declaration* ni kwa sababu Mheshimiwa Rais alikubali ku-*host* huu mkutano.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kishoa amezungumza vizuri sana. Hii ni nyaraka ambayo watu wote na wasomi wote na kila mtu atakayekuwa anazungumza nishati Duniani na Bara la Afrika ataizungumzia. Wakuu wa nchi waliokuja; tunaweza

tukazungumza wakuu wa nchi waliokuja 22, lakini ninataka niwaambie wako wakuu wa nchi ambao *last minutes* kwa sababu ya matatizo yaliyotokea waliahirisha lakini walituma viongozi muhimu sana na ndio maana mliona lile tamko lilisainiwa na wakuu wa nchi na wakaonesha kuwa hii ni *document* yetu Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza tumeingia kwenye *record* ya Dunia kwamba sisi tumekuwa sababu, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa na tamko la Wakuu wa Nchi wa Afrika kwa nia ya kupeleka nishati ya umeme kwa watu wake. Waheshimiwa Wabunge, ninataka niwaambie kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *notes* zangu aliniambia niliongeze hili, hiki mlichokifanya leo mmetenda uungwana mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninawasikiliza Waheshimiwa Wabunge, nywele zilikuwa zinanisisimka na sababu ni moja tu. Ni kawaida sana mwanadamu kuangalia mabaya kuliko mema. Ninyi mmefanya jambo kinyume chake. Kulitafuta jema ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya na mkalisema kwa uchungu na kwa hasira kubwa kwamba ninyi mtaungana naye kusukuma mipango ya Serikali aliyonayo kwa ajili ya kupelekea umeme wananchi. Mngeweza kunyamaza, kwanza jambo lenyewe limeshafanyika wala hakuna mtu angewadai.

Mheshimiwa Spika, nyumba hii imethibitisha uungwana na ustaarabu wa kumwambia Mheshimiwa Rais, "Tuko na wewe, tunakuunga mkono, tunakutia moyo, tunakuombea, tunakutakia mema na utashi wetu kwako ni kuona Tanzania inaendelea." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo haikutarajiwa kabisa, hata kwa vyama vingine, wamesema walichofanya Chama cha Mapinduzi, kumweka mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea na Makamu wa wake Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi lilikuwa ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie tena kwa niaba ya wote tulio chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa kwenye sekta ya nishati, tutaenda kuisimamia mipango hii ili matokeo yapatikane. Mheshimiwa Rais na Bunge hili ambalo wakati wote limekuwa likitupa ushirikiano wa kuhakikisha kuwa tunapeleka umeme kwa watu wetu, tusingependa kuona haya yanabaki kuwa makaratasi, tungependa kuona yanakuwa matokeo yanayoonekana tena yasiyotetewa kwa maneno, bali yanayotetewa kwa vitendo na kuonekana hadharani bila kupigiwa debe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru sana kwa fursa hii, nawe mwenyewe tunakuombea kila la heri; na kwa kweli mtoa hoja tunakushukuru mno kwa kuja na hoja hii; na wale wote mliochangia tunawashukuru sana. Nimeona ulivyosema tuendelee kuchangia, Wabunge wote wakasema hayo yaliyosemwa hata tukisema tutarudia. Ni kama mimi ninarudia yale yale waliyoyasema, nisingependa kuwachosha kwa kuwashukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu.

Sasa nimwite mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, uje uhitimishe hoja yako.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi tena na wakati huu nikiwa nimerudi nina furaha kubwa sana ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Furaha niliyonayo ni kuona kila Mbunge aliyemo humu ndani anatamani kusema yale yote mazuri mema yaliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninayo furaha na faraja kubwa, huko nje Watanzania wanasema, "Tuseme nini Bwana zaidi ya kushukuru?" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania na sisi tunasema, "*Innallah maswaabirina.*" Hakika kila mwenye kusubiri, yuko na Mwenyezi Mungu. Nasi Watanzania tuko na Mwenyezi Mungu, tunaisubiri Oktoba, 2025 tukampitishe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote kwa kuwa walitamani kuchangia, lakini kwa sababu ya muda, nami pia sitatamani kuutumia muda wenu kwa kuwa mnadhamira na nia ya dhati na njema kwa Taifa letu kwa kuziunga jitihada za kiongozi huyu jemedari, mchapakazi, mahiri, mtulivu na mpenda maendeleo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, wamechangia jumla wachangiaji tisa, akiwemo Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Sitatamani kupunguza wala kuongeza yale yote uliyotuambia kwa sababu ulikuwa ni sehemu ya mkutano huo na umetupa mrejesho ambao kila Mbunge na kila Mtanzania ameupokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, Mheshimiwa Jesca Kishoa alisema, "Akina mama wako naye, wakina mama tuko naye." Mimi napenda kusema, akina baba wako na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; wazee wa Kitanzania wako na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; na vijana wa Kitanzania wako na mwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, watoto wa Kitanzania leo wanaokalia majengo ambayo hayakuwahi kuwepo, ya kisasa vijijini, yenye umeme na vioo ambavyo vilikuwa vimezoeleka mijini, leo wanasema wako na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile, wakulima na wafugaji wa nchi hii wako na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo, kwa sababu ya muda tunasema, "*Innallah mashwabirina.*" Tunasubiri Oktoba 2025, Mama Samia alale, sisi tuna deni naye. Kwetu sisi Watanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia kafanya. Tunakuombea kila

la heri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu akupe uzima na afya, Watanzania tumeona kwa mfano na kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi vijana ukiingia mtandaoni, nchi za jirani mitandaoni wanasema inafika lini tumpigie kura? Tunataka kuwahakikishia vijana wa nchi za jirani na wananchi wa nchi nyingine kwamba Watanzania tutaifanya kazi hiyo 2025 na ninyi mfanye kazi ya kupiga makofi na kuushangilia ushindi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuruhusu mjadala huu na kuruhusu hoja hii kuja hapa Bungeni kwa sababu wewe ni mama na una mapenzi mema na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja hii ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga kuhusu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika *(Mission 300)* kwa mwaka 2025. Wote mmeafiki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) kwa Mwaka 2025 lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa namna ambavyo baada ya kuhojiwa wote mmeafiki azimio hili, sasa nitumie nafasi hii kutangaza rasmi kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo siku ya tarehe 31 Januari, 2025, limeazimia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika *(Mission 300)* kwa Mwaka 2025. Kwa hiyo, hili sasa limekuwa Azimio la Bunge na tutamfikishia Mheshimiwa Rais kwa maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kwanza kabisa kuipongeza *TWPG* (Umoja wa Wabunge Wanawake) waliopo humu ndani kwa sababu wazo hili lilitoka kwao. Kwa hiyo, nampongeza sana Mwenyekiti wa *TWPG,* Mheshimiwa Shally Josepha Raymond (kama Mwenyekiti wetu), Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, na Katibu wetu Mheshimiwa Agnes Hokororo. Tunawapongeza viongozi wetu lakini nasi wanawake wote, na Wabunge wote. Ndiyo maana leo nimewapa Wabunge wanaume nafasi kubwa zaidi kuliko wanawake kwa sababu hili lilikuwa ni wazo la Wabunge wanawake wote kufanya hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza sana hawa viongozi wetu, lakini nawapongeza Wabunge wote kwa kazi nzuri na hasa yule ambaye ametutangulia sisi sote, Mheshimiwa Asia Halamga, kwa namna alivyowasilisha hoja kwa umahiri wa hali ya juu na ameweza kuleta mawazo yetu wanawake wote.

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri wa namna mlivyoonesha kila mmoja ana hamu ya kusema jambo, lakini siku ya leo na kwa mujibu wa kanuni zetu ilikuwa inataka tuzungumzie hilo jambo moja la uwenyeji kwa sababu ndiyo azimio linalizungumzia hivyo. Kama ingekuwa pengine ni azimio la jumla hivi, kwa kweli kila

Mbunge anacho cha kusema na hata kwenye hili kila Mbunge anacho.

Kwa hiyo, niwatambue Wabunge wote mliokuwa mmeomba nafasi kwa ajili ya kuchangia azimio hili. Ni dhahiri kila mmoja anayo kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Ya kumshukuru kwa kweli yako mengi, pamoja na kwamba na ya kumwomba kama Bunge yako mengi, lakini lazima tuoneshe shukrani kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa yale ambayo anakuwa ameyafanya vizuri, ni vizuri tukampongeza ili tumtie moyo kwamba yale anayoyafanya tunayaona. Bila shaka sisi sote tunamuunga mkono kama wawakilishi wa Watanzania. Hivyo, Watanzania wote wanamuunga mkono katika hayo.

Kipekee Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu umetoa taarifa hapa kuhusu maendeleo ya Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa kweli ni taarifa njema ambazo kama Taifa, na sisi kama wawakilishi wa wananchi tunafurahi kwamba sasa fedha zilizokuwa zinaelekea kule Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa zitahamia upande ambao kuna mambo ambayo bado kwa kweli tunatarajia Serikali iwekeze nguvu zaidi. Hasa ukitazama yakitokea hapa maswali ya Wabunge kuhusu Barabara, basi ni *TARURA* pesa, *TARURA* pesa na *TANROADS* pesa*,* *TANROADS* pesa. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, shukrani hizi ambazo tumetoa leo kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujitoa kwake kuhakikisha miradi hii ya kimkakati inaendelea na inafika mwisho. Sasa bwawa limefika mwisho, tunaamini yale mengine sasa ambayo huwa tunayauliza hapa ndani nayo kuna siku *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie, tutamshukuru Mheshimiwa Rais kwamba amekamilisha mambo mengi ambayo kwenye maeneo yetu tungetamani pia yafikiwe.

Sasa, kwa kile nilichokiona siku ya leo hapa kwa sababu watu kwa kweli mngependa kuzungumza kuhusu maendeleo ya kiuchumi ambayo kwa kweli tumepiga hatua kukusanya takribani

shilingi trilioni tatu kwa mwezi, siyo haba ni sehemu kubwa. Tumepiga hatua kubwa sana.

Kwa hiyo, pengine mwingine angependa kuwe na azimio la kupongeza kukua kwa Uchumi. Mwingine angesema kukua kwa usafiri na usafirishaji, mambo yaliyofanyika humo tuseme; na *SGR* tuseme na mambo kama hayo. Tuseme shule zilizojengwa na tuseme hospitali zilizojengwea, kwa kweli ya kusemwa yapo mengi.

Katika wiki mbili zijazo, kwa sababu wiki hii tumefanya kazi ya kutunga sheria, wiki mbili zijazo tutakuwa tunazungumzia yale ambayo yamefanyika kwa maana ya Taarifa za Kamati na yale ambayo bado kuna changamoto ni kipindi hicho.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hamkupata nafasi ya kuzungumza leo, msiwe na wasiwasi, bado ipo nafasi ya kutambua kazi kubwa sana aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika wiki mbili zijazo, kwa sababu sasa tutakuwa tunazungumzia kazi aliyoifanya kwenye kila sekta.

Kwa kadiri muda unavyokwenda kama itatokea kwamba tunahitaji siku maalumu kwa ajili ya kazi hiyo tu, ya kuzungumza basi msiwe na wasiwasi tutaiweka, kwa sababu pia huenda tunahitaji kufanya hivyo ili sisi tuseme yale ambayo Watanzania wanayasema kuhusu kazi nzuri anazozifanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Nimeona niseme hivi ili usione sasa umekosa fursa ya kuzungumza mazuri ambayo Mheshimiwa Rais amefanya kwa sababu leo hukupata nafasi. Wiki ijayo tutakuwa tukizungumza kwenye sekta mbalimbali, basi utapata nafasi ya kuzungumza kwenye sekta zinazohusika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo pia nitumie fursa hii kuwashukuru ninyi nyote kwa kazi nzuri mliyoifanya. Maana kuvumilia mpaka saa hizi nayo siyo haba. Kwa hiyo, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu, muda wetu umekwenda sana. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia katika utungaji wa sheria ahsanteni sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya. Upande wa Serikali mkiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeendelea kuutoa mara zote hoja zinapokuwa hapa na ushirikiano mnaotoa pia kwenye ngazi ya Kamati.

Kwa hiyo, bado Bunge linaendelea, lakini nimeona nitoe shukrani hizi mahususi kabisa kwa sababu katika utungaji huu wa sheria Serikali mmetoa ushirikiano mkubwa sana kwa Bunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawakumbusha kesho wote tukutane kwenye Bonanza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ananiangalia kwa makini sana, naona anawaza namna atakavyowahi sana kwenye mazoezi. Kwa hiyo, tuwahi sote huko.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa kunisikiliza na sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.45 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 3 Februari, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*